Kikao cha Kumi na Mbili - Tarehe 15 Julai, 2013

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kuwasilisha hati mezani na leo kuna wageni ambao wamekuja kuona shughuli zetu, na wageni wetu wa leo ni kama ifuatavyo: Waheshimiwa Wajumbe wageni wetu wa leo ni wageni Jimbo la Amani jumla yao ni 7 wakiongozwa na Katibu wa CCM Tawi la Sebleni, wageni hawa ni wa Mhe. Fatma Mbarouk Said Mwakilishi wa jimbo hilo la Amani. Pia katika wageni hao ipo familia yake ambao ni watoto wake watatu, kama ifuatavyo:-

Ndugu Nasour Seif
" Abdul-Malk Said Mdarus
" Ash-raf Said,

Katibu huyu wa CCM pamoja na familia ya Mhe. Fatma Mbarouk Said naomba wasimame msalimiane na Waheshimiwa. Karibuni sana muone shughuli zetu ambazo Waheshimiwa Wajumbe wanafanyaka kwa ajili yenu, karibuni sana. Waheshimiwa Wajumbe ahsanteni sana.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka 2013/2014.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Naomba pia nimkaribishe Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii.

Mhe. Farida Amour Mohammed: Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii naomba kuwasilisha Hati Mezani ya Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka 2013/2014, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 109

Ukosefu wa Huduma kwenye Soko la Samaki Chake Chake

Mhe. Nassor Salim Ali: (Kny) Mhe. Saleh Nassor Juma- Aliuliza -

Kwa kuwa inaonekana wazi kuwa Serikali ilikurupuka kuwahamisha wafanyabiashara ndogondogo wa mji wa Chake Chake kuhamia chini kwenye soko la samaki tena kwa lazima bila kujali kuwepo kwa miundombinu itakayokidhi haja kwa wafanyabiashara

hao. Na kwa kuwa eneo hilo la soko ni finyu na halina huduma za msingi za kutosha kama vile vyoo, maji na majengo ya kudumu.

(a) Je, ni lini Serikali itawasogezea wafanyabiashara hao mambo ya msingi kama vile maji ya kutosha pamoja na vyoo.

(b) Kwa kuwa sehemu kubwa ya eneo hilo la soko lilipatikana baada ya kufukia eneo la bahari Je, ni lini Serikali itaandelea na zoezi hilo ili kupanua sehemu hiyo ya soko.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. – Alijibu -

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake nambari 109 lenye sehemu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

Kwanza Mhe. Spika, naomba kumfahamisha Mhe. Mwakilishi kwamba wafanyabiashara waliondoka pale katika Soko la Chake chake kwenda kwenye soko jipya la Qatar hawakulazimishwa kama alivyouliza kwenye swali lake, na pia Serikali haikukurupuka mpango ulikiwa wa muda mrefu na ulianza taratibu toka mwaka 2011 na zuri zaidi wafanyabishara wale walifahamishwa tatizo liliopo katika Soko la Chake chake ni hasa ile *stand* ya Chake Chake.

Kwa sababu wafanyabiashara wengi waliopelekwa kule Qatar walikuwa wakiuza biashara zao katika sehemu ya *stand* ya soko la Chake chake. Sasa walifahamishwa na kwa nia njema kabisa ya Serikali kupunguza msongomano pale ndio kukabuniwa wazo la kwenda kule na wakaliwafiki na mimi niwapongeze sana wameitikia wito mzuri sana na vizuri sana wakashirikiana wakaenda tukawapimia sasa wanaendesha shughuli zao kwa kweli kwa hali inayopendeza kabisa. Baada ya utangulizi huo Mhe. Spika, sasa naomba kumjibu Mhe. Saleh Nassor Juma kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Katika kuweka mazingira mazuri ya biashara katika soko la Chake Chake, Serikali ina mpango wa kujenga soko kubwa katika eneo hilo. Ujenzi wa soko hilo utagharamiwa na mradi wa *"Market Infrastructure Value Addition Resourse Funds"* au kwa kifupi *MIVARF***.** Hata hivyo, hatua za makusudi zimeanza kuchukuliwa zikiwemo kujenga choo kipya kinachotumiwa na wafanyabiashara wa soko hilo.

Haladhalika kuimairsha miundombinu ya maji mahodhi mawili yameshajengwa moja kusaidia huduma za chooni na nyengine pia kuwasaidia upande wa sokoni. Kama mnavyofahamu kwamba kuna Serikali hivi sasa imo katika ukarabati wa miundombinu mikubwa ya maji katika mji wa Chake Chake. Kwa hivyo, upatikanaje wake pale sokoni hauna uhakika uko kwa zamani. Ndio maana umejengwa kwanza kwa hatua ya mwanzo mahodhi mawili kusaidia suala zima la upatikanaji wa maji.

(b) Michoro ya mapendekezo ya awali juu ya matumizi ya eneo hilo limeshatayarishwa kwa kushirikiana na Idara ya Mazingira. Hatua itakayofuata ni kufanyautafiti utakaowezesha kutoa taarifa za namna ya ufukiaji wa eneo hilo. Kazi rasmi ya ufukiaji itaanza baada ya kukamilika kwa utafiti unaotarajiwa kufanywa.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, mbali ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri katika jibu lake mama amesema kwamba Serikali ina mpango wa kujenga soko kubwa na la kisasa katika eneo lile.

(a) Je, ni lini mpango huo utaanza kwa kujenga soko hilo.

(b) Katika soko lile kuna barabara ambayo inatoka katika mlima na pale kunakuwa ni hatari kwa ajili ya magari kutembea katika njia ile. Je, ina mpango gani kuweka matuta ili kuondoa ajali katika soko lile.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi- Mhe. Spika, kwanza kama nilivyosema hatujatoa tarehe maalum ya kuanza ujenzi kwa sababu kama nilivyosema kwanza tunafanya utafiti kuona uwezekano wa hilo soko kuweza kujengwa sehemu ile. Nilivyosema kunahitaji kufukiwa sasa tunafanya utafiti kuona kama inawezekana kushirikiana na watu wa mazingira na hiyo michoro je, inaweza ku-*fit* pale. Ikishakubalika hivyo tutaamua tena tuanze lini lakini kwa sasa hivi hatujaamua tuanze lini kwa sababu huo utafiti bado haujakamilika.

Kuhusu suala la njia ni kweli kwamba ile njia hairidhishi pale na pana mlima mkali sana. Sasa tulifanyakazi kidogo ya kutia kifusi lakini *inshaallah* tutajitahidi kuanza kwanza alau kuanza kujaza fusi katika mwaka huu ujao wa fedha ili ile njia iweze kupitika na kupunguza yale matatizo yaliopo.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Spika, Mhe. Waziri alisema katika suala lake mama alisema kwamba kwa kuwa mpango ule ulikuwa wa muda mrefu wa kuwahamisha wafanyabiashara wale katika soko la juu na kuwapeleka katika chini. Je, Mhe. Waziri Serikali haoni isingeweza kuwajengea vyoo kwanza ili wafanyabiashara wale watakapofika pale wakapata vyoo na kuweza kujistiri, ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi- Mhe. Spika, ni kweli kwamba pale huduma za vyoo zilikuwa hazitoshelezi, kulikuwa na choo kimoja hakitoshi kilikuwa kikongwe hakitoshi. Lakini hivi sasa Serikali au Baraza la Mji la Chake Chake wameshajenga choo kipya na tayari kimeshaanza kazi na tuna nia ya kujenga chengine ili kupunguza shida hiyo walioizungumza hiyo ndio nia yetu kama nimepata vizuri swali lake.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, Mhe. Waziri katika kutoa jibu lake alisema Serikali haikukurupuka na wale wale wafanyabiashara wadogo wadogo hawakulazimishwa kwenda kule. Lakini walishauriwa na wakaona umuhimu wake na wakakubali.

(a) Hivyo, Mhe. Waziri haoni kuwachukuwa wafanyabishara wadogo wadogo kutoka kwenye eneo lote lenye watu la mji akawaweka kando kule kwenye mikandaa ni kuwafanya kuwa biasharaza zao zisiende vizuri.

(b) Kwa sababu katika mji ukitizama hapa mjini Unguja soko la samaki liko mbali na bidhaa nyengine na sehemu nyengine hata Wete hivi hivyo kuna soko la samaki mbali halafu ndio kuna soko la bidhaa nyengine. Hivi haoni Mhe. Waziri kuwachukuwa hawa wafanyabishara wadogo wadogo akawachanganya katika soko la Samaki na Samaki tunajua sifa zake katika sehemu ambayo haitoshelezi ni suala ambalo wamekwenda tu kwa sababu hawana budi lakini hawakuliridhia.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi- Mhe. Spika, nazidi kusisitiza tena kwamba Serikali haikukurupuka kulikuwa na mipango mizuri ambayo iliwashirikisha wafanyabishra wenyewe na jumuiya yao katika soko lile

kongwe la Chake Chake na kama Mhe. Salim Abdalla Hamad atakumbuka hali ilivyokuwa pale zamani sokoni Chake Chake ule uwanja ambao ulikusidiwa uwe wa magari basi nusu yake walikuwa wafanyabiashara wale.

Sasa ikawa nafasi ya maegesho ya gari ikawa haipo. Lakini ukenda hivi sasa pale pote panatumika kwa kuegesha magari tena panapendeza kabisa na utaratibu mzuri kabisa. Sasa kule nao wamekwenda wakapangiwa lakini siku zote mwanzo unakuwa mgumu na kila mtu mwanzo kidogo anakuwa mbishi.

Lakini sasa hivi ukenda Mhe. Salim Abdalla Hamad panapendeza na wenyewe wamefurahi na watu wameshazoea kabisa unakwenda soko la juu kule na ukikosa unakwenda pale. Kwa kweli inapendeza kabisa na mimi nawapongeza sana wafanyabiashara wale wa soko kuu ambao walikuwa wakifanya pale kazi nzuri kabisa na inaridhisha.

Nam. 17

Serikali Kusaidia Wananchi walioharibikiwa katika Kilimo cha Mpunga Muyuni

Mhe. Jaku Hashim Ayoub– Aliuliza-

Wakulima wa Mpunga wa Muyuni wamefanya jitihada kubwa ya kuitikia wito wa Serikali wa “Kilimo kwanza” kwa kujitayarisha kwa wakati na kupanda mpunga kama inavyotakiwa. Hata hivyo, wakulima wale hawakupata kitu msimu huu kwani mpunga wao umeharibika.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wakulima wa Muyuni walioharibikiwa na kilimo cha mpunga msimu huu.

(b) Je, kwa vile kilimo cha kutegemea mvua kimeshapitwa na wakati, Serikali ina mpango gani wa haraka kuleta Mapinduzi ya kweli ya kilimo cha umwagiliaji maji.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili - Alijibu-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 17 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatav yo:-

Mhe. Spika, kwanza naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kutufikisha leo siku ya sita ya mwezi mtukufu wa Ramadhani kuwa bado tuko katika hali ya afya na uzima.

Mhe. Spika, kabla ya kujibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye vifungu (a) na (b) kwanza naomba kutoa maelezo mafupi kuhusiana na kilimo cha mpunga kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli mwanzoni mwa msimu huu wakulima wa mpunga mwaka 2012/2013 hali ya hewa ilikuwa ni jua kali na iliathiri mipunga michanga kiasi cha kuwakatisha tamaa wakulima. Hata hivyo, mvua za masika mwaka huu zilianza mapema mnamo tarehe 04.03/2013 na kuleta mabadiliko makubwa ya hali ya hewa ya mpunga mabondeni. Mipunga imeimarika vizuri na wakulima wa Muyuni ni miongoni mwa tunawatarajia kupata mavuno yaliyo bora. Kama kutakuwa na mapungufu basi hayatakuwa makubwa.Vile vile Serikali imewasaidia sana wakulima hao kwa kuwapatia huduma za matrekta na pembejeo kwa bei za ruzuku ya zaidi ya asilimia 80. Huu ni msaada atoa motisha kwa wakulima wa mpunga ambao ndio wanaofaidika na ruzuku hiyo.

(b) Mhe. Spika, Ni kweli kilimo cha mpunga cha kutegemea ni cha kubahatisha na hakina tija ya kuridhisha na Serikali imeliona hilo zamani. Kutokana na

halihiyo Serikali ya Mapinduzi kupitia Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa kushirikiana na hawahisani imeandaa miradi na mikakati kutanua maeneo ya mabonde ya umwagiliaji Unguja na Pemba. Katika miradi hiyo, imo ile itakayopata msaada wa Korea, Tasaf, Serikali ya Marekani na mkopo kutoka *EXIM BANK*. Katika mpang huu zidi ya eka elfu tano zinatarajiwa kutayarishwa kwa kilimo cha umwangiliaji ikiwemo bonde ya Muyuni ambalo michoro yake iko tayari.

Mhe. Jaku Hasim Ayoub: Mhe. Spika, kwanza nataka kumshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa kufika kulietembelea eneo lile na kuiona hali halisi ilivyo na naomba tena Waheshimiwa Manaibu Wengine wawe mfano kama yeye wawe *physical* kutembea na kuona matatizo tusije kupata majawabu ambayo hayana kichwa wala miguu ndani ya Baraza hili.

(a) Mhe. Spika, Serikali ina mpango gani hasa wananchi wanapopata matatizo kama haya au majanga haya ukizingatia wananchi wetu kilimo ndio maisha yao.

(b) Watarajie kitu gani wananchi wa Muyuni msimu ujao wa kilimo kutokana namasikito yaliojitokeza mwaka jana na kutokana na viongozi wao wa majimbo kutafuta mbegu kwa kuwasaidia.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili- Mhe. Spika, swali la mwanzo naomba arejee.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Serikali ina mpango gani ikitokea majanga kama haya ukizingatia kilimo ndio kinachosaidia wananchi wetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili-

(a) Mhe. Spika, kutokana na majanga ambayo yanajitokeza tunaweza kusema ni suala ambalo liko kwenye uwezo wa Mwenyezi Mungu. Lakini hata hivyo Serikali baada ya kutokea majanga kama haya mabadiliko yaliotokea kwenye mabadiliko ya hali ya hewa kikubwa kinachowasaidia wakulima kuwapa ruzuku ambapo pale wakulima wanaposhindwa kuweka mbegu zao wakati wa mpando mwengine. Kwa hivyo, Serikali husaidia sana kutoa pembejeo kwa njia ya ruzuku.

(b) Suala la wakulima wa Muyuni ambao amesema kwamba kuwasaidia mbegu. Kwanza nasema Mhe. Jaku Hasim Ayoub watu wake walipatiwa mbegu kilichotokea na alichokiona yeye Mheshimiwa anafikiria hapa labda mbegu inatolewa bure. Mbegu inatolewa kwa bei ya ruzuku na hiyo tumejipanga wakati inatopokea kuwasaidia wakulima wetu kwa bei ya ruzuku, sio kuwapa bure bado Serikali hatujatangaza kuwapa wakulima bure. Kwa sababu mbegu tutanunua kama Serikali kilo shilingi elfu mbili,lakini sisi tunauza kilo shilingi mia mbili. Kwa hivyo, hiyo ni tija kumsaidia mkulima pekee.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa kulimo naomba kuongezea nyongeza ndogo katika suala la Mhe. Jaku Hashim Ayoub kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, ni kweli wananchi wetu wanapata matatizo makubwa wakati yanapotokea mabadiliko ya miongo hasa wakati ule tunapokuwa tuna mawazo ya kupata mvua na hali inapobadilika ikawa ya kiangazi. Kwa kiasi kikubwa husababisha hasara kwa wakulima wetu.

Lakini Serikali licha ya kuchukuwa jitihada za kutoa fidia mbali mbali katika masuala la kilimo ikiwemo mbegu madawa na kadhalika. Lakini pia sasa hivi utaratibu tunaofanya ili kuhakikisha wakulima wetu hawapati matatizo haya ndio maana tuna mpango kabambe wa kuendeleza kilimo cha umwagiliaji na kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri kwamba tayari tumeopata msaada kutoka kwa wenzetu ili kuhakikisha kwamba miundombinu ya umwagiliaji ina imarishwa katika maeneo mbali mbali nchini mwetu ili liwe shuluhisho ya matatizo ambayo wananchi wetu yanawakuta.

Kwa hivyo, kama alivyomuomba Mhe. Naibu Waziri, namuomba Mheshimiwa Mwakilishi na wananchi wetu wavute subira wakati huu Serikali ikilishughulikia tatizo hilo ili kupata suluhu ya kudumu. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Spika, kwa kuwa tatizo la kilimo si kwa Jimbo la Muyuni tu lakini ni kwa majimbo yote ambayo yanayo kilimo cha mpunga likiwemo jimbo la Mtambile. Na kwa kuwa wakulima Jimbo la Mtambile sehemu ya Gae la Mdungi tayari wametayarisha mashamba yao kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji shamba zipo tayari na wamechimba kisima kwa ajili ya uwagiliaji, tatizo lililobakia ni kupatiwa huduma ya umeme tu katika kisima ili kiweze kutumika kisima hicho katika umwagiliaji wa mashamba. Je, wizara yake ina mpango gani wa hivi karibuni wa kukamilika hii huduma ya umeme ili mashamba yake yaweze kutumika.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili- Mhe. Spika, swali lake nimelisikia lakini hicho kitu anachotaka kukamilishiwa sikufahamu hasa ni kitu gani.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Spika, huduma zote zimekamilika kisima kipo kimechimbwa na mashamba tayari yametayarishwa bado kupatiwa huduma ya umeme katika kisima ili huduma za kilimo zianze kutumika. Je, wizara yako ina mpango gani wa hivi karibuni wa kukamilisha huduma hiyo ili mashamba yale yatumike.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili- Mhe. Spika, mradi huu tayari jimbo la Mtabile katika jimbo lake limo kumaliza suala hili la umeme. Kwa hivyo, namuomba Mheshimiwa awe na ustahamilivu ili apate mafanikio haya.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:

(a) Mhe. Spika, Mhe. Waziri ametaja maneo ambayo yamo katika *plan* ya wawekezaji ili kuweza kupata fursa ya kulimiwa mpunga wa kumwagilia maji. Je, Mhe. Naibu Waziri na mabonde ya Kilombero na Upenja, na Pangeni yamo katika *plan* hiyo.

(b) Mhe. Spika, hivi karibuni nilisikia mlipata matrekta kwa njia ya mkopo kupitia JKT. Je, Mhe. Naibu Waziri mna *plan* gani ya kuweza kulipa hata japo nusu ya hizo fedha ili mwaka kesho tukapata mengine dhidi ya haya tuliyoyapata.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili-

(a) Mhe. Spika, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk anajua kama jimbo lake limo katika mradi wa *EXIM BANK* anajua kabisa hilo lakini anataka uhakika. Kwa hivyo, katika jimbo la Kilombero tayari mradi wa *EXIM BANK* umo katika mpango wa umwaguliaji maji.

(b) Mhe. Spika, hili la pili naomba arejee kidogo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, hivi karibuni msimu uliopita mlipata mkopo wa matrekta kwa kupitia JKT. Je, Mhe. Naibu Waziri una mpango gani wizara yako angalau kuweza kulipa tena nusu ili na mwaka kesho kuweza kupata mengi kuliko haya tulioyapata nyuma.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili- Mhe. Spika, naomba kumjibu swali lake la (b) Mhe. Makame Mshimba Mbarouk.

(b) Mhe. Spika, tatizo tuliolonalo ni kweli kwamba suala la trekta na tunajitahidi kwamba hayo matrekta tuliyoyapata hayatutoshi. Kwa hivyo, tuna mpango wa kulipa ili tupate kuongeza matrekta mengine kuwa na ufanishi wa kilimo chetu.

Nam. 89

Makumbusho ya Mkoa Kaskazini Pemba

Mhe. Bikame Yussuf Hamad- Aliuliza **-**

Kwa kuwa Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale jukumu lake kubwa ni kuenzi, kuhifadhi na kuendeleza historia ya Zanzibar kwa kutumia makumbusho ya mambo ya kale na kwa kuwa nia ya Serikali ni kuanzisha makumbusho ya Mkoa katika maeneno muhimu ya kihistoria na kuhimiza jamii kuwa na desturi ya kuyatembelea makumbusho hayo.

Je, katika Mkoa wa Kaskazini Pemba ni eneo gani ambalo linatambulika na vipi Wizara imeshajihisha jamii kuyatembelea makumbusho hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijjibu:

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 89 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale, jukumu lale kubwa ni kuienzi na kuendeleza historia ya Zanzibar kwa kutumia makumbusho. Katika kutekeleza jukumu hilo kwenye Mkoa wa Kaskazini Pemba, maeneo ya Chwaka, Tumbe na Ole Mandani ndio yanayoendelezwa na idara katika kuhifadhi historia ya Zanzibar.

Mhe. Spika, hivi sasa tayari kumeundwa kamati za wananchi wanaoishi katika maeneo hayo ya kuienzi hifadhi na kuiendeleza historia iliopo katika maeneo hayo. Serikali kwa upande wake imeanzisha vituo vya kutoa maelezo yanayohusiana na historia ya maeneo hayo, ambapo baadae vituo hivyo ndivyo vinavyofanywa kuwa makumbusho.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, napenda kumuuliza swali moja la nyongeza kama hivi ifuatavyo. Kwa kuwa maeneo haya ya kihistori ni muhimu sana na kwa kuwa maeneo ya kihistori yapo mengi Zanzibar.

a) Je, ni vigezo gani ambayo wizara yake inavizingatia mpaka ikaona hili linafaa kuwa ni histori ya mkoa.

b) Kwa kuwa katika majibu yako umesema kuwa Mkoa wa Kaskazini Jimbo la Tumbe, Chwaka ni eneo la kihistoria, ni mambo gani ambayo kuwa mmewafanya katika makumbusho yale mpaka yakatambulika hivyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, nataka nimuhakikishie Mhe. Mjumbe kwamba wizara yangu imefanya utafiti wa kutosha kwenye majengo yale ya historia yaliopo Tumbe. Umeeleza kuwa kama tulifanya utafiti. Mhe. Spika, tumeshafanya utafiti wa kutosha na tuna maradi maalum, tutakapomaliza bajeti hii kuweza kutekeleza, kuyaendeleza majengo yale na kutekeleza zaidi ufanisi wa makaburi yaliopo Tumbe na maeneo mengine yalipo kwa Pemba.

Mhe. Farida Amour Mohamed: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa maeneo ya historia ni muhimu sana na yanaiingizia serikali pato kubwa.

Je, katika bajeti hii kuna shughuli yoyote iliyopangwa kufanywa katika makumbusho hayo na ni shilingi ngapi zimetengwa kwa jumla, kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Ahsante Mhe. Spika. Mhe. Spika, nataka nimuhakikishie Mhe. Mjumbe, kama nilivyoeleza mwanzo kwamba nimefanya utafiti, lakini siwezi kukuambia ni kiasi gani, nitakuletea kwa maandishi.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Nakushukuru Mhe. Spika. Kabla ya hapo naomba nimshukuru Mhe. Naibu Waziri wangu kwa majibu yake mazuri. Mhe. Spika, kiasi ambacho kimepangwa katika bajeti hii ya mwaka 2013/2014 kwa jumla ni shilingi milioni 230.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa na mimi kumuuliza Mhe. Naibu Waziri, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri. Mhe. Spika, katika eneo la makumbusho ya kihistoria, ukiachana na kule Chwaka ambayo iko katika Wilaya ya Micheweni. Lakini katika Jimbo la Micheweni kuna mapango mengi ambayo ni ya historia.

Je, Mhe. Naibu Waziri mapango hayo anayajua na kama anayajua amejipanga vipi ili kuona kuwa kuna maeneo na mapango mazuri tu ya historia ya zamani, ili kuyaweka katika historia ya mambo ya kale nayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, tuna mpango maalum wa kuweza kufanya utafiti kwenye mapango yaliko katika Jimbo la Micheweni na mapango yenyewe ni Panga ya Mumbuni na Maziwa ya Ng'ombe.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 - Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, majadiliano yanaendelea. Lakini tulikubaliana tangu wiki iliyopita kwamba majadiliano ya jumla tumemaliza. Kwa hivyo, leo moja kwa moja naomba nimkaribishe Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Mhe. Naibu Waziri ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Subuhanahu Wataala, kwa kutuwezesha kukutana hapa asubuhi hii tukiwa wazima wa afya na salama na amani.

Pili, nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia bajeti ya wizara yangu. Vile vile nimshukuru Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati pamoja na watendaji wote wa wizara hii kwa mashirikiano makubwa tuliyokuwanayo na kuweza kuikamilisha bajeti ya wizara hii.

Mhe. Spika, kwanza naomba nianze kwa kupitia sekta ya ardhi. Mhe. Spika, kuhusu suala la kupanga matumizi ya ardhi kwa muda mrefu. Wazara yangu kwa kupitia Idara ya Mipango Miji, imeshakamilisha mpango mkuu wa matumizi ya ardhi kwa miaka 25.

Mhe. Spika, kuhusu uchache wa mahakimu. Ni kweli Mhe. Spika, tulikuwa na tatizo la uchache wa mahakimu katika Mahakama ya Ardhi, lakini Mahakama Kuu ya Zanzibar kwa kushirikiana na wizara yangu, tayari imeshateuwa mahakimu watatu. Mahakimu wawili watafanyakazi hapa Kisiwani Unguja na mmoja atafanyakazi huko Kisiwani Pemba. Tunategemea sana baada ya uteuzi huu mahakimu hawa watafanyakazi vizuri, na ule mkusanyiko wa kesi ambazo ziko katika Mahakama ya Ardhi, basi hizi zitapatiwa ufumbuzi haraka iwezekanavyo ili wananchi wapate haki ya kutumia ardhi zao kwa mujibu wa sheria za nchi.

Mhe. Spika, kuhusu madeni makubwa ya wananchi wanaodaiwa ambao wamepangishwa nyumba za serikali. Mhe. Spika, ni kweli kuwa kuna madeni ambayo wanadaiwa wananchi waliopangishwa nyumba za serikali, wananchi wasiopungua 170.

Mhe. Spika, ni kweli wananchi hao wengi wao hawalipi madeni ya nyumba hizo za maendeleo, kwa kisingizio cha kuwa nyumba hizo wamepewa na mheshimiwa Marehemu Mzee Abeid Aman Karume. Suala hili limeshaundiwa kamati na kamati tayari imeshafanya uchunguzi na imeshawasilisha ripoti yake serikalini, muda sio mrefu serikali itatoa maamuzi yanayofaa kutokana na wapangishaji hao.

Mhe. Spika, kuhusu suala la maji tangi la Konde kwamba tangi hilo ni bovu. Mhe. Spika, ni kweli mji huu wa Konde unatumia matangi mawili kwa sasa. Tangi moja likiwa ni tangi la zege ambalo ni zima halina tatizo lolote na tangi hili kwa kweli halitoshelezi huduma hiyo kwa wananchi hao wanaoishi katika mji huo wa Konde kutokana na ukubwa wa mji huo.

Mhe. Spika, wizara yangu italifuatilia ombi hili na kuhakikisha kwamba tunawajengea tangi jengine, ili wananchi hao wanaoishi katika mji huo na wao wafaidike kupata huduma hiyo toshelevu kama wanavyopata wananchi wanaoishi katika maeneo mengine.

Mhe. Spika, kuhusu upatikanaji wa maji katika Kisiwa cha Makoongwe. Mhe. Spika, Kisiwa cha Makoongwe tayari huduma hiyo ya maji safi na salama inapatikana katika vijiji vyote bila mgao, isipokuwa changamoto zilizokuwepo ni upasukaji wa mabomba yaliyokuwepo baharini na Mamlaka ya Maji Pemba pale tu ambapo inapata ripoti ya maharibifu hayo, basi mafundi wetu hufuatilia uharibifu huo na kufanya matengenezo, ili kuhakikisha kwamba wananchi hao wanarejeshewa huduma hiyo kama inavyostahiki na kama ilivyokuwa hapo awali.

Mhe. Spika, kuhusu *transformer* iliopo Muhimbini nani anastahiki kuirejesha *transformer* hiyo. Mhe. Spika, naomba nimfahamishe Mhe. Mwakilishi kwamba wanao wajibu wa kuirejesha *transformer* ni Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa kupitia Shirika la Umeme.

Mhe. Spika, naomba nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba Shirika langu la Umeme tayari limeshaagiza *transformer* na kwa sasa hivi ziko njiani, pindi tu zitakapofika hapa Zanzibar, basi *transformer* hiyo tutabadilisha na tutamuekea *transformer* nyengine mpya, ili wananchi hao waondokane na usumbufu huo.

Vile vile Mhe. Spika, ningewaomba Waheshimiwa Wawakilishi na wananchi kwa jumla, kwamba kuna raia ambao sio wema wanaofanya vitendo vya hujuma, raia hawa baadhi yao huwa wanaiba *urthing* pamoja na nyaya za kopa, jambo ambalo linasababisha matatizo makubwa kwenye *transformer* hizi kwa sababu husababisha kuungua mara kwa mara kwa *transformer* hizo. Waheshimiwa Wajumbe ningewaomba kwamba suala hili wananchi pamoja na sisi viongozi sote tuwe walinzi wa kulinda huduma hii, kwa sababu pindi linapotokea tatizo kama hili, wanaoanza kuathirika basi ni wananchi wanaotumia *transformer* hiyo. Lakini vile vile husababisha kulitia hasara Shirika la Umeme na kushindwa kuzifanya shughuli zake zinazostahiki kutokana na hasara hizo zinavyopatikana.

Kwa hivyo, nawaombeni sana kila mmoja awe mlinzi wa rasilimali hii, hii ni rasilimali ya serikali na wananchi ni wananchi wa serikali. Kwa hivyo, ningewaomba sana tushirikiane katika kulinda miundombinu yetu hii. Sio kweli kwamba wafanyakazi wa shirika watawekwa katika *transformer* zote zilizokuwepo Zanzibar, hilo ni suala ambalo haliwezekani, kwa sababu Zanzibar kuna *transformer* nyingi mno zilizokuwemo kwenye

mitaa. Kwa hivyo, ningewaomba sana, sisi tunaowekewa na kutumia *transformer* basi sisi ndio tuwe walinzi wa kuzilinda na kuzienzi *transformer* hizo.

Mhe. Spika, kuhusu usambazaji wa umeme katika vijiji vilivyokuwemo katika Jimbo la Mtambwe. Mhe. Spika, utekelezaji wa upelekaji wa huduma ya umeme katika vijiji hivyo kwa mwaka huu wa fedha 2013/2014, vijiji vya Mtambwe ambavyo vimeingizwa katika mpango wa kuingizwa umeme ni vijiji vifuatavyo. Mtambwe Mkuu, Chanjaani, Mtambwe Kinazini na Kivumoni pamoja na kukamilisha kazi ya Matuuni.

Mhe. Spika, wizara yangu kupitia Shirika la Umeme imejitahidi kwa kiasi kikubwa kuwasambazia wananchi huduma hii ya umeme katika vijiji vingi vya Zanzibar. Lakini pamoja na hayo kuna kasoro hii ambayo huwa inajitokeza mara nyingi, pamoja na serikali kujitahidi kusambaza umeme, pamoja na serikali kujitahidi kuliondoa tatizo la mgao wa umeme, lakini bado kuna tatizo la wizi wa umeme unaofanyika ndani ya nchi hii. Ningewaomba wananchi kama serikali imejitahidi kuondoa tatizo hili la mgao wa umeme na sisi tujitahidi tuondowe tatizo la wizi wa umeme. Kwa sababu Shirika la Umeme linapata mzigo mkubwa wa matumizi ya umeme, ambapo umeme mwingi sasa hivi unapotea bila ya kueleweka nani ambaye anatumia umeme huu na shirika lina wajibu wa kulipa kutokana kwa mujibu wa matumizi ambayo yametumika. Kwa hivyo, ningewaomba sana viongozi tulisimamie hili ili tuhakikishe kwamba shirika letu linabaki na uhaki katika shughuli zake ili liweze kujiendesha zaidi.

Baada ya hayo Mhe. Spika, nitamke rasmi kwamba naiunga mkono bajeti hii kwa asilimia 100, nakushukuruni ahsanteni sana. *(Makofi).*

Mhe. Waziri ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Spika, kwanza napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijaalia kuwa mzima wa afya na kupata nafasi kuja kusimama tena mbele ya Baraza lako tukufu kutoa ufafanuzi kwa masuala ambayo wenzangu wameyazungumza, kwa dhamira na kwa sababu ya kutaka kuona kwamba wananchi wetu wanapata maendeleo hasa katika sekta hii ya umeme, maji, nishati na kadhalika, nashukuru sana.

Mhe. Spika, nimepata wachangiaji wengi ambao walizungumza katika Baraza lako ni 21, ukimjumlisha pamoja na Mhe. Naibu Waziri. Wachangiaji waliochangia kwa maandishi ni 6, lakini pia hivi sasa wakati nanyanyuka kuja hapa nimepata wengine 3, kwa hivyo jumla ni wachangiaji wa maandishi 9, na mmoja hata jina lake sijalijua maana ndio nimeipokea wakati nasimama kuja kujibu hoja hapa sijamjua ni nani.
Mhe. Spika, nawata hawa ambao kwa bahati naweza kuwajua ambao ni;

1. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3. Mhe. Salim Abdalla Hamad
4. Mhe. Ali Abdalla Ali
5. Mhe. Saleh Nassor Juma
6. Mhe. Salma Mohemed Ali

7. Mhe. Hamza Hassan Juma
8. Mhe. Abdalla Mohemed Ali
9. Mhe. Farida Amour Mohamed
10. Mhe. Haroun Ali Suleima
11. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
12. Mhe. Suleiman Hemed Khamis
13. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
14. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
15. Mhe. Hassan Hamad Omar
16. Mhe. Fatma Mbarouk Said
17. Mhe. Ussi Jecha Simai
18. Mhe. Mlinde Mbarouk Juma
19. Mhe. Mgeni Hassan Juma
20. Mhe. Rufai Said Rufai
21. Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati

Mhe. Spika, waliochangia kwa maandishi kwa mujibu wa orodha niliyonayo hapa ni;

1. Mhe. Mohamed Mbwana Hamad
2. Mhe. Mrina Joel Thomas
3. Mhe. Thuwaybah Edington Kisasi
4. Mhe. Salma Mussa Bilal
5. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman
6. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa
7. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa
8. Mhe. Abdi Mossi Komb
9. Huyu aliyeleta sasa hivi kwa bahati mbaya jina lake Mhe. Spika, silioni nimejaribu kutizama sana. Lakini na yeye yupo katika hesabu atanieleza baadae, ili kuweka kumbukumbu zangu sawa.

Mhe. Spika, michango ya wizara yangu ilikuwa katika maeneo makubwa sita. Nayo ni;
1. Eneo la kwanza lilikuwa ni suala la Mahakama ya Ardhi;
2. Masuala ya upangaji wa miji na matumizi ya ardhi;
3. Suala la uchakavu wa nyumba za serikali;
4 Suala la mafuta na gesi asilia;
5. Usambazaji wa umeme vijijini na
6. Upatikanaji wa huduma ya maji

Mhe. Spika, yamo mengine madogo madogo lakini haya ndio makubwa yaliyotawala katika hoja. Mhe. Spika, nataka niseme nisije nikasahau, michango ya waheshimiwa wajumbe kwa wizara yangu ni mizuri sana na kwa kweli naithamini sana, yote karibu ina lengo la kujenga. Hakuna hata mmoja katika humu ana lengo la kubomoa, ni kwa lengo la kujenga kwa ajili ya kutafuta maendeleo ya wananchi wetu.

Mhe. Spika, nilipokaa na wenzangu wa wizara tukizungumza juu ya masuala haya nimewaambia kwamba katika hii michango iliyotolewa, bila shaka yamo mambo tunaweza kuyatekeleza, kwa hivyo nakuombeni wenzangu yale ambayo tunaweza kuyatekeleza basi tuyapangie mpango wa kuyatekeleza na yale ambayo yatatushinda basi itabidi tutizame mwakani kuja kuyafanyia kazi. Niliwaeleza kabisa kwamba tafadhali msije mkatoa ahadi ambazo hamuwezi kuja kuzitekeleza, itakuwa kama tumewarubuni Wajumbe wa Baraza ili wapitishe bajeti yetu tu, hapana tusifanye hivyo. Ahadi tutakayoitoa yoyote basi tuitowe kwamba tunaweza kuitekeleza na tusiloliweza tuseme, hili kwa mwaka huu hatuliwezi. Tusifanye utaratibu wa kujibu hoja kwa sababu ya kuwarubuni Wajumbe wa Baraza kama kwamba wapitishe tu hii bajeti upesi.

Mhe. Spika, katika hilo na yale yote waliyosema kwamba watatekeleza wameniahidi kwamba watayatekeleza na yale yatakayowashinda wameniambia kwamba haya Mhe. Waziri yatatushinda kwa mwaka huu, itabidi tuje tutizame baadae. Maana mahitaji ni mengi na uwezo wetu kiserikali ni mdogo kabisa kifedha kwa kuyatekeleza yote ambayo yametakiwa na wananchi.

Mhe. Spika, sasa naanza kupita katika kutoa ufafanuzi kwa hoja mbali mbali. Hoja ya kwanza ilikuwa inatoka kwa Mhe. Salim Abdalla Hamad, inayozungumzia suala la upangaji wa bajeti kwa Pemba na alisema kwamba kuna bilioni 1,123,000,000 kwa Ofisi ya Pemba, wakati fedha zilioko katika bajeti nzima ni nyingi sana, kwa nini Pemba wamepangiwa fedha hizo.

Mhe. Spika, nasema kwamba kwa utaratibu wetu fedha za miradi zinaratibiwa na Idara ya Mipango na Uendeshaji, makao makuu mbali mbali ya taasisi husika. Kwa hivyo, katika fedha za maendeleo kutoka SMZ katika bajeti yangu ni jumla ya shilingi bilioni 4,890,000,000 ambazo miongoni mwa hizo, shilingi bilioni 2,369,370,000 zitatumika Pemba, sio ile bilioni moja peke yake pale, ile ni ya kuendesha kazi tu kwa Ofisi Kuu ya Pemba. Lakini kuna bilioni 2,369,370,000 zitatumika Pemba katika miradi mbali mbali na bilioni 2,490,630,000 zitatumika Unguja.

Mhe. Spika, fedha za maendeleo kutoka washirika wa maendeleo ni jumla ya shilingi bilioni 64,831,030,000 ambapo miongoni mwa hizo shilingi bilioni 28,707,780,000 zitatumika Pemba za miradi ya maendeleo hizo na Tshilingi bilioni 36,123,250,000 zitatumika Unguja. Kwa hapa katika fedha za maendeleo utaona Pemba zimekwenda shilingi bilioni 28,000,000,000 na Unguja bilioni 36,000,000,000. Kwa hivyo, kwa ujumla kati ya fedha za maendeleo shilingi bilioni 77,240,030,000. Kwa Pemba zitatumika shilingi bilioni 32,310,157,000 na Unguja zitatumika shilingi bilioni 44,969,873,000. Uchambuzi zaidi wa mipango ya matumizi ya fedha za maendeleo Mhe. Mjumbe akitaka nitampa, ninao mgao huo na atauona kabisa ulivyofanywa.

Mhe. Spika, kuna suala la hoja ya Mwenyekiti wa kamati juu ya wawekezaji kuhodhi ardhi bila ya kuziendeleza. Mhe. Spika, hivi sasa wizarani kwangu mimi nina zoezi na katika zoezi hilo nimeshamaliza Kaskazini na sasa hivi niko Kusini, tunaendelea na kazi ya kuviorodhesha viwanja vyote vya wawekezaji, ambapo tunataka kujua

kwamba vingapi vimeendelezwa na vingapi havijaendelezwa na vilivyokuwa havijaendelezwa, basi tutachukua hatua ya kuvirejesha serikalini, huo ndio uamuzi wa serikali.

Mhe. Spika, halafu Mwenyekiti wa Kamati ametushauri vile vile juu ya suala la kupanga matumizi ya ardhi kwa muda mrefu. Wizara yangu kwa kupitia Idara ya Mipango Miji imeshakamilisha, mpango mkuu wa matumizi ya ardhi ambao utaweka mpango wa matumizi ya ardhi yote ya Zanzibar kwa muda wa miaka 25, bado kuutia katika utekelezaji, lakini umeshapangwa tayari.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tumsikilize Mhe. Waziri anafanya majumuisho.

Mhe. Waziri ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, Mhe. Mwenyekiti alizungumzia pia suala la uchache wa mahakimu, bila shaka anakusudia Mahakimu wa Ardhi. Hapa Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ameshasema au ameshajibu suala hili, kwamba tunashughulika na suala la kupanua Mahakama ya Ardhi hapa nchini kwa Unguja na Pemba.

Mhe. Makame Mshimba alizungumzia juu ya mtu aliyefutiwa kiwanja na kisha kurejeshewa. Mhe. Spika, mwananchi huyu alipewa hati ya matumizi ya ardhi nambari 684 huko Pwani Mchangani. Hati hiyo ilifutwa na wizara tarehe 30/06/2011.

Mhe. Spika, kuna kesi ilifunguliwa mahakamani, lakini uwamuzi wa Mahakama Kuu uliamua kuwa mwananchi huyo sio sehemu ya mshtakiwa. Kwa hivyo, serikali ilimrejeshea hati yake. Hata hivyo, kwa kuwa mahakama ni chombo huru si vyema suala hili tukalijadili sisi hapa.

Mhe. Spika, hoja nyengine ya Mhe. Makame Mshimba ni wizara isitowe ongezeko la *grass period.* Mhe. Spika, kuanzia mwaka huu na hata mlipojadili hotuba ya Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ni kwamba hakutakuwa na *grass period* kwa mtu anayepewa ardhi. Moja kwa moja akipewa ardhi ataanza kulipa *lease*.

Kurekebisha sheria ya ardhi, Mhe. Makame Mshimba amezungumza suala hilo. Mhe. Spika, wizara imeviangalia vifungu vyote vyenye utata na tayari marekebisho madogo madogo yameshafanyiwa kazi na mwishoni mwa Baraza hili tunaloendelea nalo, tutaleta marekebisho hayo kwa kusomwa kwa mara ya kwanza.

Mhe. Makame Mshimba katoa ushauri juu ya ujenzi holela. Mhe. Spika, Idara ya Mipango Miji kwa kushirikiana na Tawala za Mikoa, tayari imeshafanya mapitio juu ya mfumo wa sasa wa kutoa vibali vya ujenzi *UDCA*, na kuweka mfumo mpya chini ya *plan authority* ambao utaondoa kero nyingi zikiwemo ucheleweshaji wa shughuli za utoaji vibaji vya ujenzi.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk amezungumzia kuhusu kuchelewa kwa maposho ya wazee wa mahakama (*assessors*). Mhe. Spika, wizara kupitia mahakama imekuwa

ikiwalipa wazee hao malipo yao kwa mujibu wa fedha zinavyoingia. Kwa upande wa Unguja *assessors* wanadai malipo ya miezi miwili, yaani Mei na Juni na kwa upande wa Pemba *assessors* hawadai posho yoyote. Kwa hivyo, tunajitahidi kuona kwamba tunawalipa kwa wakati.

Hoja nyengine ambayo imetolewa na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Abdalla Moh'd Ali na Mhe. Salma Mussa Bilal ambaye alichangia kwa maandishi ni uhaba wa mahakama, majengo ya ofisi za mahakama ya Ardhi. Mhe. spika, wizara tayari imeshaweka utaratibu wa kuanzisha mahakama kwa kila mkoa, ambapo mikoa yote ya Pemba mahakama hizo zipo Wete kwa Kaskazini na Chake Chake kwa upande wa Kusini Pemba.

Kwa upande wa Unguja Mkoa wa Mjini Magharibi tayari ipo Mahakama ya Mkao hapo Majestik. Mkoa wa Kaskazini Unguja tunashukuru kwamba tayari wizara imeshapata jengo la mahakama hapo Gamba na mara baada ya kufanyiwa matengenezo mahakama hiyo itaanza kazi.
Aidha kwa Mkoa wa Kusini Unguja wizara hivi sasa inafanya matengenezo makubwa ya jengo la Mahakama hapo Koani, ambalo linatarajiwa shughuli zake mara tu baada ya matengenezo hayo yatakapokamilika katika mwaka huu wa fedha. Kwa hivyo, tumejaribu kwa kuanzia kuzitawanya hizo Mahakama za Ardhi.

Mhe. Saleh Nassor Juma, Mhe. Hamza Hassan Juma na Mhe. Jaku Hashim Ayoub wamezungumzia kiwanja kilichotolewa uwanja wa Malindi mbele ya *substation* ya umeme kwa ajili ya ujenzi wa *Petrol Station*, kwa nini kama haiwezekani ujenzi wa kituo cha mafuta kuangaliwa matumizi mengine kama vile ya maduka, mstaafu huyo wa serikali kimsaidie kiwanja hicho kimaisha.

Mhe. Spika, Mheshimiwa ambaye aliyehusika na suala hili ni swahibu wangu wa karibu sana, lakini hoja hii ndio kwanza nimeisikia ndani ya Baraza hili, yaani siijui na nimeipata hapa. Kwa hivyo, ni kweli ujenzi wa kituo cha mafuta mbele ya *substation* ya umeme ni hatari.

Sasa mapendekezo ya matumizi mengine, basi wizara pamoja na mamlaka zake italichukua na kutafakari kwa kina, kwa sababu nimelipata na huyu ni mwenzangu na tulikuwa pamoja katika Baraza hili kama walivyosema Waheshimiwa Wajumbe wenzangu na wala sifanyi kwa upendeleo, lakini najua kwamba na mimi siku moja nitastaafu na nitakuwa ninayo mahitaji muhimu na mshahara wako Mhe. Spika sitokuwa nao na maposho nitakuwa sipati. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Mwenyezi Mungu akaniwezesha kutengeneza mradi ambao utanisaidia kupata chochote kama anavyotaka kufanya huyu basi ni jambo zuri. Mhe. Spika, nitashughulikia kwa wakati.

Mhe. Spika, katika hoja hizi kuna suala moja ambalo linahusu Ndagoni, ambapo Mhe, Saleh Nassor Juma alilizungumza kuhusu eneo lililojengwa Skuli ya Ndagoni Pemba.

Kwa kweli nataka niseme wazi kama alivyosema Mhe. Mgeni Hassan Juma mimi sipendi sana kuzungumzia suala la ubaguzi, kwani ubaguzi katika nchi yetu si mzuri na wakati wake umekwisha haupo tena, hivi sasa hakuna wakati wa kubagua katika Zanzibar na wazanzibari sasa ni wamoja. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mtu anapokuwa na tatizo lake, yaani mwananchi ana tatizo la serikali la wizara hii akaja kuniona na halafu akanieleza tatizo lake na halafu kabla ya kuondoka akanitolea kipande cha CCM humuuliza cha nini na wewe ni mwananchi, nakuwa sipendi na masuala ya vyama tutakutana kwenye majukwaa huko, lakini masuala ya utekelezaji hujali chama, isipokuwa unatekeleza kwa sababu wananchi wote wanayo haki ya kupata katika nchi. *(Makofi)*

Skuli ya Ndagoni imeanza kujengwa mwaka 1992 baada ya wananchi na wazee wa vijiji vya Ndagoni, Javini, Utaani, Uyuni, Kichanjaani, Uchangani na Kunguuni kukaa pamoja na kutafakari tatizo la watoto la wao wanaolazimika kutembea masafa marefu kwa kufuata skuli katika eneo la Wesha Komba Mweupe. Mhe. Spika, baada ya mashauriano ya pamoja na Wizara ya Elimu, basi wazee wa Ndagoni walitakiwa watafute eneo la katikati ya maeneo hayo na wizara itawasaidia ujenzi.

Kwa hivyo, eneo la Javini ilipo skuli hizi za sasa ndilo lililokubalika na kuridhiwa na wote wakiwemo wenye mashamba, ambao kwa upande wa familia ya bwana Ayoub Suleiman wakati huo maamuzi yalitolewa na mama na watoto wa Mzee Ayoub baada ya kuwa yeye ameshatangulia mbele ya haki wakati ilipojengwa skuli ile.

Aidha sehemu ya skuli pia imejengwa katika shamba la bwana Hassan Baya Songoro. Mhe. Spika, skuli ilijengwa kwa makubaliano ya wananchi na mashirikiano ya Wizara ya Elimu na baada ya kumalizika wanafunzi walianza kupokelewa kutoka vijiji husika katika mikondo mbali mbali wakati wa mwaka 1999.

Wizara yangu iliombwa kutoa hati kwa ajili ya umiliki wa eneo hilo tu, yaani huo mwaka 1999, eneo lililojengwa skuli sehemu ya shamba la Mzee Ayoub Suleiman na shamba la Bwana Hassan Baya Songoro.

Mhe. Spika, eneo la skuli lililopimwa lina ukubwa wa hekta 3.3 na bado kuna sehemu ya ardhi ya shamba la mzee huyo ambaye tumemtaja bado lipo na liko wazi na wala halijachukuliwa.

Mhe. Spika, shughuli za maendeleo ya jamii katika vijiji zinazoanzishwa na jamii yenyewe mara zote hupatikana ridhaa ya wanakijiji wenyewe kabla ya mradi huo kuanzishwa.

Kwa hivyo, mimi ningelimuomba tu hawa wenye familia hizi ambazo wamehusika na suala la ujenzi wa skuli, tayari wameshatanguliza sadaka zao kwa Mwenyezi Mungu na wala tusiivunje ile skuli pale na skuli iendelee kuwepo na iwasaidie watoto na hiyo ndio *Swadakatu Jaria* na Sheikh Abdalla Juma Abdallah anajua hilo, kwa sababu ndio

ameshatanguliza huyo mbele ya haki atakuta huko benki itakuwa inaingia kila siku na yeye hana habari inaingia tu na hizi zinatoka wapi tena? Zinatoka Ndagoni hizo, ndio.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Saleh Nassor Juma kama kuna maelezo zaidi yamebakia ambayo pengine mimi sijajui maana mimi sikai huko, basi mimi niko tayari kushirikiana naye twende tukaangalie na kama kuna dhuluma imepita turekebishe na wala si vizuri kuwadhulumu watu haki yao. Lakini kama eneo lile lipo na limejengwa skuli basi mimi ningeshauri kwamba skuli iendelee kuwepo.

Mhe. Ali Abdalla Ali ameuliza kwa nini wananchi wa Selemu na Nguruweni hawapewi haki ya matumizi ya ardhi. Mhe. Spika, kufuatia agizo la Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, ardhi hizo tayari zimeshahakikiwa na sasa wizara inaandaa hati za kuwapatiwa wakulima wa sehemu hizo.

Vile vile kuna hoja ya wananchi wanaouza viwanja kwa zaidi ya mtu mmoja na hii ni hoja ambayo imetolewa na Mhe. Farida Amour Mohammed. Mhe. Spika, katika kukabiliana na udanganyifu wa mauziano ya ardhi serikali imeanzisha Bodi ya Uhaulishaji wa Ardhi. Kwa hivyo, tunawashauri wananchi kuitumia bodi hiyo katika kufanya mauziano kuepuka mitego ya matapeli, maana haya mambo Mhe. Spika yanatokea kweli.

Kwa kweli mimi nawashauri wenzangu pamoja na wananchi kwa jumla kwamba wakiambiwa kwamba kuna kiwanja kinauzwa basi ni vizuri waulize sana na wala wasione tabu kuuliza sana na wakivamia ndio wanaingia kwenye mtego huo kwamba unauziwa kiwanja.

Kwa mfano, mimi kuna jamaa yangu ameuziwa kiwanja tena ameuziwa kwa bei ndogo (chee), alizungumza na mwanangu na kumwambia nimenunua kiwanja kwa bei rahisi sana. Sasa yule mwanangu alimwambia bwana hiyo bei nina wasi wasi kwamba hicho kiwanja kinamatatizo mbona hiyo bei ni ndogo sana na mwanangu alimshauri hilo suala, hapana mimi nimeshakipata kiwanja kipo pazuri kikubwa, basi kuanza kupeleka mawe na matofali tayari mwenyewe amejichomoza na kusema kiwanja change hichi na huyo aliyekuuzia si chake kabisa na wala hamjui hata alipokimbilia na akabakia analia tu na hayo ndio mambo.

Mhe. Hamza Hassan Juma amezungumzia kuhusu suala la mwekezaji wa *Cristal Resort* kunyanyasa wananchi akiwemo ndugu Mudrik. Mhe. Spika, naijua hamu ya Mhe. Mjumbe juu ya suala hili na tayari ameshalifanyia kazi muda mrefu na wala hakuanza leo. Lakini tatizo suala hili limefunguliwa kesi mahakamani, kwa hivyo sisi tunashindwa kuendelea nalo, kwa sababu hivi sasa liko kwenye mahakama. Mhe. Spika, tunaomba chombo hicho kiendelee na kazi yake, vyenginevyo tutakuwa tunaingia muhimili mmoja wapo wa dola, na mihimili hii mara nyingi tunasema isiingiliane baina ya muhimuli mmoja na mwengine.

Mhe. Hamza Hassan Juma na Mhe. Jaku Hashim Ayoub wamezungumzia kuhusu suala la miundombinu Tunguu. Mhe. Spika, wizara imeliona hilo na miongoni mwa kazi za Idara ya Mipango Miji katika mwaka huu wa fedha ni kuratibu mpango utakaopelekea uwekaji wa huduma muhimu huko Tunguu na kwenye ukurasa wa 24 wa hotuba yangu imezungumza suala hilo kwamba tunataka tufanye hivyo.

Vile vile wamezungumza suala la ujenzi wa njia ya kurukia ndege Kigunda. Mhe. Spika, wizara tayari imeshakutana na mwekezaji huyu katika kikao kilichofanywa pamoja na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Sasa kwa vile masuala ya msingi ya usalama, leseni na matumizi ya anga hayakumalizika.

Kwa hivyo, kikao kilimshauri mwekezaji amalize kutatua masuala hayo katika taasisi zinazohusika, yaani *TCAA* na *ZAA*. Mhe. Spika, mwekezaji mwenyewe amekubali hili na ameahidi kufanya hivyo. Kwa hiyo, mara tu masuala haya yatakapokwisha basi wizara itampa mwekezaji huyu eneo husika kwa ajili ya kuendeleza shughuli zake.

Mhe. Abdalla Moh'd Ali, alizungumzia suala la ubaha wa vyombo vya usafiri katika Mahakama ya Ardhi. Mhe. Spika, ni kweli kwa sasa Mahakama ya Ardhi inakabiliwa na uhaba wa vyombo vya usafiri na vile vilivyopo vimechakaa. Hata hivyo, katika mwaka huu wa fedha mahakama imejipanga kununua gari moja na vespa kwa ajili ya kutatua masuala ya usafiri.

Mhe. Spika, pia Mhe. Mjumbe alizungumzia kuhusu wananchi wapewe elimu ya juu kuhusu umiliki wa ardhi. Mhe. Spika, tayari taasisi za ardhi zimeandaa *Program* ya Elimu ya Ardhi inayoitwa *Communication Strategies*. Lengo ni kuwafikishia wananchi wote taaluma juu ya umiliki na matumizi endelevu ya ardhi na kuanzia elimu hiyo itaanza kutolewa kwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu.

Hoja juu ya suala la ujenzi wa katika maeneo ya kilimo ni moja ya matatizo ya ujenzi holela na wizara isimamie ipasavyo suala hili katika mfumo mpya wa utoaji vibali vya ujenzi. Aidha *Master Plan* mpya ya mji ituwezeshe kuwaka maeneo mapya na kuyapanga, ili kuepusha kabisa uvamizi wa maeneo ya kilimo na hoja hii ilitolewa na Mhe. Abdalla Moh'd Ali.

Mhe. Spika, nakubaliana na hoja hiyo kwamba Mipango Miji ni muhimu na nyenzo kubwa ya uchumi. Kwa hivyo, wizara itaongeza nguvu kuhakikisha kwamba mipango yake inatekelezwa.

Hoja hizi nyengine ambazo ninazitaja Mhe. Spika, ni kwamba hivi sasa ziko kwenye pipeline ya kufanyiwa kazi na ndio maana ninajibu hivyo kwamba tunatia mkazo kuendelea na program zetu ambazo tunazo katika wizara.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub ameuliza swali moja, anasema huo mji mpya wa Zanzibar uko wapi? Uko Tunguu au wapi? Mhe. Spika, eneo la mji mpya wa Zanzibar ni eneo hili hili la Mkoa wa Mjini Magharibi, isipokuwa eneo hili litapangwa vizuri, ambapo kazi

kuanzia Saateni hadi Mpigaduri kutakuwa na sehemu ya biashara na ofisi katika *Master Plan*.

Kwa hivyo, sio kama tutakwenda kutafuta mji mwengine ni huu huu, lakini sasa tunataka *program* ya kujenga, ili uwe mzuri na *concept paper* tayari zimeshatayarishwa na hata *concept drawing* pia tayari zimeshatayarishwa na kitu muhimu hivi sasa ni kutavuta uwezeshaji wa kulitekeleza hilo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hili lisijelikaonekana ni gumu sana hili, kwa dunia ya hivi sasa. Kwa mfano, wenzetu Dar-es-Salaam tayari wanatengeneza mji kama huo Kigamboni, siku hizi kuna vyanzo vingi duniani ambavyo ukishirikiana navyo unaweza kujenga mji mzuri kabisa kama ambavyo ameshawahi kuzungumza Mhe. Hamza Hassan Juma, kwa hiyo lisijelikaonekana ni gumu na kusema ah! Hizi ni ndoto za Ali Nacha hapana, ukitaka kufanya maendeleo *think big* na uki-*think big* utafanya maendeleo. Lakini ukianza kufikiria kibanda chako tu kila siku utaishi kibandani na wanao watamalizikia kibandani, lakini *think big* na uki-*think big* basi utapata maendeleo. *(Makofi)*

Vile vile kuhusu suala la Forodha Mchanga Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Mhe. Spika, ni kwamba suala hili amelileta kwetu sisi Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, lakini hili ni suala la bandari kwa ujumla liko chini ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na wao wanayo sheria na kanuni wanazozifuata kuhusiana na masuala haya. Kwa hivyo, tuwaachie waendelee na mipango hiyo na sheria pamoja na kanuni zao wazifuate.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, katika mchango wake wa maandishi amezungumzia juu ya suala la inavyoonekana wananchi wameshahamasika sana katika kuyapima maeneo ya ardhi kuyafanya viwanja kwa ajili makaazi. Kwa hivyo, tunaomba idara husika iwe inatoa elimu ya juu ya mambo haya na kuzingatia kama vile kuacha maeneo kwa vituo vya afya, skuli na hata maeneo mengine yaachwe wazi, ili kuzingatia suala zima la mazingira.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba kumekuwa na wimbi na wananchi kujipimia na kukata viwanja na kuviuza. Kwa kweli ijulikena kwamba wanachokifanya wananchi hao ni kinyume na sheria na tuelimishane sana juu ya suala hili. Kwa kushirikiana na Halmashauri ya Magharibi idara tayari imeshasimamisha baadhi ya ukataji na upimaji huo. Hata hivyo, mwanzo ilivyokuwa na sasa ilivyo kidogo ni tofauti, yaani hivi sasa kidogo imepungua uuzaji wa namna kama hiyo na inaonesha kwamba tunaendelea.

Kwa hivyo, idara inawataka wananchi kufika Ofisi ya Mipango Miji, ili kupata miongozo ambayo itapelekea mipango bora endelevu ya ardhi. Mhe. Spika, watu wanazungumza kwamba ah! Hao Mipango Miji bwana wanakawia watakuchelesha na urasimu mwingi, basi njoo unijuilishe kwa sababu mimi nimewekwa pale *as Political Commissar,* basi nijuilishe kama umekuja na tatizo hilo na mipango yako inakuwa inakwama.

Mhe. Spika, idara itazidi kuwaelimisha wananchi katika mchakato wa kutengeneza *Master Plan* juu ya umuhimu wa mipango bora ya ardhi.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis ameuliza ni sababu zipi zilizopelekea kushindwa kutekeleza *Master Plan*. Mhe. Spika, kama nilivyosema hapo juu kwamba wizara haijashindwa, isipokuwa zipo changamoto ambazo tunaendelea kuzifanyia kazi. Kwanza ukuaji wa haraka wa mji unaosababishwa na ongezeko la kasi la watu.

Kwa mfano, mpango wa mwaka 1982 ulikusudia kuhudumia watu 300,000 ifikapo mwaka 2002. Sasa Sensa ya Watu mwaka 2002 inaonesha eneo hilo lilikuwa na watu 390,077. Lakini Sensa ya Watu mwaka 2012 inaonesha eneo la Mkoa wa Mji Magharibi lina wakaazi 593,678, ambao ni asilimia 46 ya wakaazi wote wa Unguja na Pemba, yaani karibu 50 *percent* ya wakaazi wa Unguja na Pemba wako kwenye mkoa huu. Kwa kweli *almost* inakaribia kuwa 50 *percent* ni mrundikano mkubwa sana Mhe. Spika tena ni wimbi kubwa sana na usipokuwa na kifua madhubuti basi unaweza kupasuka kifua na hiyo ndio hali halisi ya mji unavyokua.

Mhe. Spika, ukuaji huu umepelekea ujenzi holela, kwa sababu ukuaji umekuwa mkubwa, basi na ujenzi na mtu anatafuta japo kibanda mahala anajenga au anavamia na wengine ndani ya mashamba ya watu na wananchi wengine wanakuja wanalalamika kwamba shamba lako linajengwa. Kwa hivyo, hali ya uchumi ambayo haikuwezesha serikali kuweka miundombinu katika maeneo yaliyopimwa kama nilivyosema katika suala lile. Kwa kweli hivi sasa ndio tunatafuta kuweka hiyo miundombinu lakini maeneo ndiyo yamevamiwa hayo.

Pia kuna tatizo jengine la muingiliano wa majukumu wa vyombo tofauti kiutendaji na kupelekea utekelezaji mdogo wa *Master Plan.* Halmashauri za Wilaya zinatafuta mapato, kwa hiyo na wao wanafanyakazi hiyo ambayo si vizuri na wangejirekebisha, kwa sababu ni kinyume na sheria.

Aidha wizara imeona udhaifu wa suala la utoaji wa vibali vya ujenzi kushirikiana na taasisi za mikoa. Hivyo, wizara tayari imeshafanya utaratibu mpya wa utoaji vibali ambavyo utaondoa karoso zilizoonekana.

Mhe. Spika, wizara imetayarisha kanuni mpya na mfumo mpya wa usimamizi wa kanuni hizi zitaanza kutumia kuanzia mwaka huu wa fedha.

Mhe. Spika, kuna suala la sekta ya makaazi, bajeti ndogo kwa ajili ya matengenezo ya jengo la Kengeja na Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa amelizungumza suala hili. Kwa kweli bajeti ya matengenezo ya nyumba ya maendeleo Kengeja ni shilingi bilioi 1.2. Lakini kutokana na hali ya fedha serikali imetenga shilingi milioni 200 kama hatua ya mwanzo ya kulihami jengo hilo kwa kuliezeka na baadaye kuendelea na hatua nyengine ya matengenezo kwa mujibu wa fedha zitakavyoingizwa.

Tunafanya hivi kwa kufuata maelekezo ya wataalamu wa ujenzi, ambao walilitembelea jengo lile na walilitizama na kuthibitisha kwamba jengo hilo linatengenezeka. Mhe. Spika, sisi tumeamini kwa sababu kauli hiyo pia wameitoa ndani ya Baraza la Mapinduzi,

maana yake tulilizungumza kwenye Baraza la Mapinduzi na wakasema jengo la Kengeja linatengenezeka kwa hatua kwa hatua, yaani tutaanza kuezeka na halafu tutachukua ngazi ya kwanza na tutakwenda tena ngazi ya pili mpaka tutafika kwenye hatua ambayo ni nzuri.

Madeni makubwa wanaodaiwa wananchi kwa taasisi za serikali. Mhe. Spika, hoja hii Mhe. Naibu Waziri tayari ameshaijibu juu ya madeni hayo.

Vile vile kuna hoja inasema kwamba mwaka jana wewe ulisema kwamba suala hili liko juu ya meza yako. Mhe. Spika, ni kweli lilikuwa juu ya meza yangu na mimi nikalitoa kulipeleka kwenye vyombo tofauti baada ya kutoka kwenye kamati na vyombo navyo tayari vimeshamaliza kutoa maoni yao na hivi sasa kilichobakia ni uamuzi wa Baraza la Mapinduzi tu, kwa sababu mimi niliitoa na kuipeleka kule ifanyiwe kazi ionekane mapendekezo yalivyo na kilichobakia ni kuitela kwenye Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Spika, nadhani Makatibu Wakuu watamaliza siku mbili hizi hizi, kwa sababu na wao walikuwa nalo wamekaa na hawajayamaliza kutokana na wingi wa mambo ambayo wanayoyajadili. Kwa hivyo, hivi sasa baada ya muda mfupi utatoka uamuzi juu ya suala hili.

Kutokana na hali hiyo, nawaomba wale wote ambao wamo kwenye kadhia hii wawe wastahamilivu kidogo na wala si muda mrefu.

Hoja nyengine Mhe. Spika, ni kupenda wananchi wetu waishi kwenye nyumba nzuri zinazoendelea kutunzwa na kufanyiwa matengenezo. Aidha wizara izingatie kwa upana wake nyumba za Kengeja na Mtemani hoja hii pia imetolewa na Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, Mhe. Saleh Nassor Juma pamoja na Mhe. Hussein Ibrahim Makungu.

Mhe. Spika, azma ya serikali ni kuona kuwa wananchi wa visiwa vyetu wanaishi katika nyumba nzuri za kisasa na zilizo salama. Wizara italipa umuhimu mkubwa suala la matengenezo ya nyumba za Kengeja na mtemani, ili kuondosha usumbufu wowote unaoweza kutokea kutokana na ubovu wa nyumba hizo.

Matarajio ya wizara kuwa uanzishaji wa Shirika la Nyumba utasaidia kwa kiasi kikubwa na sio tu kupunguza tatizo la makaazi bali pia itasaidia kuzifanyia matengenezo yanayofaa nyumba hizo zilizopo na pia shirika litaweza kujenga nyumba za makaazi kwa wananchi wa vipato vyote.

Mhe. Spika, hii ndio maana ya kuleta Shirika la Nyumba na kama alivyozungumza Mhe. Hassan Hamad Omar, kwamba Shirika la Nyumba litasaidia sana kutatua matatizo haya. Hata hivyo, na ile Sheria yetu ya Kondomia itasaidia sana kutengeneza masuala ya nyumba hizi za maendeleo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk amezungumzia juu ya ubadhirifu wa fedha katika Idara ya Majenzi. Mhe. Spika, mhusika aliyemzungumza Mhe. Mjumbe ambaye yeye inasemekana hakuhusika na upotevu wa fedha. Kwa kweli jambo hili bado halijathibitishwa, kwa sababu kesi hii tayari tumeshaipeleka kwenye vyombo vya sheria basi tusubiri matokeo ya uchunguzi wa vyombo vya sheria na hapo ndipo tutakapojua tunafanya nini.

Nyumba za Vijiji zilizojengwa na serikali kwa kutumia matofali ya udongo sehemu mbali mbali ni za serikali au binafsi na hili ni swali la Mhe. Saleh Nassor Juma. Mhe. Spika, nyumba zilizojengwa sehemu tofauti za vijijini Unguja na Pemba kwa kutumia matofali ya udongo baadhi yake ni za serikali na nyengine ni za watu binafsi baada ya kuuziwa na serikali. Jumla ya Nyumba 161 za Vijiji zimeuzwa sehemu tofauti za Unguja na Pemba na zoezi la uuzaji wa nyumba zilizobakia linaendelea.

Je, ujenzi wa eneo la wazi Mambo Msiige unaendelea sambamba na uendelezwaji wa Hifadhi wa Mji Mkongwe Mhe. Salim Abdalla Hamad ameuliza hili. Mhe. Spika, nafikiri swali hili Mhe. Naibu Waziri aliligusa ni kwamba ujenzi unaoendelea sasa katika eneo la Mambo Msiige unakwenda sambamba na Uhifadhi wa Mji Mkongwe, baada ya ramani zao za awali kuwasilishwa ambazo zilikuwa hazikidhi uhifadhi.

Kwa hivyo, ramani hizo zilifanyiwa marekebisho makubwa kwa kushirikiana na wataalamu wa Mji Mkongwe, yaani serikali, wataalamu wa *UNESCO* na *ICOMOS* na haya ndio mashirika yanayoshughulika na hifadhi. Vile vile mikutano miwili ya masuala haya mimi binafsi nilihudhuria. Kwa mfano, Saint Petersburg Urusi nimehudhuria kwa suala hili na juzi nilipokwenda Carmbodia nilikwenda kwa suala hili hili, ili kuweza kueleza vizuri na kutosheleza na *ICOMOS* na *UNESCO* juu ya suala hili.

Mhe. Spika, ile nyumba hivi sasa ukipita ukitizama utasema kunajengwa nyumba ya kisasa kabisa kutokana na *blocks* zilizozimamishwa za saruji. Lakini juzi nilisema nilipokuwa nikijibu swali hapa tusiseme kwamba Mji Mkongwe ni mji wa nyumba mbovu. Kwa kweli jambo muhimu ni kwamba *finishing* za nyumba zile zilingane na nyumba ziliopo Mji Mkongwe lakini nyumba yenyewe iwe ya kudumu.

Kwa mfano, Mhe. Spika ningeomba Waheshimiwa Wajumbe watembelee jengo la *extension* lililofanywa katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais nyuma pale na ilianza vile vile na tulipata maswali kama vile kwamba kusimamishwa *blocks* pamoja na matofali, lakini leo ukenda kuitizama basi nyumba ile inafanana kabisa na nyumba za Mji Mkongwe.

Mhe. Spika, hata Mhe. Jaku Hashim Ayoub anajenga nyumba pale na mandhari yake inafanana na mandhari za Mji Mkongwe, ni kwa sababu *finishing* lazima ilingane na Mji Mkongwe. Skuli ya Forodhani ile haikuanzwa chini, lakini nayo imetengenezwa na kurejeshwa tena katika sura ya Mji Mkongwe na hali kadhalika na Skuli ya Tumekuja na hivi sasa Skuli ya Hamamni wanaendelea na kazi hiyo.

Kwa kweli tusiufanye Mji Mkongwe ni kwamba mji wa nyumba mbovu, isipokuwa tuufanye ni kwamba mji ambao utakuwa na nyumba zinazofanana. Kwa mfano, pale Saint Petersburg kuna nyumba za kudumu lakini sura yake ukioneshwa nyumba ile ambayo imejengwa leo na ukioneshwa nyumba ambayo imejengwa zamani zinafanana kabisa na unaweza kusema kama zote zimejengwa zamani, kwa sababu pale wana-*control* nyumba lazima ije katika sura ile ya Mji Mkongwe na wala isije kwenye sura nyengine.

Sasa huko ndani kui-*strengthen* kuifanya iwe madhubuti na mambo mengine na hilo ni suala jengine, lakini *finishing* yako lazima ilingane na nyumba ya Mji Mkongwe. Kwa hivyo, hapa ni mfano mzuri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Raisa pale nyumba, basi tembeleeni mutaiona ile nyumba imefanana kabisa na Mji Mkongwe na madirisha yake yale ya *louvers* kama nyumba za Mji Mkongwe, lakini ilianza kwa *concrete* na kila kitu.

Mhe. Spika, ndani ya Mji Mkongwe kuna majengo mabovu ambayo ni hatarishi kwa wakaazi na wapita njia kwa maisha yao na mali zao. Kwa hivyo, juhudi zichukuliwe, ili majengo hayo tasijekuleta maafa kwa wananchi Mhe. Hassan Hamad Omar amezungumza hoja hii.

Vile vile wizara kupitia Mamlaka ya Mji Mkongwe itaongeza juhudi zaidi ya kutoa elimu vipi kuyakabili majengo hayo kwa kuweza kuyatumia kuondokana na ubovu, kujua mbinu za kitaalamu, kujihami na madhara wakati serikali inajipanga kwa njia mbali mbali za kuweza kuyakarabati majengo hayo.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu amezungumzia kodi zinazolipwa kwa nyumba za serikali ni ndogo sana na anashauri ziongezwe. Mhe. Spika, marekebisho ya kodi za nyumba za serikali tayari yameshafanywa na yataanza kutumika katika mwaka huu wa fedha na tutayatangaza na wananchi watayasikia kwamba hivi sasa nyumba za serikali zinakodishwa kwa bei hizo ambazo tumeshakubaliana.

Njia ya kutoka Posta ya Shangani kupitia Wizara ya Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora imezibwa na kuwekwa vizuizi Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Mhe. Spika, serikali baada ya kuona kila siku zikenda mbele msongamano wa magari ndani ya Mji Mkongwe unazidi na kusababisha kuleta athari kubwa kwa Mji wa Urithi wa Kimataifa ambapo haikubaliki, basi imekuwa ni kero kubwa kwa wananchi na wageni ambao ni watalii.

Mhe. Spika, hata juzi tulipokwenda Carmbodia *ICOMOS* walituambia na ofisa wao mmoja alikuja hapa na akakuta kwamba magari mengi sana Mji Mkongwe na alisema Mji Mkongwe wa Zanzibar ni *Unique* na mukiuacha kupita magari namna kama ile ni tatizo. Kwa hivyo, ni vizuri mkapunguza idadi ya magari Mji Mkongwe yabakie huko huko.

Kutokana na hali hiyo, serikali imeunda kamati kubwa ya wataalamu chini ya Mwenyekiti wake Mkuu wa Mkoa wa Mji Magharibi kwa ajili ya kulishughulikia suala

hili, wataalamu hao ni kutoka Idara ya Mipango Miji, Mamlaka ya Mji Mkongwe, Shirika la Bandari, Jeshi la Polisi, Baraza la Manispaa, Idara ya Leseni na Ofisi ya Wilaya ya Mji.

Kwa kweli kamati hiyo ilifanyakazi kwa muda uliowekwa na kuwasilisha ripoti hiyo serikalini na kupata baraka na ndipo maamuzi hayo yakatolewa na haya ni maamuzi ya pamoja ya chombo maalum na tunatizama hivi sasa tunafika wapi katika hilo.

Mhe. Spika, huu utaratibu tunaoufanya sasa wa kuondoa ofisi katika Mji Mkongwe. Kwa kweli ni vyema hivi sasa ofisi zote tukaziondoa katika Mji Mkongwe na ndio maana hivi sasa zinajengwa nje ya Mji Mkongwe, ili Mji Mkongwe ule ubakie. Kwa hivyo, tuna hakika tukiondoa ofisi katika Mji Mkongwe, basi magari yatapungua na wala hakutakuwa tena na sababu ya kufunga njia. Hivi sasa ndio kuna phase out wizara moja moja tunazitoa nje kabisa zije nje ya Mji Mkongwe, ili Mji Mkongwe tuweze kuu-*preserve* vizuri kabisa.

Mhe. Hassan Hamad Omar na Waheshimiwa, wengine waliogusa suala hili la pongezi kwa lengo la kutaka kuanzisha Shirika la Nyumba na ameshauri jitihada zifanywe ili shirika liweze kuanzishwa. Mheshimiwa pongezi hizi tunazichukua na tunaahidi jitihada zitachukuliwa ili Shirila la Nyumba liweze kuanzishwa.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis, ameuliza ni lini nyumba za wakfu zitarudishwa kutokana Idara ya Nyumba.

Mhe. Spika, nyumba za wakfu zilizokuwa chini ya Idara ya Nyumba tayari zimesharejeshwa na kukabidhiwa kwa Kamishna wa Wakfu na Mali ya Amana. Lipo tatizo dogo ambalo mimi na Waziri wa Wakfu tunalizungumza hivi sasa ili tulimalize ya zile nyumba nne, hilo ndio tunaendelea nalo kwa nia ya kutaka kuwakabidhi wenyewe nyumba zao hizo. Na ile moja Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria aliyosema mmenipa kwa jina la Mali ya Amana, hapana ile isiwe hivyo, hilo nalo mimi na yeye tunalizungumza na mwenyewe alisema kwamba hilo suala tunalishughulikia. Lakini hatuna tena nyumba nyengine ya Mali ya Amana ambayo tumeiweka katika hifadhi.

Hoja ni kwamba kuna baadhi ya nyumba zinauzwa na nyengine haziuzwi, Je, kuna sheria katika hili, Mhe. Abdalla Moh'd Ali.

Mhe. Spika, kuna baadhi ya nyumba za vijiji zimepangiwa Idara Maalum hizi haziuzwi. Zile ambazo hazipangiwa taasisi maalum zinauzwa. Kwa hivyo Mhe. Abdalla kama yeye alikuwa akikaa katika nyumba ya serikali katika hizi na anaitaka, atengeneze ombi, hatuna matatizo ikiwa haikupangiwa idara maalum. Ikiwa imepangiwa idara tutamuomba radhi ebwana wee hiyo nyumba imeshapangiwa idara, lakini kama haijapangiwa idara tutamuuzia.

Je, serikali ina takwimu ya nyumba zake na inazijua maeneo zilipo? Mhe. Abdalla.

Mhe. Spika, tumejitahidi sana kujua kwamba mali bila ya daftari hughibu bila ya habari. Kwa hivyo nimejaribu sana kuzitafuta nyumba zinaweza zikawa hazijesha lakini nyingi tunazijua.

Michenzani	flat 723
Kikwajuni	flat 100
Kilimani	flat 13
Mombasa 'A'	flat 61
Mombasa 'B'	flat 30
Saateni	flat 30
Betrasi	flat 2
Gamba	flat 136
Makunduchi	flat 96
Mazizini	Nyumba za viongozi 51
Nyumba ndogo ndogo	11
Mji Mkongwe	389
Nyumba za Maendeleo Pemba ni	275
Jumla ya Nyumba zote	**1917**

Mhe. Spika, hizo ndizo tunazozijua kama zipo nyengine ambazo hatuzijui Waheshimiwa watusaidie ili tuweze kuzijua zote. Hizo ndio nyumba zetu tunazozijua sasa hivi na zoezi linaendelea kuzitafuta ili tuweze kuzijua zote kabisa na kuzipangia utaratibu maalum wa kuzitumia.

Kuna viongozi wanaokaa katika nyumba za serikali na baada ya kumaliza muda wao wa uongozi huwa hawahami na kuzirejesha nyumba serikalini, Mhe. Abdalla Moh'd Ali.

Mhe. Spika, ni kweli wapo viongozi kama hao, jitihada zinafanywa ili kuwataka wahame na wapo ambao wameanza kutekeleza agizo hilo la kuhama na wengine wanajiandaa kuhama. Sasa kwa sababu limezungumzwa hapa ni vizuri wale ambao wapo katika nyumba za serikali viongozi na wameshaondoka katika madaraka yale wazirejeshe nyumba serikalini kwa sababu baadhi ya viongozi ninao hapa bado sijawapatia nyumba na wapo *entitle* kupata nyumba na wao sijawapatia nyumba.

Nyumba za maendeleo zipo katika hali mbaya ikiwa pamoja na za Makunduchi na ushauri wa Wizara kuwashirikisha Wabunge na Wawakilishi ambao katika majimbo yao kuna nyumba hizo. Mhe. Haroun Suleiman. Ushauri wako ni mzuri na tunaupokea na tutazidi kushirikiana katika hilo.

Nyumba nyingi za serikali ni chakavu, masuala hayo yamezungumzwa na Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Saleh Nassor, Mhe. Fatma Mbarouk na Mhe. Ussi Jecha.

Mhe. Spika, ni kweli nyumba nyingi za serikali ni mbovu na jitihada za makusudi zinafanywa ikiwa ni pamojia na uwanzishwaji wa Shirika la Nyumba ili liweze kuzifanyiwa matengenezo nyumba hizo.

Wizara yangu ipo tayari baada ya bajeti hii kukaa na Mhe. Hamza Hassan Juma kuangalia namna ya kuonana na hawa wawekezaji wa Marekani, amesema wapo wawekezaji na wapo tayari kujenga nyumba. Mheshimiwa mimi nipo tayari kuhusiana na suala hili, tukae pamoja tuzungumze na tuone na tuzizame masharti, yakiwa masharti yenye muafaka tutakwenda nao, ikiwa masharti hayana muafaka hatutokwenda nao.

Sekta ya Maji, hoja kuongeza juhudi za kuwafikishia wananchi huduma ya maji safi na salama na kulinda, kutunza na kuvitafutia hati miliki vianzio vya maji. Hili lilikuwa ni swali la Mwenyekiti wa Kamati kwenye mambo ya maji.

Mhe. Spika, naomba kutoa maelezo kutokana na ushauri uliotolewa na Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliana na ujenzi juu ya jitihada ambazo wizara yangu kupitia mamlaka ya maji inafanya katika kuboresha huduma ya maji safi na salama katika maeneo ya mjini.

Wizara yangu pia mradi unaendelea sasa hivi usambazaji wa maji na usafi wa mazingira, imeelekeza nguvu zake zaidi ambayo miji mitatu ya Chakechake, Mkoani na Wete kwa upande wa Pemba. Kwa upande wa mjini Unguja kupitia mradi ambao utekelezaji wake unaanza sasa umeelekeza nguvu zake katika Mji wa Zanzibar, sambamba na jitihada za serikali katika kuboresha huduma ya maji safi na salama kwa kuongeza uzalisha maji. Aidha kwa upande wa kulinda hifadhi na kuvitafutia hati miliki vianzio vya maji. Napenda niseme kuwa wizara yangu imepokea ushauri huo na tutaufanyia kazi suala hilo.

Mhe. Ali Abdalla Ali, kupatiwa maelezo kuhusu mradi wa Mfenesini/Bumbwini, mradi wa ACRA.

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba nikubaliane na Mhe. Ali Abdalla Ali, Mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini juu ya bomba zilizopo nje katika mradi wa Mfenesini/Bumbwini. Tatizo hili lilichangiwa zaidi na ujenzi wa nyumba karibu sana na barabara kiasi ambacho kimekosekana masafa ya mita 12 kutoka katika barabara ambayo inaruhusiwa kwa kuweka miundo mbinu ya maji. Hata hivyo Mamlaka ya Maji imefanya mazungumzo na Wizara ya Mawasiliano na Miundombinu juu ya ucheleweshaji wa miundombinu hiyo baada ya ujenzi wa barabara. Hatua za awali ambazo limechukuliwa na Mamlaka ya Maji ni kuyanusuru mabomba hayo kutokana na ujenzi wa barabara ili huduma ya maji iendelea kupatikana kwa wananchi.

Ukosefu wa maji katika vijiji vya Kidundo, Chochea, Chanjaani, Makongeni, Mtambuni na Kinazini uliopo katika jimbo la Mtambwe. Mhe. Naibu Waziri alilizungumza suala hili ambalo lilizungumzwa na Mhe. Salim Abdalla Hamad.

Mhe. Mwakilishi naomba ukubaliana nasi kwamba kati ya vijiji vinane (8) kati ya vijiji kumi na moja (11) vya Shehia ya Mtambwe Kaskazini vinapata maji kupitia kisima cha Uondwe na vijiji vitatu tu alivyovitaja Mheshimiwa ndio havipati maji, hii ni kutokana na gharama kubwa za utekelezaji wa mradi wa Mtambwe Kaskazini awamu ya kwanza.

Hivyo Mhe. Spika, naomba nilihakikishie Baraza lako tukufu kwamba jitihada zinafanywa na Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji Mhe. Mwakilishi anazijua na anatoa ushirikiana wa kutosha katika kukamilisha ujenzi wa mtandao wa mabomba ya vijiji hivyo. Wafadhili wameahidi karibu dola za Marekani 60,000 (sitini elfu) ili kukamilisha ujenzi wa mtandao wa maji safi na salama. Kukamilika kwa ujenzi wa mradi huo kutawaondoshea kwa kiasi kikubwa wananchi wa vijiji hivyo tatizo la upatikanaji wa huduma wa maji safi na salama.

Kwa upande wa vijiji vya Makongeni, Mitambuuni na Kinazini, vilivyokuwepo Mtambwe Kusini. Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji imefanya juhudi za makusudi za kuwapatia wananchi huduma za maji safi na salama kupitia TASAF II. Lakini wananchi wa vijiji hivyo walichagua mradi wa barabara kwanza kama ndio kipaumbele chao, ishafika hata hivyo, bado najua jukumu la kuwapatia maji wananchi ni la Serikali ya Mapinduzi Zanzibari. Mamlaka ya Maji inafanya jitihada mbali mbali za kuwafikishia wananchi wa vijiji hivyo huduma ya maji safi na salama na tutamjulisha baada ya muda mfupi.

Tangi la maji la Konge Mhe. Naibu Waziri ameshalizungumza hili. Hoja nyengine ni kiasi gani tumetumia kwa ajili ya mradi wa Japani na kwa kiasi gani asilimia ya mafanikio ya utekelezaji wa mradi huu Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Spika, mradi wa matangi ya Welezo na Dole umetumia shilingi 32 bilioni katika kukamilisha kazi za mradi katika awamu zote mbili, *phase I* na *phase II*. Kwa ujumla mradi huu umefanikiwa kwa zaidi ya asilimia 90 ya kazi zilizokusudiwa yaani ujenzi wa miunbo, kamaf:

- Uchimbaji wa visima 11
- Ujenzi wa matangi makubwa manne (4), mawili (2) Welezo, kimoja (1) Kinuni na kimoja (1) Kijichi,
- Ujenzi wa mabomba makubwa ya nchi 6-24 kutoka visimani kwenda katika matangi yaliyojengwa na pamoja na kutoka tangini na kuunganisha mitandao mikubwa iliyokuwepo katika mtandao wa maji.

- Uimarishaji wa kituo kikubwa cha Saateni na ujenzi wa mitambo ya kuyatia dawa maji yanayokwenda kwa wananchi.

Mhe. Spika, wakati mradi huu unaandaliwa mwaka 2010, mahitaji ya maji yalikuwa ni lita milioni 48 kwa siku. Baada ya kukamilika kwa mradi uzalishaji ulikuwa ni lita milioni 40. Changamoto ya mradi huu ni uchakavu wa miundombinu ya maji ambayo inapelekea upotevu wa asilimia 35 ya maji yanayozalishwa ambayo ni sawa na lita milioni 14 pamoja na ongezeko la watu. Katika kukabiliana na changamoto hizo ndio maana tumeanzisha mradi wa uimarishaji wa miundombinu ya maji unaolenga kurekebisha hali hiyo. Mradi huo unaanza kazi hivi sasa hivi, tayari tumeshasaini mkataba ili kuondosha tatizo la maji katika mji wa Unguja. Maji ya mji wa Unguja hayatopatikana kwa kutumia matangi ya Welezo. Kuna jitihada zaidi zitekelezwe na

visima zaidi vichimbwe kwa kuingizwa katika magangi yale ambayo yameshajengwa hivi sasa hivi.

Mhe. Hamza Hassan amezungumza kuwe na utaratibu wa kupeleka miundombinu ya maji kudaidia majimboni badala ya kupeleka magari ya maji mwezi wa Ramadhani.

Mhe. Spika, najua alilisema kwa nia safi hili na kwamba suala la kupeleka magari ya maji katika maeneo ambayo huduma hiyo ina upungufu au haipatikani ni hatua ya dharura ya serikali katika kutekeleza jukumu lake ili kuwafikia wananchi wake huduma ya maji safi na salama.

Lakini napenda kumkumbusha Mheshimiwa kwamba pamoja na Baraza lako Tukufu kwamba Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji bado hawajasita katika kuwatafutia suluhisho wananchi ambao hawapati huduma hii au wanaipata lakini haitoshelezi. Ndio maana tunafanya juhudi hiyo ya kupeleka magari ya maji hasa katika Mwenzi huu Mtukufu wa Ramadhani, maana mwezi Mtukufu una nidhamu yake, lazima magharibi ufutari, hakuna namna nyengine, madamu umefunga lazima ufutari na unakula kwa wakati. Kwa sababu kufunga watu wanachoka sana kwa hivyo ndio maana tunawapelekea maji kuwapunguzia ile mihangaiko ya kutafuta maji katika mji.

Hoja ya upatikanaji wa maji katika Hospitali ya Makoongwe kwa kiasi fulani Mhe. Naibu Waziri ameshalijibu hilo.

Hoja ya ukosefu wa huduma ya maji katika kisiwa vya Uvinje ni lini huduma hiyo itakuwa ya kutosheleza katika kisiwa hicho. Mhe. Farida Amour Mohammed, nimelizungumza hili.

Mhe. Spika, changamoto za huduma ya maji katika kisiwa cha Uvunje zinatokana na ubovu wa tangi la Raha na ujenzi wa barabara ya Ukunjwi unaoendelea. Kwa kawaida kisiwa hichi kinapata maji kutoka mtandao wa Gando kupitia kisima cha Kijuki. Bomba linalohudumia Kisiwa hicho limepita katika kisiwa cha Fundo, uhakika wa upatikanaji wa maji katika kisiwa hiki unategemeana na kukamilika na ujenzi wa barabara hiyo na ukarabati wa tangi la Raha.

Hatua ya utengenezaji wa miundo mbinu ya maji sambamba na ujenzi wa Barabara zinaendelea. Tumepata pale tulikuwa tunatafuta *plate* ya kulitengeneza lile tangi la Raha. *Plate* tumezipata Alhamdulillah lakini kuna vifaa vichache vinahitajika. Pia tupate wataalamu, vijana wetu wale wa maji pale Pemba tumewapeleka kupata mafunzo kidogo ya kuunga lile tangi ambalo linavuja hivi sasa hivi juu ya kilima pale Raha, hilo tunategemea kwamba litaondoa tatizo laji katika maeneo hayo. Barabara nayo ikimalizika, lakini tunavyojua barabara zile za Pemba sasa hivi zina mitihani. Lakini Ishallah Mwenyezi Mungu akipenda mtihani huo utaondoka na tutafanikisha suala hilo vile vile.

Kuna mafunzo ya Mamlaka ya Maji Arusha, imewataka watendaji kufanya kazi nzuri kwa yale waliyojifunza ili kuleta ufanisi katika Mamlaka hiyo, Mhe. Salma Mussa Bilal ametupongeza, kwa kupeleka watu kupata mafunzo Arusha ya maji. Pongezi zimepokelewa.

Pongezi nyengine ni ZAWA kwa jitihada kubwa wanazozichukua, tunaiomba serikali kututafutia njia mbadala za kutatua matatizo ya maji licha ya ongezeko kubwa la watu nchini. Mhe. Shadiya Mohamed Suleiman.

Tunatoa shukurani zetu za dhati kwa Mheshimiwa kwa kuziona jitihada za serikali licha ya changamoto zilizokuwepo. Serikali kupitia Wizara yangu imeliona hilo na inaendelea na jitihada za kuhakikisha kwamba inawapatia maji wananchi wake kupitia miradi iliyokuwepo, inayoanza sasa pamoja na kubuni miradi mbali mbali yenye ufadhili wa serikali wa Shirika wa Maendeleo pamoja na nguvu za wananchi. Kipaumbele cha Wizara yangu kwa mwaka wa Fedha 2013/2014 ni maji. Ambapo bajeti hii tunayoizungumza naomba ipitishwe asilimia 70 ya bajeti hii inashughulikia masuala ya maji. Masuala ya umeme alhamdulillah tumefika pazuri sasa hivi tunataka maji, hilo ndilo tulilolitikia mkazo, ndio maana asilimia 70 ya bajeti yangu hii itakayopitishwa hapa ni maji, asilimia 30 ndiyo mambo mengine, kwa sababu nataka tutatue tatizo la maji.

Kitu gani kinachopelekea ukataji wa miti ya wananchi bila ya kupewa taarifa na kutolipwa fidia ya mazao hayo kule Wete Pemba, Mhe. Farida Amour Mohammed.

Wizara yangu inashirikiana na uongozi wa Serikali ya Wilaya kupitia Masheha katika kuwasiliana na wananchi katika maeneo mbali mbali ambayo mradi unaendelea kwa bahati mbaya baadhi ya wananchi hawafiki kauitikia wito huo kwa sababu mbali mbali, ikiwemo hoja ya kudai sehemu inayotaka kutumika kwa mahitaji ya mradi ni kubwa. Hivi wananchi hao hukataa kushiriki katika kuona tathmini hiyo inafanywa hali hii inazorotesha kazi za mradi.

Najua limetokea tatizo moja Mhe. Farida, Mhe. Spika, kwa idhini yako namjibu kwamba eneo lile ni kubwa na halafu kuna maeneo ambayo yamefanyiwa tathmini hayakuwemo lakini sasa hivi yameingizwa. Hilo tuko tayari kulikabili na kufanya malipo kwa haya maeneo mapya yaliyoingizwa katika mradi ule.

Hoja ya ukarabati wa mabomba ya maji Bububu na Pemba Air Port, Mhe. Hussein Ibrahim Makungu.

Mhe. Spika, ni kweli Pemba Air Port lilikuwepo bomba ambalo lilikuwa na matatizo ya uvujaji wa maji katika kifaa cha *fire hydrate* ambacho huwa kinatumika kwa kuhudumia kikosi cha Zimamoto. Kiukweli bomba hiyo sasa haimwagi tena maji baada ya kufanyiwa matengenezo mwezi mmoja sasa.

Pia suala la Bububu ni kweli ulitokezea wakati watengenezaji wa barabara kwa kuweka kifusi. Bomba hizo ziliharibika lakini hatua za utengenezaji wa bomba kubwa tayari

zimechukuliwa na mara tu baada ya kupata taarifa hizo. Kwa upande wa bomba ndogo ndogo ZAWA wanaendelea na jitihada ya kuzitengeneza kila wakapopatiwa taarifa.

Nampongeza sana Mhe. Hussein kwa jitihada zake alizoifanya katika kukitia kifusi njia hii.
Tunamshauri kwa kufanyia kazi katika kuongeza juhudi za kutoa taaluma kwa wananchi, suala zima la kuchangia huduma ya maji. Ni vizuri tunapofanya matengenezo yetu Waheshimiwa Wawakilishi tufikirie kama mahala kumepita mabomba ya maji basi tushirikiane na ZAWA ili kujua tutalishughulikia vipi suala la matatizo ya maji. Ni kazi nzuri amefanya Mhe. Hussein katika eneo lake.

Hoja kisima cha maji cha misufini kimeharibika na kutoa pampu lakini pampu hii ni ndogo haipeleke maji tangini na hata kwa wanchi wa karibu. Aidha wafanyakazi waliokuwepo katika kituo hicho wapo kwa muda mrefu lakini hadi sasa hawajaariwa je, ni kwa sababu gani? Mhe. Mlinde Mbarouk Juma.

Ni kweli kisima hichi kilipata hitilafu hivi karibuni kwa kuungua pampu iliyokuwa ikitumika. Wizara yangu ilichukua hatua za haraka na dharura kwa kufanya matengenezo pampu ilizokuwa nazo na kuirejesha huduma hii muhimu kwa wananchi. Sasa tupo katika matayarisho ya kupata pampu mpya yenye uwezo sawa na uzalishaji wa kisima kwa kuwafikishia wananchi.

Kwa upande wa wafanyakazi wa kisiwa hicho kuwa hawajaajiriwa hadi sasa hii ni kwa sababu chimbuka la wafanyakazi hawa wanatokana na utekelezaji wa miradi ya wananchi kwa mashirikiano na waheshimiwa Wawakilishi, Wabunge na Madiwani na hatimaye wananchi kuchukua nafasi ya kuvilinda vituo vya maji. Jambo zuri kabisa nawapongeza sana Wawakilishi hata hivyo Mamlaka imeanza zowezi la uhakiki wa wafanyakazi hao. Endapo Mamlaka itakuwa na uwezo wa kuwaajiri haitosita kufanya hivi, tunawahakiki sasa hivi tuwajue maana ni wengi, hawapo hapo tu Bungi wapo katika maeneo mengi wanafanya kazi ni wengi sana.

Mhe. Salma Mohammed Ali, amezungumza kuwasaidia mafundi wa Mamlaka ya Maji kupata posho.

Napenda kutoa shukurani za dhati kwa Mhe. Mwakilishi kwa kuziona jitihada zinazofanywa na mafundi wa ZAWA na tunapenda kusema tumepokea ushauri huo. Mamlaka ya Maji inautaratibu wa kuwalipa posho kwa mafundi wake na tutajitahidi kuwaongeza maposho kadri hali ya Mamlaka ya fedha itakavyoruhusu.

Mhe. Hassan Hamad Omar, amezungumzia suala la ukosefu wa maji eneo la Forodhani.

Mhe. Spika, kiukweli Forodhani parking ni miongoni mwa eneo la Mji Mkongwe ambayo yanapata huduma ya maji vizuri sana. Nimuhakikishie Mheshimiwa kuwa tunaendelea kushirikiana vyema na watendaji wanaohusika na usimamizi wa eneo ili kuangalia tatizo hili kwa kulipatia ufumbuzi wa kuduma ili huduma hiyo muhimu ya maji

iweze kurejea kupatikana kwa uhakika na kuleta haiba nzuri ya mji wetu Mkongwe wa Zanzibar.

Mhe. Spika, sitaki kufanya fumbo hapa, ila nataka kusema kwamba deni la maji pale ni kubwa na kwa sababu hiyo ndiyo tukalazimika kukata. Kwa hivyo sasa hivi tunashauriana na Wizara husika ili tulipe lile deni ili tuweze kurejesha huduma ya maji, lakini maji yapo hayana matatizo pale, deni tu ni kubwa. Kwa hivyo tukishirikiana kwa hilo maji tutayarejesha.

Pamoja na juhudi iliyofanywa na Mheshimiwa Mwakilishi na Mbunge kwa kupeleka huduma ya maji katika Kijiji cha Jitenge bado huduma hiyo haijakuwa ya uhakika katika kijiji hicho. Ni lini huduma hiyo itakuwa ya uhakika kijijini hapo. Mhe. Hassan Hamad Omar

Mhe. Spika, kweli kupitia mfuko wa jimbo walifanya juhudi za kulaza mabomba ya nchi mmoja kutoka jitenge hadi maziwani bila ya ushauri wa ZAWA Makamo Makuu. ZAWA tawi la Pemba itarekebisha kosa hilo la kulaza bomba la nchi moja na kuweka bomba la nchi moja na nusu ili kuboresha huduma ya maji kwa kijiji cha Jitenge. Kazi itakamilika katika robo ya kwanza ya mwaka wa Fedha 2013 hii ni ahadi, ndiyo ile niliyowambia watu wangu tuweni ahadi mtakayoiweza hapa wamenihakikishia kwamba hii wataifanya, wataweka bomba la nchi moja na nusu katika eneo lile.

Hoja ya kuwa muda mrefu sasa wanachi wa Moga na Kinyasini wamekosa huduma ya maji safi na salama iliyotokana na ahadi ya muda mrefu ya kuchimba kisima ameitoa hoja hiyo Mhe. Ussi wa jimbo la Chaani.

Mhe. Spika, wananchi hao watanufaika na mradi wa Rasilhema wa uchimbaji wa visima nchini. Miongoni mwa maeneo yaliyopangwa ikiwemo Shehia ya Moga na Kinyasini ambapo ndani ya bajeti ya mwaka huu wa Fedha wananchi watanufaika na huduma ya maji safi na salama.

Mhe. Spika, bajeti hii ni ya miezi 12 kwa hivyo matumizi yetu yanakwenda ndani ya miezi 12, tutajitahidi kurekebisha kama tunavyotoa ahadi katika haya maeneo kwamba tunatoa ahadi tukiingiziwa fedha vizuri bila shaka nategemea itakuwa hivyo. Kwa hivyo tustahamili, tusubiri kidogo ingawaje maji hayastahamiliki lakini tutafanyaje, hatuna la kufanya lazima itatubidi tustahamili, tusubiri ili kuweza kuwafikishia maji lakini najua kwamba mradi wa Rasilhema upo tayari na umeshaanza kuchimba visima na yata yaye alipozungumza na miye nilimwambia kwani hawajaja huko Rasilhema kwa sababu najua Rasilhema wanachimba visima katika maeneo haya yenye matatizo kwa hivyo tumemuweka katika mradi huu.

Sekta ya Nishati, Mhe. Mwenyekiti, wa Kamati ametoa pongezi kwa kufanikisha miradi ya ujenzi wa njia ya pili ya umeme na mradi wa uimarishaji wa njia za umeme pamoja na uondoshaji wa *transformer* iliyopo Chakechake sokoni Pemba, pongezi tunazipokea.

Mhe. Mwenyekiti, ameshauri kwamba wafanyakazi katika ufungaji wa mita za TUKUZA katika mwaka 2013/2014 tuongeza wafanyakazi ili kupunguza madeni ya wateja ya 22.9 milioni. Madeni kweli tunayo na mbele huko nitazungumza, ushauri huo tumeupokea kuongeza watu.

Suala la utafutaji wa mafuta halikuzungumza sana katika kitabu cha Bajet, je, suala hilo lipo katika hatua gani, huyo alikuwa ni Mhe. Salim Abdalla Hamad, Mhe. Saleh Nassor Juma, Mhe. Mlinde Mbarouk Juma, Mhe. Mgeni Hassan Juma, Mhe. Hamza Hassan Juma na Waheshimiwa wengine waliochangia katika hili.

Mhe. Spika, kwanza nataka nimjibu Mhe. Mlinde alipokwenda Uholanzi aliambiwa Waziri alisema kwamba atakuja hapa lakini mbona hajaja. Nataka Mhe. Mlinde afahamu suala lile nilikuwa sijaja kwa sababu sikuwemo ndani ya ile *delegation*. Alipokuja Balozi wa Uholanzi Ofisini kwangu kuniona alinambia kwamba anataka kujenga uwezo kwa Waheshimiwa Wabunge wa Jamuhuri ya Muungano juu ya suala la mafuta na atawapeleka Uholanzi. Tukamuomba sio Wabunge peke yao uchukuwe na Waheshimiwa Wawakilishi. Ndio Waholanzi wakaleta ombi hapa kwa Baraza lako wa Wawakilishi kwamba watafutwe watu waende katika kutizama uzoefu juu ya suala la mafuta kule Uholanzi, hilo ombo lilikuja. Nashukuru Mhe. Spika, ukalitekeleza. Nilipokuwa kule na Mhe. Rais Kikwete yule mtu wa Shella akaniuliza eebwana weee vipi! katika suala la mafuta Unguja utakuja? Nikamwambia ntakuja ukinialika. Nadhani mwenyewe alitafsiri mualiko aliokuleteeni nyie na mimi niwemo. Mimi sikuwemo, sikuulizwa, ndio imeshamalizika. Hiyo ndio hali halisi ilivyo.

Mhe. Spika, majibu ya hoja ya mafuta na gesi. Naomba kukiri kwamba suala hili halikutolewa maelezo ya ndani katika hotuba hii ya kwa kufupisha ukubwa wa kitabu na kuzingatia kuwa maelezo hayo tayari yako bayana. Hata hivyo kwa sasa suala hili limeundiwa Kamati maalum inayongozwa na Wanasheria Wakuu wa Serikali mbili, SMZ na SMT. Kamati hiyo imeundwa na Mhe. Waziri Mkuu wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa madhumuni ya kutoa muongozo ambao utawezesha Zanzibari kusimamia kikamilifu suala la mafuta na gesi katika kipindi hichi cha mpito mpaka kumalizika kwa mchakato wa Katiba mpya. Kimsingi katika rasimu ya Katiba hiyo suala la mafuta na gesi tayari limeshaondolewa katika orodha ya mambo ya muungano. Lakini kuna mambo lazima tuyaanze sasa hivi ndio Kamati ya Wanasheria inatizama sheria ili kutoa uwezekano wa sisi kuanza mambo yetu ya mchakato wa kutafuta mafuta hapa kabla hata huo mchakato wa katiba mpya haujawa tayari.

Mhe. Spika, naomba kuchukua nafasi hii kuwatosheleza watoa hoja waliotaka kujua lini mafuta yatachimbwa. Kwa kuwahakikishia kuwa mara tu baada ya utaratibu huo kukamilika wizara yangu itachukua hatua za kuliarifu Baraza hili Tukufu wa wakati huo huo kuanza rasmi kuanza kulishughulikia suala la mafuta na gesi kikamilifu kwa kuwaruhusu wawekezaji. Sisi wenyewe Wazanzibari kuanzia shughuli za utafiti na hatimaye uchimbaji wa rasilimali yetu ya mafuta na gesi kwa maslahi ya Zanzibar.

Napenda kuwahakikishia tena wananchi wa Zanzibar kwa sasa Wizara hii inajitayarisha kikamilifu kwa kujijengea uwezo kwa madhumuni ya kulimamia suala hili kikamilifu kama nilivyoeleza kabla. Ni vizuri kukumbuka kuwa hitilafu katika maslahi ya Zanzibar kwenye mafuta na gesi ndio kitakachowanyamazisha wananchi wa Zanzibar katika suala la mafuta na gesi lirudishwe kwa Wazanzibari. Na uzuri kuhakikisha kuwa hitilafu hizo inapata suluhisho la kudumu ndipo tuanze shughuli hizo rasmi za maslahi ya mafuta. Hiyo ndio hali halisi ya mafuta. Nategemea Wanasheria wetu watoe maelekezo ya kisheria ili tuanze kazi ya kutafuta mafuta. Kwa hiyo Kamati sasa hivi imeshaanza kazi.

Hoja ya Mhe. Saleh Nassor Juma, Mhe. Abdalla Mohammed Juma, Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa na wengine, wameuliza kuna mpango gani wa sera katika kujiimarisha kuwa na nishati mbadala ya uhakika kuzalisha umeme Zanzibar badala ya kutegemea umeme kutoka Tanzania Bara.

Mhe. Spika, napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa hivi sasa tayari Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekwisha kutoa uamuzi wa kuendeleza utafiti wa nishati mbadala na wizara yangu tayari imekwisha kuanza kuchukua hatua ya kuanzisha mradi wa utafiti yakinifu ya nishati hizo ukurasa wa 53 kifungu cha 136 kinaeleza kwamba mshauri muelekezi wa kazi hiyo tayari ameshaanza kazi kwa mashirikiano makubwa na wataalamu wa wizara hii. Tunatarajia baada ya utafiti huo Zanzibar kuweza kuwekeza katika uzalishaji wa umeme mbadala. Kwa upande mwengine wizara yangu imo katika maandalizi ya kutathmini mpango wa uzalishaji wa umeme kwa kutumia gesi mara tu baada ya shughuli za uchimbaji wa mafuta na gesi zitakapokamilika hapa nchini.
Mhe. Mlinde amezungumza juu ya uwepo wa gesi na mafuta Zanzibar.

Mhe. Spika, ni kweli kwa ripoti mbali mbali zinazungumzia kuwepo kwa mafuta na gesi katika ukanda huu wa Afrika Mashariki. Lakini ripoti hizo hizo zinazungumzia umuhimu wa kufanyia utafiti wa ziada katika maeneo ya Zanzibar ili kuelewa ni sehemu gani na kiasi gani cha mafuta na gesi kinaweza kupatikana katika visiwa vya Zanzibar. Naomba tustahamili katika kuhakikisha jibu la hoja mpaka hapo Zanzibar itakapoanza rasmi kazi ya utafiti kwa maslahi ya Zanzibar. Hivi karibuni baada ya kukamilika taratibu za kuwezesha Zanzibar kusimamia suala hilo rasmi lenyewe.

Mhe. Salma Mohammed Ali umetoa ushauri kwamba Mhe. Waziri kuongeza nguvu katika kuimarisha mafunzo ya wataalamu wa mafuta na gesi.

Mhe. Spika, nataka kulihakikishia Baraza lako kuwa wizara hii inajiandaa vizuri katika kujitayarisha na kujenga uwezo wa Idara ya Nishati ya wataalamu wameanza kuajiriwa wengine kupelekwa masomoni na wengine wa wameanza mwishoni mwa 2013. Hata hivyo ushauri wa kuongeza kasi katika kujiimarisha zaidi umechukuliwa kwa heshma zote. Kiambatisho D kinazungumzia wafanyakazi wawili tu waliopelekwa masomoni.

Mhe. Mgeni Hassan Juma ameuliza swali hili, najibu sasa, ni kweli mpaka sasa ni wafanyakazi wawili tu ndio waliopata mafunzo ya muda mrefu. Hata hivyo mbali ya wafanyakazi wengine zaidi kupangiwa kuendelea na mafunzo hayo Wizara yangu kwa

mashirikiano ya pamoja na Bodi ya Mikopo imeandaa mikakati maalum ya kutoa upendeleo kwa wanafunzi ambao wanadhamiria kusoma fani ya mafuta na gesi kwa ngazi ya shahada ya kwanza *undergraduate* tayari Mhe. Spika, wanafunzi sita wanaendelea na mafunzo hayo kupitia mkopo wa Bodi hiyo na wengine zaidi ambao wanachukua mafunzo hayo kwa njia nyenginezo katika vyuo mbali mbali ndani na nje ya nchi, wote hao wizara yangu inafatilia kujua maendeleo yao na iko tayari kufanikisha ajira zao mara tu baada ya kumaliza na kufaulu masomo yao. Mpaka sasa tayari tunao wataalam watano katika Idara na idadi hiyo itaendelea kuongezeka baada ya mkumbo wa wanafunzi walioko masomoni kwa sasa kumaliza masomo yao kufikia mwaka 2014/2015. Tunatarajia kuwa na wataalam zaidi wa kusimamia suala la mafuta na gesi katika mwaka huu.

Kwa hivyo Mhe. Spika, tunasomesha sio wale wawili niliowataja kwenye hotuba yangu. Nimezungumza mara hii baada ya wizara yangu kuchukua jitihada za kuwahasisha wanafunzi ambao wamemaliza na kufaulu kidato cha sita wanafunzi wengi zaidi wameonekana kujiunga na fani ya mafuta na gesi na kupata upendeleo maalum ya mikopo ya serikali kupitia bodi ya mikopo ya Zanzibar. Kwa mtazamo huu ni hakika kuwa Wizara hii imeanza kuchua hatua muafaka katika kujijengea uwezo wa kujiimarisha katika fani ya mafuta na gesi asilia na tumo katika kuendeleza hatua hizo za ziada katika kuongeza nguvu na matayarisho yake.

Mhe. Spika, Mhe. Makame Mshimba alizungumza juu ya suala la kuwapatia wananchi wanyonge mikopo ya kuingia umeme, Mhe. Naibu Waziri amelitaja lakini nasema kwamba hiyo jitihada tayari tunaendelea nayo kutoa umeme kwa mikopo. Hoja ya upatikanaji wa transforma Mhe. Makame Mshimba Shirika tayari limeshaagoza transforma na zinatarajiwa kuwasili karibuni. Usambazaji wa Umeme katika vijiji viliomo katika Jimbo la Mtambwe Mhe. Salim Abdalla Hamad utekelezaji wa upelekaji wa umeme katika mwaka 2013/2014 vijiji vya Mtambwe viliongizwa katika mpango huo ni Mtambwe Mkuu Chanjaani ambaye Mhe. Naibu Waziri ameshalieleza.

Na hoja za gharama za umeme ni ghali hizo wananchi wa vijiji hawazimudu vile vile Mhe. Naibu ameshazungumza na transforma iliyopo Muhimbini nani anatakiwa kubadilisha napenda kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi kuwa transforma itabadilishwa mara tu baada ya kuwasili kwa transforma zilizoagizwa na Shirika tunaomba wananchi kuwa wastahmilivu.

Ulipaji wa fidia mazao yanayokatwa kwa ajili ya upelekaji umeme Kwareni Vitongoji Mhe. Saleh Nassor Juma, Mhe. Spika, kwa kawaida ulipaji wa fidia kwa wananchi walioathirika kutokana na upatikanaji wa umeme hulipwa na shirika au mteja aliyepeleka umeme huo. Aidha kwa kadhia ya upelekaji umeme Kwareni anaepaswa kulipa ni Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na Shirika la Umeme. Hata hivyo Mhe. Mwakilishi mimi na yeye tuna miadi tukutane ili kulitatua tatizo hili, kwa hivyo ile miadi bado ipo Mheshimiwa, tukutane tulitatue tatizo hili watu walipwe haki zao.

Mhe. Spika, umeme unakuwa hauna nguvu sana katika maeneo ya Kwarara, Mambosasa, Kibondeni na Pangawe na kwa maana hiyo kama Maungani na Kichaka punda hamna umeme kabisa Mhe. Thuwaibah.

Mhe. Spika, shirika linaendelea na mpango wa kufanya marekebisho katika maeneo yote hayo aliyoyataja na tumeshaanza na maeneo ya Kwarara Mambosaa na Kibondeni, katika mpango wa kupeleka umeme vijijini. Katika mwaka huu tumepanga kupeleka Kibondeni, Kipungani na Kitongani.

Hoja nyengine kwamba fedha zilizotolewa na Mbunge, Mwakilishi na wananchi wa kijiji cha Mapate Mwembeni Chambani na kijiji cha Ndegeni, Mhe. Mohammed Mbwana Hamad, jibu ni kwamba Wizara kupitia Shirika ina azma kubwa kupeleka umeme katika kijiji cha Ngomeni. Fedha zilizotolewa na Mbunge, Mwakilishi na wananchi wa kijiji cha Mapate, Mwembeni Chambani na kijiji cha Ndegeni Mhe. Mohammed Mbwana Hamad fedha hizo ambazo ni Tanzania shilingi milioni tano mia saba na sabiini saba elfu mia tisa na tisa zilizolipwa kwa jili ya kijiji cha Mapate, Mwembeni, Chambani na Tanzania shilingi milioni nne mia tano ishirini na tatu elfu mia tatu arubaini na mbili za kijiji cha ndegeni zimeshatumika na zimejumuishwa pamoja katika ukurasa wa 58 kifungu cha (1) 48 kitabu cha hotuba yangu kwenye maelezo ya fedha zilizotumika katika mradi wa usambazaji umeme vijijini na vile vile kwa uchanganuzi vinaonekana kwenye kiambatisho (a) ukurasa wa 99.

Hoja nyengine ya Mohammed Mbwana ni kwamba wananchi wa kijiji cha Vuleni na Maweni ambao wameshaanza kulipia gharama za kutiliwa umeme ni lini watafaidika na huduma hii ya umeme. Mhe. Spika, tunamuhakikishia Mheshimiwa kwamba hiyo kazi itakamilishwa kabla ya kumalizika robo ya pili ya mwaka wa fedha 2013.

Ni lini kijiji cha Moga Kirama kitasambazwa umeme na wananchi wapo tayari kuchangia Mhe. Ussi Jecha. Kijiji cha Moga Kirama kimepangwa kupatiwa umeme ndani ya mwaka huu wa fedha tunaomba mashirikiano yake.

Kufungwa mita za tukuza katika jimbo lake Mhe. Suleiman Hemed Khamis tunamuahidi Mheshimiwa mita za tukuza tutazifunga katika jimbo lake na lengo la shirika kuwafungia wateja wote Unguja na Pemba.

Ni lini vijiji vitatu vilivyomo katika jimbo lake vitapatiwa umeme Mhe. Suleiman Hemed Khamis. Mhe. Spika, hatua za usambazaji katika vijiji vitatu umepangwa kusambazwa ndani ya mwaka wa fedha ninamuomba Mheshimiwa kushirikiana na Shirika ili tufanikishe. Mambo haya kwa kweli tumekusudia ndani ya miezi hii kumi na mibli tuliyonayo tuyafanye. Kwa hivyo tushirikiane karibu zaidi. Maana ya kushirikiana ni kwamba tuwe tunakumbushana.

Lini vijiji vya ngomeni, Banaani na Mwachawa vitapatiwa huduma ya umeme Mhe. Abdalla Juma. Mhe. Spika, wizara kupitia shirika ina azma kubwa ya kupeleka umeme katika kijiji cha ngomeni kwa hivyo Mheshimiwa tushirikiane kwenda kutembelea kijiji

hiki kuona uwezekano wa kupata njia ya kukikipatia umeme kijiji hicho ili tuepuke kukata mikarafuu mingi iliyopo Ngomeni. Mhe. Abdalla twende tukatizame hiyo sehemu niko tayari, tupange tukatizame tuone.

Vijiji vya Banaanina Mwachawa tunaahidi kuwasambazia ndani ya mwaka huu wa fedha hichi kimoja tukashauriane, hiki kimoja mwaka huu wa fedha.

Hoja kazi ya ujenzi wa laini ya kijiji ya Kivugo ikamilishwe Mhe. Hassan Omar tunapenda kumhakikishia kwa ajili Kivugo kitakamilishwa haraka iwezekanavyo.

Halafu Mhe. Hussein Ibrahim aliomba vituo viwe kwa masaa 24. Shirika limeona hilo na kwa kutumia teknologia iliyopo ipo kwenye mchakato wa kutoa huduma kwa simu za mikononi na tayari imeshafanya mazungumzo na Kampuni ya Zantel katika kufanikisha hilo. Lakini pia wazo lake sio baya la kuongeza muda katika vituo vile.

Uhaba wa wafanyakazi katika tawi la Pemba ufikiriwe Mhe. Hussein Ibrahim Makungu. Mhe. Spika, uongozi wa Shirika umeliona tatizo hilo na Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika imeshaidhinisha nafasi kumi na nane za ajira mpya kuanzia mwaka huu wa fedha.

Ni kiasi gani Shirika linadaiwa na Tanesco Mhe. Hussein Ibrahim Makungu anauliza. Mhe. Spika, hadi kufikia Machi, 2013 Shirika lilikuwa linadaiwa jumla ya shilingi bilioni ishini na sita, mia mbili arubaini na mbili milioni laki tisa sabiini na saba elfu mia na thamanini, Shirika linazidai taasisi za SMZ hadi Machi 2013 ni shilingi bilioni kumi na tatu mia nne na sitini na nne milioni na sitini elfu na mia mbili. Mheshimiwa haya ndio madeni tunayodaiwa lakini utatatibu wa kulipa serikali inajiandaa kulipa hivi sasa hivi kuna sehemu ya fedha tayari ziko katika Jamhuri ya Muungano, Wizara ya Fedha na Wizara ya Fedha wanashauriana bilioni kumi na nane zende zikalipe madeni haya na hizo zitakazobakia hapo Shirika linatakiwa liteneneze shedulle ya kulipa kwa utaratibu wa *installment* ili madeni yaondoke ya kudaiwa umeme.

Ni lini Kisiwa cha Makoongwe kitasambazwa umeme Mhe. Abdalla Mohammed Ali, Kisiwa cha Makoongwe kimo katika mpango wa usambazaji wa umeme vijijini na huduma hiyo inatarajiwa kupelekwa kuanzia mwaka 2014, sikwambii mwaka 2013. Hii ndio niliyowauliza wenzangu semeni jambo mnaloliweza msiseme jambo msiloliweza. Kwa hivyo akanambia mwaka 2014 hili suala litakuwa.

Gari ya wafanyakazi Pemba inaonekana milioni ishirini na tano kati ya elfu mbili na hamsini na tano. Mhe. Salma Mohammed Ali, jumla ya wafanyakazi wote wa Wizara ni 2055 ambapo kwa upande wa Pemba ni 674 ambao wanajumuisha 135 Ofisi Kuu Pemba, 155 Zeco Pemba na 324 Zawa Pemba.

Mhe. Rufai Said Rufai kusaidiwa kupatiwa umeme vijiji viliopo katika jimbo lake tunamhakikishia Mheshimiwa kuwa tutatoa mashirikiano kupatiwa umeme vijiji hivyo. Maana tukisema tutatoa mashirikiano ni kwamba bado Mhe. Rufai tuendelee kuzungumza tutizame uwezo wetu serikali. Kijiji cha Kijichi hili lishapatiwa umeme

Mhe. Rufai, Kijiji cha Kijichi huduma ya umeme ipo isipokuwa umepungua nguvu kutokana na ongoezeko la mahitaji. Sehemu hiyo Shirika limeshindwa kujengwa laini mpya ya umeme ya juu kutokana na ujenzi holela uliofanywa. Hata hivyo Shirika linatarajia kutumia njia ya umeme wa ardhini ili kukipatia kijiji cha Kijichi umeme mzuri.

Hoja je, fedha iliyotajwa katika hotuba kuhusu mradi wa usambazaji umeme ni ya shirika pekee au na mchango wa wananchi Mhe. Rufai huyo. Mheshimiwa jumla ya fedha hizo zimejumuishwa na mchango wa wananchi, SMZ na Shirika la Umeme.

Mhe. Spika, Mhe. Mtando kama angelinileta juzi au jana angepata majibu mazuri sana, lakiniamenileta leo tena hapa hapa ina ukurasa moja mchango wake huo, ukurasa wa pili mchango wake huo, ukurasa wa tatu mchango wake huo, ukurasa wa nne, mchango wake huo, ukurasa wa tano mchango wake huo, ukurasa wa sita mchango wake huo, ukurasa wa saba mchango wake huo, ukurasa wa nane ni *document* kamili. Ningeliipata jana hii ningeliitengenezea majibu, lakini Mheshimiwa nimeipata leo na mna vifungu vya kuvifanyia kazi. Maana yake mimi nilipita mchana hapa kwa sababu nilisahau kitabu changu cha makisio. Nilipofika hapa niliambiwa na Mhe. Mtando kaja kuchukua kitabu sasa hivi nikajua anaandaa kitu. Sasa hizi Mhe. Mtando itabidi nishirikiane Mhe. Spika, sitoweza kuyajibu hapa ghafla, maana hayo niliyoyajibu nimekaa pamoja na wenzangu kule na tukafanya kazi hii.

Mhe. Abdi Mosi Kombo yeye ametaja baadhi ya vijiji vyenye matatizo ya maji ambavyo vishughulikiwe maji na umeme navyo vile vile ninamshukuru ni michango mizuri lakini sasa ndio hivyo hivyo ningelipata kuwaeleza wale wenzangu watatengeneza lini masuala haya wala wasingepata tabu hiyo lakini wamenipa hapa. Na huyu mmoja ambaye jina lake nimelitafuta sana humu sijalipata halimo vile vile mna hoja nzuri tu. Mheshimiwa mambo haya yana hoja nzuri sana lakini nimeyapata hapa, sasa wenzangu wale hawakuyaona maana hii kazi tunafanya pamoja, uongozi wa pamoja ndio tunaoendesha.

Mhe. Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi na ninawashukuru sana waheshimiwa wajumbe kwa kunisikiliza juu ya masuala haya lakini bado naendelea kuwapa maombi yangu, haya mambo ni mazito na yote yanawagusa wananchi na yanahitaji kutekelezwa kwa utaratibu maalum sio buu, baa si rahisi kutekeleza mambo haya ya umeme maji, nishati kwa buu, baa yatengenezwe kwa utaratibu maalum.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kutoa hoja.

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Spika, nilikuwa nataka muongozo wako kidogo, Waziri alipokuwa ametoa hayo majumuisho hapo, ametaja kwamba document nimempelekea asubuhi ya leo. Lakini na mimi ndio muda ambao nimeafiki kuupata. Maana yake juzi ulipokuwa unaahirisha hapa kikao mtu wa mwisho alikuwa ninafikiri ni Mwalim Harun ndio ukatwambia kwamba huyo atakuwa mtu wa mwisho waliobakia

maana yake tupeleke kwa maandishi lakini na kikao ndio kilikuwa kinaahirika. Sasa Waziri anasema kama angeipata jana angeweza kujibu, lakini jana bahati mbaya kulikuwa hakuna Baraza na utaratibu wetu hapa huwa tunapeana hapa Barazani. Sasa nilikuwa naomba muongozo wako katika hili kupata majibu ya yale ambayo nimeyaandika.

Lakini jengine Mhe. Spika, nilikuwa naomba muongozo wako vile vile kwa sababu hata mwaka jana kuna michango kama hii niliitoa ya maandishi katika Wizara ya Mifugo na Wizara ya Elimu na Waheshimiwa mawaziri walipokuwa wamefanya majumuisho yao waliahidi kutoa michango ile kwa sababu ililetwa asubuhi na muda ambao tunaopata. Kwa sababu unapoahirisha Baraza ndio tunaambiwa kwamba sasa hamtoweza kuchangia mtachangia kwa maandishi. Kwa hivyo inabidi na wewe ukajiandae asubuhi umletee, lakini asubuhi anakuwa anafanya majumuisho, anapofanya majumuisho ni kweli hatoweza kuyajibu maana yake mengi yanahitaji takwimu na vitu vyengine mimi nakubaliana nayo, lakini wanapotoa ahadi ya kwamba watajibu kwa maandishi waheshimiwa mawaziri huwa hawatujibu mara nyingi sana ni wachache sana wanaojibu.

Mimi nina kumbukumbu za kikao kilichopita cha mwaka jana katika Wizara ya Mifugo na Wizara ya Elimu mpaka hii leo Mhe. Spika, sijajibiwa. Na leo Mhe. Waziri keshasema hawezi kujibu ni kweli, document anasema ina kurasa 8 kweli ni nane tena ndio haba hizo nimejaribu kupunguza kweli lakini nina mengi ndio pale huwa tunaomba tuchangie lakini na muda nao pia unatukwaza. Sasa nilikuwa naomba muongozo wako Mhe. Spika, katika hili.

Mhe. Spika: Waheshimiwa wajumbe suala la kuchangia kwa maandishi kwa mujibu wa taratibu za kanuni makatibu wangu watanambia kanuni gani lakini ninahitaji taarifa itolewe na inaendesha kikao mapema kidogo kufuatana na ule muda ambao unavyoonekana. Kwamba kufuatana na muda nitakuwa na wachangiaji hawa na waliobaki wachangie kwa maandishi wakati ule kabla ya kuahirisha kikao. Inawezekana sana kwamba aliyekuwa anaendesha kikao hiki ambae alikuwa ni mimi sikuwahi kufanya hivyo, ingawa nilielekeza mara kwa mara kwamba kwa kweli muda wetu ni mfupi mno kuna baadhi ya wajumbe waliwahi kumpelekea Mhe. Waziri michango ya maandishi hata kabla ya kufikia mwisho. Na kwa bahati nzuri kuna mmoja yeye alibahatika kuitwa na kuchangia lakini pia ikawa tayari amepeleka maelezo yake kwa maandishi. Bahati nzuri Mhe. Waziri ameyajibu hayo.

Sasa kanuni inatambua michango ya maandishi lakini kanuni hii haiweki wazi pahala ambapo unaweza ukazuia fungu. Kwa sababu ukiangalia 98 (6) (c) inaelekeza kwamba kama una mjumbe anataka kutoa hoja ya kupunguza fungu na ikiwa inaanzia kwenye kutaka maelezo na hatimae unataka upunguze fungu kuzidisha hamna lakini kupunguza fungu ataeleza nia yake hiyo wakati anachangia makadirio. Sasa hapa wakati anachangia makadirio ni ile ya kusema kwamba utumie hii microphone ndio inayotambulikana. Kwa hivyo ndio maana hapa mwisho mwisho hasa kabla ya kuwahoji waheshimiwa wajumbe nilisema kwamba masuala mengine Mhe. Waziri atayafanyia kazi, kauli ile maana yake ni nini?

Kuna baadhi ya mambo itakuwa hakuyajibu na kuna baadhi ya mambo yamekuja kwa maandisho, bila shaka haya ayachukue kwa kukayafanyia kazi. Na kwa sababu hii kanuni yenyewe haisemi wala haielekezi kama yula anayechangia kwa maandishi anaweza kuzuia fungu lolote na kupunguza fungu lile na ndio maana nikasema kwamba Waziri masuala mengine atayafanyia kazi wakati anaendelea na shhughuli hizi. Lakini kimsingi michango ya maandishi inakubalika kwa mujibu wa kanuni hii, taarifa inapaswa iwe imetolewa mapema ili wale ambao watakosa na kwa kawaida unawataja hasa wale ambao watakosa kuchangia kwa kutumia microphone basi wajitayarishe kuchangia kwa maandishi. Nadhani hayo ndio maelekezo ambayo ningeweza kuyatoa.

Kwa hivyo nisisitize tu kwamba Mhe. Waziri tukubaliane kwamba baadhi ya mambo ambayo yapo kwa maandishi jitihada ya maelezo ambayo ameyatoa basi itoshe na mengine anayachukua kwa ajili ya kuyafanyia kazi.

UTARATIBU

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, samahani kidogo nilikuwa najaribu kutaka ufafanuzi wa ziada hasa kwa hii hoja ambayo aliyoizungumza Mhe. Mtando ambayo na wewe umejaribu kuitolea maelezo ya kutosha, sasa na mimi nilikuwa nataka utusaidie maelezo ya ziada.

Mhe. Spika, kwa kuwa kanuni yetu iko silent kwa wale ambao waliochangia kwa maandishi na kwa bahati mbaya sana muda wetu tuliojipangia kufanya shughuli zetu kwa kweli vile vile na nafasi wanaopata wachangiaji tofauti na ile ambayo iliyokuwemo kwenye kanuni yetu kwa hivyo watu wengi huwa wanakosa kuchangia kwa mdomo kwa hivyo huwa wanachangia kwa maandishi. Kwa hivyo ina maana kuwa kuwa wanachangia kwa maandishi na hawana fursa tena ya kuja kuzuia fungu kwa hivyo ina maana wanakosa ufafanuzi wa yale ambayo waliyoyahoji. Na mfano mzuri aliotoa Mhe. Mtando kama kungekuwa kuna utaratibu mzuri kwa yale ambayo yaliyochangiwa kwa maandishi yakajibiwa vile vile kwa maandishi sisi tungekuwa tunafurahi sana kwa sababu hatupendi kuonekana kama tunasema, huwa tunapenda kwamba tuishauri serikali na serikali isikilize yale tunaoshauri na vile vile iweze kutekeleza.

Sasa mimi nadhani kwa kuwa kanuni iko silent, mimi nadhani tungeliwaruhusu wakazuia mafungu kwa sababu mtu anapozuia fungu si kama anazuia kama bajei isipite anahitaji ufafanuzi wa kutosha na kwa sisi Mheshimiwa Spika, sisi hatufanyi kazi mawizarani, kwa hivyo mambo mengi tunayoyazungumza humu ni matukio ambayo yanayotokea ndani ya mawizara yetu. Kwa hivyo kuna watu wanasikiliza je, lile tatizo letu suluhishi litakuwa vipi? Sasa kama haya yanakuwa hayakujibiwa Mhe. Spika, hatuwatendei haki wananchi wetu. Kwa hivyo mimi nadhani ushauri wangu kwa kuwa kanuni iko wazi na yale ambayo Mhe. Waziri hakujiandaa kuyajibu atayasema. Maana kuna mambo mengi unajua mawaziri wanakuwa na uzoefu. Kuna mambo mengi anaweza kwamba hakupata mapema lakini baadaya kumsikia mwenyewe akihoji lile suala anaweza akamjibu pale pale, kwa sababu ni mambo ya utendaji ya kila siku, kwa yale ambayo atakuwa hana

takwimu za kutosha hana uhakika nayo anaweza kumwambia tu nitakujibu wa maandishi na sisi tutakuwa tuna-quote ili kuweza kupata ufafanuzi.

Mhe. Spika, hayo si hayo tu ya maandishi kuna ahadi za mawaziri ambao katika bajeti iliyopita walitueleza watatekeleza mpaka leo hayakutekelezwa vile vile na bajeti zao zinakuja. Sasa mimi nadhani Waheshimiwa Mawaziri wajitahidi sana kwa yale wanaoyasema nitalitekeleza, wawe wanayaandika tu isije ikawa tunasumbuana kwa mambo madogo madogo. Mhe. Spika, nilikuwa nataka muongozo wako hasa kwa wale waliochangia kwa maandishi na kutokana na muda.

Lakini kubwa zaidi Mheshimiwa hili siku zote tunalizungumza lakini bado hatujalifanyia utaratibu, kuna siku ambazo tumejipangia kwa mujibu wa kanuni siku za kupitisha bajeti. Mheshimiwa siku hizi tulizirithi tulipokuwa tuna Wizara 13, sasa hivi tuna Wizara 16, muda tuliojipangia ndio ule ule. Sasa utakuta bado kuna mambo mengi Mhe. Spika, inabidi kama yako silent katika kanuni basi mimi nafikiri tuyatolee muongozo ili wananchi wetu tuweze kuwawakilisha vile vile ipasavyo.

Mhe. Spika, mimi jimbo langu ninawakilisha wananchi 25,000 ukinipa mimi dakika 20 na wakati mwengine dakika 15 watu 25,000 wa jimbo langu mbali wazanzibari waliobakia na watanzania wengine dakika 15 tutakuwa tunatenda haki. Mhe. Spika, huu mwezi wa Ramadhani hili posho tunalopata hapa hebu tulitumia kihaki lillahi ili tuweze kupata thawabu kwa Mwenyezi Mungu.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe ninafikiri yapo baadhi ya mambo, kwanza hii kanuni ni taratibu ambazo tunaweza tukazihuisha sisi wenyewe kwa mujibu wa muada na wakato tunaona unafaa. Bahati nzuri kanuni hii tuliifanyia marekebisho ya mwisho mwaka 2012 mwaka jana tu wakati hizo wizara 16 hili hatukuliona lakini tulijadili vya kutosha kabisa, lakini hili la kuzidisha muda hatukuliona. Hilo moja.

Lakini la pili mimi ninafikiri tujaribu kuangalia kwa makini sana kwa sababu unapotoa muda mkubwa kwa ajili ya kuchangia jambo tuelewe kwamba kutakuwa na muda mrefu zaidi ya mkutano huu. Ukiwa na muda mkutano mkubwa zaidi tuseme miezi miwili na nusu mfano, hiyo maana yake ni kwamba muda wa miezi miwili na nusu kufuatana na hali ya uchumi wa nchi yetu itakuwa tunafanya matumizi yaliyo makubwa. Kwa hivyo masuala haya lazima tuyaangalie katika pande mbili. Ni kweli kabisa wizara zimezidi, kununi hii tuliirekebisha mwaka jana lakini hilo hatukuliona.

Sasa tunaweza tukasema tuongeze muda lakini wakati huo huo tuzingatie hata ule muda wa kuchangia, maana mtakubaliana nami kwamba katika michango mingi sana inakuwa na marejeo marejeo mengi ambayo kanuni hii hii haitaki. Ile ya waheshimiwa wajumbe kusema kwamba sasa ninakazia kidogo pale huwa tunasaidiana ili kuona huo mkazo labda kuna pointi nyengine mpya imeingia. Sasa ninachosema ni kwamba mambo haya lazima tuzingatie katika pande zote.

Mfano Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania dakika 15 ninafikiri iko hivyo, sisi kanuni yetu dakika 30 ndivyo inavyohitaji katika mikutano hii ya makadirio na kwa bahati nzuri ndio mikutano mirefu. Kwenye vikao vya kawaida dakika 20 sasa kupanga ni kuchagua lakini unapotumia muda mkubwa tuelewe na bajeti yake inakuwa ni kubwa zaidi, inapendeza tuchangie vya kutosha kuwasaidia wananchi wetu juu ya yale tunayoyachangia kuiambia serikali ifanye hili na lile kwa ajili ya wananchi, lakini wakati huo huo tuzingatie kwamba uchumi huo, keki hiyo hiyo ndogo ije itumike kwa ajili ya kuwapelekea hao wananchi huduma hiyo, ikiwa ni pamoja na maji ambayo ni muhimu mno.

Sasa mimim bado ninasihi tena ninasihi sana kwamba hapo usoni kuna mapendekezo hapa ya kurekebisha kanuni kwa baadhi ya mambo ambayo nyinyi waheshimwa wajumbe mmeyasema na mengine tumewapa watendaji wetu wayazingatie na hilo tutaliangalia lakini bado sishawishiki kwamba muda wa kutumia uwe ni dakika 30 kwa kweli sishawishiki hata kidogo, kwa sababu muda utakuwa ni mrefu, matumizi yatakuwa makubwa na ni vizuri tukapata matumizi makubwa kwa vyombo hivi, lakini tuzingatie pia na huduma za wananchi.

Sasa kwa jambo ambalo kwa mujibu wa kanuni hii, katibu wangu pia atanisaidia hili. Jambo ambalo halikuwekewa utaratibu, ndio kama hiyo kanuni ambayo iko *silence*, Spika, anatakiwa atoe muongozo wa namna gani juu ya jambo hilo. Muongozo niliotoa ni kwamba Mhe. Waziri, ayachukue haya akayafanyie kazi. Baada ya hayo mimi nadhani nimuombe Mhe. Waziri, sasa aje asome aombe Baraza hili nini tufanye.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: kidogo Mhe. Spika, katika huu mchango wa maandishi Mhe. Spika, Waziri ndio anauchukua anakwenda kuufanyia kazi na mchana nategemea kwamba ataleta yale majibu, lakini mazungumzo ambayo yanafanyika katika Baraza huwa yanarikodiwa kwenye *Hansard*. Niliwahi kuuliza katika hotuba ya Mhe. Waziri wa nchi, Afisi ya Makamo wa Pili, juu ya utaratibu wa kuyaweka katika kumbukumbu haya mananoe. Lakini bado sijapata utaratibu gani unaotumika na hapa Waziri anayachukua na akiwa ameyatupa huwa kumbukumbu ndio hazipo, inakuwaje jambo hili.

Mhe. Spika: ni kweli nakumbuka jambo hilo ulisema wakati wa hotuba ya Makamo wa Pili wa Rais, na kweli halimo katika kanuni hii kwamba michango yamaandishi inaingia katika *Hansard* hamna hilo jambo. Tukaeleza kwamba itabidi hilo tulitafutie utaratibu ili tujuwe namna ya ku-print maelezo haya yakaingia katika *Hansard* ili ibakie kuwa ni kumbukumbu. Sasa hilo jambo hatujalifanya lakini ni kweli kabisa kanuni hii haina maelekezo, kwamba michango ya maandishi itaingiaje katika *Hansard* kwa sababu hii inakuwa *recorded* moja kwa moja, lakini michango ya maandishi ni ile ambayo unamkabidhi, maana yake ni kutafute utaratibu iwe *printed* iingie katika kitabu kile cha majadiliano. Lakini jambo ambalo tulifanyie utafiti hata wenzetu wanafanya nini katika suala la aina hii, maana nafikiri hata Bunge la Jamhuri, sijui walikokuwa Bungeni kama wana *experience* hiyo, lakini hata Bunge la Jamhuri nafikiri haingii katika *Hansard*. Sasa tume na kwa wenzetu nini wanafanya ili kuweza kuweka hizo kumbukumbu. Haipendezi kwamba yatupwe tu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali hotuba ya bajeti ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kupitisha vifungu vya matumizi ya Wizara hii.

Mhe. Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko: Naafiki

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU 25 WIZARA YA ARDHI, MAKAAZI, MAJI NA NISHATI

kifungu 0301

Mhe.Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, mimi katika mchango wangu niliulizia kuhusu haya mafungu ya makisanyo katika Ofisi Kuu Pemba. Hasa ukiangalia kwenye fungu la kwenye kodi ya malipo ya uendeshaji, makusanyo haya yanaonekana ni *copy and paste*. Mwaka jana kwa mfano kwenye kifungu 141503 Kodi ya Nyumba za Serikali, ilikusanya shilingi 61,000,000/= na mwaka huu makisio yapo pale pale pale 61,000,000/=. Ukija kwenye kifungu 142206 mauzaji ya nyumba za Serikali ilikisiwa milioni kumi na tatu mwaka jana na mwaka huu kuna milioni kumi na tatu. Kwenye utoaji wa viwanja na nyaraka 30,000,000/= mwaka jana na mwaka huu 30,000,000/=. Kwenye mauzo ya kokoto mwaka jana 1,000,000/= na mwaka huu 1,000,000/=. Kwenye malipo ya huduma za kazi au seramala mwaka jana 1,000,000/= na mwaka huu 1,000,000/=. Sasa mimi nimepata shaka kidogo nikataka kujua, hivyo haya matukio kwa mwaka jana tunawakisia mle kwa mfano wanunuaji kokoto walikuwa 5 na mwaka huu watakuja wale wale 5 tu, hakuna mabadiliko yoyote. Sasa nimepata shaka hebu naomba kidogo maelezo, yako mengi haya mafungu tusitupe muda mwingi ukiyatizama haya nakusanyo, hasa kwa Pemba haya, mengi yamekuwa yanajirejea rejea yale yale, hebu Mhe. Waziri, atusaidie kidogo makusanyo hayo umeyakusudia vipi hata yakaja yaoane kila kitu kioane, maana ingebadilika ikawa angalau imeshuka ukasema tunataraji kwamba kushuka au yakawa yamepanda kidogo, lakini yako pale pale, nataka maelezo kidogo kwenye hilo.

Mhe. Mwenyekiti: huu ni mchango ambao wa maandishi ambao kwa mujibu wa tafsiri za kanuni chini ya kanuni ya 98 hii huwezi ukazuia fungu. Kwa hiyo anachohitaji maelezo, maelezo yakitoka basi.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, kikawaida ukifanya makisio mwaka huu ukiyaona hukuyapata basi Wizara ya Fedha mwaka unaofuatia wanakupa makisio yale yale wanakwambia nenda ukajitahidi uyapate, ndio maana ukakuta kwamba kule kuna 61,000,000/= na safari hii imekuwa hiyo hiyo na mashaka yanayokodishwa mikarafuu ambayo safari hii sisi hatutokodisha mashamba kwa

sababu mashamba yote yamepelekwa kilimo sie hatuna ndio maana hatujaweka makisio yetu.

Mhe. Mwenyekiti, hivyo inapotokezea kwamba 30,000,000/= mwaka jana hukuzipata, Wizara ya Fedha wanakwambia hapana hatukuachi safari hii tuchukuwa hiyo hiyo 30,000,000/= uende ukafanye kazi, ndio maana zimekuja tena vile vile, tutajitahidi mwaka huu tukamatane tuache kufanya kazi kwa mazoea ili tuzipate fedha hizi.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, wakati jana ninachangia hotuba hii, kwa masikitiko makubwa sana nilizungumza kwa unyonge sana jinsi ya watendaji pale Pemba wanavyoendelea kumega ardhi ya Skuli ya Ndagoni na kutafutwa hatimiliki kwa Shule ile. Ingawa Waziri, amejibu hapa lakini kwa kiasi kikubwa makubaliano ya mwanzo ilikuwa ni sehemu tu ya ile shamba ya wale Sleiman Ayoub na familia yake, lakini sasa mpaka juzi wanaendelea kujenga banda na kukata miembe pamoja na kuchukua sehemu ya makaburi ya ile familia ya mzee Ayoub Suleiman pale. Sasa huu utaratibu wa kuendelea kukiuka makubaliano waliyofanya mwanzo, nakubali kwamba mwanzo walitoa kibali chao. lakini sasa kila siku wanaendelea kuichukua ile shamba na wakiendelea kudai wanasema ah! mashamba ya waarabu wacha tuchukue. Sasa haoni Mhe. Waziri, katika hili. Mimi nashukuru kwamba yeye mwenyewe hataki ubaguzi na namkubali kwa ninavyomjua huyo hataki ubaguzi, lakini hii kuchukua ardhi za watu bila ya ku-*negotiate* na wale jamaa, hii si dhulma kwa Wizara yako.

Mhe. Mwenyekiti: hili la sehemu ya mapato au kwenye uendeshaji, mimi nafikiri uendeshaji. Kwa hiyo hebu tuende kwenye uendeshaji kule tafuta pahala Mhe. Waziri, huyu mbane umuulize masuala.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mimi sikupata majibu yangu vizuri sikiyasikia niliona kama labda Mhe. Saleh anaendelea kwenye hoja ile ile, sasa yale majibu sikuyasikia vizuri.

Mhe. Mwenyekiti: nilielekeza hivi ulipaswa usikilize kwa makini, nilielekeza hivi kwa jambo ambalo halikuendana kwa mujibu wa kanuni kwamba nina nia ya kuzuia fungu kadhaa, kanuni ya 98(6)(c) ndio inayosema hayo. Kwa maelezo ya maandishi ruhusa nitakayoitoa ndio katika ile miongozo hiyo, haiko hiyo. Lakini muongozo anauotoa muendeshaji kikao ni kwamba maelezo yakishatoka yatoshe, kwa sababu venginevyo itakuwa sasa unazuia fungu.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, lakini nimejaribu kuangalia hicho kifungu unachokizungumza Mhe. Mwenyekiti, cha 98(6)(c) kinaeleza kuwa Mjumbe anayetaka kutoa hoja kupunguza fungu lolote anaeleza nia yake hiyo wakati anachangia makadirio ya Wizara inayohusika na matumizi hayo. Sasa mimi katika mchango wangu nimeandika hayo kwamba nina nia ya kulizuia fungu kama sikupata maelezo yakutosha, kwa maana mchango wangu badala ya kuusoma nimeuandika kwa maandishi, hata Waziri akisoma ataona humu.

Mhe. Mwenyekiti: Mchango unaotajwa hapa ni ule wa kutumia *microphone*, kama nilivyosema pale, ndio unaozungumziwa humu. Wakati wa kuchangia ni ule mchango unaotumia *microphone* hii ndio unaotajwa hapa.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, mimi sitaki kubishana na kiti sana, lakini tunapozungumzia kuchangia maana yake michango iko ya aina mbili, kuna michango ya maneno ya michango ya maandishi yote inakubalika ni michango nachangia ile hotuba, Sasa kama nimechangia mimi sikwamba sikuja kazini nilikuwepo, lakini sikupata nafasi ya kuchangia kwa sababu muda wenyewe haukuwa umetosha, sasa nimeambiwa nichangie kwa maandishe, mimi nimechangia kwa maandishi na nimeeleza nia yangu hiyo. Sasa Mhe. Mwenyekiti, kama nitakua sasa sikupewa hiyo fursa ile haki itakuwa imeenda upande mmoja alosema kwa maneno, aliyesema kwa maandishi haikuwa, mimi naona kama itakuwa si sahihi. Lakini Mhe. Mwenyekiti, unaweza kutupa muongozo wako zaidi.

Mhe. Mwenyekiti: Sitaki nimtetee Mhe. Waziri, lakini sijui kama mchango wako ulikuwa wa namna ya amb*u*sh kwa sababu, kwa sababu *ambush* ni ile usiotegemea kwamba mchango wenyewe umekuja hapa hapa, mie kaniandikia pale nikamwambia basi tuache nitatoa maelekezo na maelekezo ninayotoa ndio hayo, Waziri toa maelezo, maelezo ametoa basi itoshe. Kwa sababu yeye hakupata nafasi, wewe ulikaa ukajipangia kwamba niseme kadhaa wa kadhaa, yeye hakupata nafasi ya kujitayarisha na hilo.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Kwa utaratibu huu unaokwenda inaonekana sasa sisi Wajumbe wako tutakuwa hatupati nafasi ya kuchangia. Kwa sababu ikiwa kwamba Mhe. Waziri, kasema, kwanza hicho kitabu chenyewe kinaletwa ile siku ya kuchangia ndio anakitoa, anakileta kitabu Mhe. Waziri, wakati yeye mwenyewe sasa anakaa pale kukisoma, na mimi ninataka nichangie kwa mujibu wa vile ambavyo kile kitabu mwenyewe kakileta, mimi hoja zangu zinatokana na kitabu, sasa kitabu anakileta kwa siku ile, anasoma akimaliza kusoma tuanze kuchangia na kuchangia wenyewe tuko Wajumbe 81 humu, tukianza kuchangia Mhe. Mwenyekiti, kwa muda ambao tunapewa haiwezekani sote tukachangia, ndio maana ukawa unasema tutachangia kwa maandishi, sasa kama kwa maandishi muda ambao unatuambia sasa tuchangie kwa maandishi huwa muda wa kufunga Baraza ushafika, siwezi kutoka na mchango wangu nikampelekea Mhe. Waziri, nyumbani kwake, lazima nimsubirie wakati hapa kwenye ndio nimpe mchango, nimeuleta mchango leo asubuhi kwa sababu juzi tumeahirisha, Jumamosi hamna kazi, Jumapili hamna kazi hamna Baraza, leo Jumatatu ndio Baraza limeanza nimeuleta. Mhe. Mwenyekiti ukinambia nimefanya *ambush* itakuwa kwa kweli hukunitendea haki, nimeuleta kwa sababu ndio kikao kilipokuwepo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa mimi nimeshaleta mchango wangu nimeeleza ndani yamchango wangu nina moja mbili tatu, sasa na mimi nina haki kama yule ambaye alichangia kwa mdomo, kwa sababu pia unaweza kuchangia kwa maandishi, imeandikwa kwenye kanuni. Sasa Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa ninaomba kama mtu ana buti lake tuendelee kupiga Waziri anauwezo wa kujibu atujibu hana atatuomba kwamba atatuletea kwa maandishi hakuna tatizo, lakini wawe wanaleta kwa sababu nimezungumza hapa Mhe.

Mwenyekiti, mwaka jana tumeambiwa haya haya ntamjibu kwa maandishi, lakini sasa kuna mwaka bajeti nyengine hii majibu hatujayapata na haya tunayazungumza sana kwamba Waheshimiwa Mawaziri wanaposema nitajibu kwa maandishi inakuwa kama ndio kichaka chao kile maandishi, wanaondoka hadithi imekwisha.

Mhe. Mwenyekiti, na hili linatokana na nini, vile vile tunapokuwa tunachangia kwa maandishi Baraza halina kumbukumbu la kuweza kuwakumbushia Mawaziri au kuikumbusha Serikali juu ya yale ambayo tumeyazungumza. Sasa hilo nalo linakuwa tatizo, ndio lile nililokuwa nakwambia Mhe. Mwenyekiti, na leo naona Mhe. Waziri, na maandishi yangu akishakuyatupa yanapatikana wapi na maneno ya Mjumbe anayozungumza kwenye Baraza huwa ni kumbukumbu yanawekwa haya kuna watu wanakuja kufanya utafiti, na wewe mwenyewe Mjumbe ukitaka kujua ulichokisema maana yake uende kwenye *Hansard*, lakini kama inakuwa yale hayachukuliwi na hakuna utaratibu mzuri inakuwa yanapotea. Kwa hiyo nilikuwa ninaomba sana Mhe. Mwenyekiti, utukubalie Waheshimiwa Wajumbe wako kwamba kama kuna mtu amechangia kwa maandishi anapiga buti apige buti, Waziri ana uwezo wa kujibu ajibu hana atuambie hana uwezo atujibu kwa maandishi lakini watuletee majibu yetu kwa maandishi kweli.

Mhe. Mwenyekiti: nilichoeleza Waheshimiwa Wajumbe kwa ujumla ni kwamba suala hili la michango ya maandishi linakubalika, lakini kukaa katika kumbukumbu za *Hansard* hilo utaratibu wake haujakuwepo hadi sasa. Ndio niliposema kwamba ni jambo ambalo labda tulifanyie utafiti wenzetu wanafanya nini. Kwa mawazo ya haraka haraka ni labda ni ku-*print*, sasa jambo hilo bado hatujakubaliana, nishauri tu kwamba labda tu-*print* ili yaje yafikie pahala yawe ni sehemu ya kumbukumbu angalau kwenye vile vitabu, lakini ni mjadala unaozungumzwa *microphone* ule unarikodiwa moja kwa moja, hilo moja.

La pili suala la uwasilishaji wa vitabu na kuchangia hapo hapo pia nalo tulilizungumza hilo na nafikiri katika maendeleo ya hasa Wenyeviti, huko nyuma ilikuwa Mwenyekiti hapati nafasi yakwenda kujitayarisha, Mwenyekiti wa Kamati, ikawa kitabu apewe angalau siku moja kabla, kanuni tukairekebisha iwe hivyo na hili tukasema kwamba ni vizuri basi vitabu vifike mapema ili wajumbe wapewe ilimradi tu visije vikapotea hatimae siku ya kusoma tayari itakuwa Mjumbe akipewa itakuwa amejitayarisha vya kutosha, lakini nalo haliko katika utaratibu kwamba tulifanye hivyo, ni mambo ambayo tuyatizame baadae katika utaratibu wa kurekebisha kanuni zetu, ndiyo nilivyozungumza hivyo. Na katika hili ambalo unataka maelezo Mhe. Mtando, nimesema Mheshimiwa akishatoa maelezo haya na hasa hasa kwa sababu mchango wako ulichelewa hakupata nafasi ya kujitayarisha akatoa maelezo yaliyo mazuri. Mhe. Hamza alitoa muongozo hapa akasema basi pale atakaponyanyuka akikumbusha apewe maelezo kwa sababu ni mambo ya kila. Kufuatana na muongozo ule ndio nikasema basi Waziri toa maelezo, lakini sasa yatoshe yasifikie kiwango cha kuzuia fungu kwa sababu uzuiaji wa fungu upo kwa mujibu wa kanuni ya 98(6)(c). Mimi nafikiri tuendelee nimejitahidi kutoa maelezo.

kifungu 0301 Ofisi Kuu Pemba 106,000,000/=

kifungu	0501	Idara ya Ujenzi	9,700,000/=
Kifungu	0701	Hifadhi ya Mji Mkongwe	24,000,000/=
kifungu	0901	Idara ya Ardhi na Usajili	3,505,000,000/=
Kifungu	1001	Idara ya Upimaji na Ramani	70,000,000/=
Kifungu	1101	Idara ya Nyumba na Makaazi	

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwanataka maelezo lakini sasa hoja yangu itakuwa ndio yale yale atakuja kusimama Waziri umwambie kwamba kachangia kwa... bora nikae tu tuendelee.

Kifungu	1101	Idara ya Nyumba na Makaazi	325,000,000/=
Jumla ya Fungu			**4,039,700,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa
na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu 0301 Ofisi Kuu Pemba

Mhe. Saleh Nassor Juma. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, wakati jana nachangia kwa masikitiko makubwa sana nilizungumzia jinsi ya Watendaji Pemba jinsi ambavyo wanatoa hati miliki katika ardhi ya Mzee Ayoub Suleiman na familia yake, pamoja na leo Waziri kwamba alitoa maelezo kuhusu yale lakini sikuridhika nayo kwa sababu makubaliano yale yalifanywa, lakini ni kwa sehemu tu ya ile shamba. Lakini juzi Mhe. Mwenyekiti, juzi juzi tu wamejenga banda jengine na wakakata miembe kwenye sehemu nyengine kabisa ya ile shamba pamoja kuchukuwa na sehemu ya makaburi ya shamba ya marehemu Ayoub Suleiman, jambo ambalo ni dhulma kwa ile familia, huku akipata majibu ya jeuri kwamba ni shamba la waarabu wacha tuchukue. Je Mhe. Waziri, pamoja na kwamba wewe ulitoa utetezi kwamba huna ubaguzi, mimi naamini huna ubaguzi lakini kile kinachoendelea Pemba kuendelea kumega lile shamba ni lini Wizara yako itafuata makubaliano ya mwanzo na kuacha kuendelea kuimega ile shamba na hiyo sehemu aliyoichukua ni lini watendaji wako wataenda kukaa na ile familia ili kufidia ile sehemu ya mazao waliochukua pamoja na kuacha yale makaburi yao kuendelea kuyafukia pale.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Muwakilishi kama hivi ifuatavyo:- nlipojibu ile hoja nilisema inawezekana kukawa kuna habari ya ziada ikawa mimi sijui, kwa sababu mimi sikai Pemba huenda kwa kazi mara moja moja kama ndio ipo mimi na yeye tushirikiane ili tufatilie kwa undani ili niweze kulishughulikia hili suala, mimi nilisema. Sasa kama ni kweli kuna eneo ambalo halimo katika eneo la ardhi ile ambayo ilipimwa kwa ajili ya skuli, lakini eneo hilo sasa limejengwa banda, lile eneo ambalo halimo hiyo ni dhulma. Kwa hiyo mimi niko tayari kusikilizana naye kwa vile hiyo sio yao labda wakubaliane wazee wa pale na huyo mwenye ardhi au vyenginevyo hilo banda livunjwe, maana lipo katika eneo silo. Kwa hivyo hili mimi na yeye tushirikiane katika kutatua tatizo hili.

Mhe.Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri, anisikilize vizuri, sikuzungumzia wazee wa pale nimezungumzia familia ya mzee Ayoub Suleiman na Uongozi wa Shule au Wizara ya Elimu, kwa hiyo makubaliano yote yatakayokwenda ni warithi wa mzee Ayoub Suleiman wakiongozwa na Suleiman Ayoub na wala sio wazee wa pale, sio makubaliano ya wazee wa pale, lile shamba lina hati miliki ya Marehemu Ayoub Suleiman. Kwa hivyo mimi katika hili Mhe. Waziri, nataka uniambie lini tuende kwa sababu hata ukiniambia mimi kesho niko tayari kwa sababu hii familia inapata shida na lile shamba ndilo wanalitegemea, leo kila siku inaendelea kuchukuliwa. Sasa makubaliano yote yatakayotokea naomba sana Mhe. Waziri, yasiwe baina ya wazee kwa sababu hilo shamba si la wazee wa Ndagoni ni shamba la familia la Mzee Ayoub Suleiman. Kwa hiyo mimi unambie ni lini tu tuende.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nataka mwenzangu anifahamu. Hapo pahala pana Skuli, wazee watu wa pale wameamua kuongeza banda kwa sababu pana matatizo, wazee wa pale wanaweza kuwasiliana na huyo muhusika wa lile eneo wakafikia makubaliano, maana na huyo mzee asili yake alikuwa anatoka pale pale Ndagoni, lakini yuko Vitongoji wanaweza wakakubaliana, lakini kama hawakukubaliana nishasema kabisa, kwa sababu silo eneo ambalo mipaka ipi inaonyesha hilo banda lipo katika eneo, kama halikukubaliana livunjwe, hawa wazee wachukue shamba lao tunakubali kabisa ndio haki hakuna njia nyengine. Sasa Wizara ya Elimu kama itakuwa na utaratibu mwengine wa kusema ah! basi tumechukuwa eneo lenu hili na sasa hivi tutakufidieni kiasi kadhaa, hii ni uamuzi wa Wizara ya Elimu, lakini mimi kama ni mtu wa kupima ardhi tumejenga katika eneo ambalo sikukupimia utaratibu wake ni kwamba hapo pahala umepavamia na pavunjwe basi hakuna utaratibu mwengine.

Kwa hiyo kama hawa wazee wa Ndagoni watakwenda kuzungumza na huyo Mzee Suleiman Ayoub wakikubaliana sisi tutafanyaje, lakini tuende mimi na yeye tukalitizame hilo sualam ndivyo nilivyokubali nataka na yeye anifahamu kwamba na mimi nina nia njema kwamba isichukuliwe ardhi ya mtu kinyume na ile tuliyoipima siye. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: nafikiri hakuna ubaya kuwahusisha wazee hawa, Wizara ya Elimu pamoja na huyo mwenye shamba, hakuna ubaya. Mimi nadhani itaweka muafaka zaidi.

Mhe. Saleh Nassor Juma: mimi napenda kumuhakikishia Mhe. Waziri, pamoja na Serikali hii kwamba hapo hapana shaka ile ardhi ni yao na malalamiko yao wamepeleka kwa Makamo wa Pili wa Rais, na barua tunayo lakini hadi leo haijapatikana ufumbuzi, katika hili kwa sababu tumeonyesha njia ya kupatikana suluhu hili suala Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu Mhe. Waziri, ameonyesha njia ya kupatikana suluhu ndani ya mwezi huu wa Ramadhan akiwa na kifungo pale mimi nadhani nikualiane nae kwa sababu yeye kama hakutekeleza atakuwa mas-ul kwa Mungu na kwa sababu kakubali hili mimi niko tayari hata kesho kulipatia suluhu hilo basi naomba tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: musije mukaenda siku za vikao vyangu naona mtanipunguzia quorum, mtafute Jumamosi au Jumapili itakuwa vizuri. Lakini mwezi wa Ramadhani sawa nadhani kama Waziri anakubali sawa, lakini mkienda kwenye siku za vikao aah!

Waziri nataka awepo na wewe nataka uwepo ili vikao hivi viende na Mawaziri wengine nao wakija wakawa miadi namna hiyo mwisho ntakuta vikao hivi haviendi maana watu wote wako kwenye safari, tafuteni muda muafaka ambao hautakwaza vikao vyangu.

kifungu	0301	Ofisi Kuu Pemba	1,116,007,000/=
kifungu	0302	Bodi ya Kudhibiti Kodi ya Nyumba	7,000,000/=
kifungu	0401		

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi hii nikapata maelezo ya ziada kutoka kwa Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mhe. Waziri kwa utulivu wake namna alivyokuwa akitujibu hoja zetu mbali mbali. Kwa kiasi fulani nadhani Mhe. Waziri wakati atapostaafu uwaziri anafaa kuwa Balozi, akateuliwa ubalozi nchi yoyote huko duniani kutokana na ule umahiri wake wa namna ya kutujibu.

Sasa hoja yangu iko hapa. Mhe. Mwenyekiti, nilimsikia Mhe. Waziri alipokuwa akinijibu katika hoja ya mtu ambaye sitaki nimtaje jina lakini nitataja cheo chake ambacho aliwahi kulitumikia Baraza hili. Na kwa bahati mbaya Mhe. Mwenyekiti, katika ile sheria ya kuwaenzi au kuwalinda viongozi hasa wanapostaafu kwa bahati mbaya Naibu wetu Spika anakuwa hayumo nadhani. Sasa kajitengenezea sheria yeye mwenyewe angalau ya kumsaidia kumlinda maisha yake baada ya kustaafu kazi. Mhe. Waziri katoa ufafanuzi mzuri hata na yeye anategemea akishastaafu kazi basi awe na vitu vitakavyoweza kumuendesha ili asiadhirike.

Mhe. Waziri amenieleza kwamba atalifanyia kazi, na amesema kwamba ndio kwanza amelipata. Sasa mimi kidogo Mhe. Mwenyekiti, kauli ile sikufichi kwa kweli sikuridhika nayo, sio sikuridhika nayo kutokana na kauli ya Mhe. Waziri, lakini watendaji wake hawamsaidii Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili lipo muda mrefu na huyu mwenzetu alikuwa kiongozi akiliendesha Baraza letu hili, leo wenzake ambao pengine hawako hata katika utaratibu wameruhusiwa kutumia maeneo yao katika eneo hilo hilo, yeye leo ndio kwanza tunaambiwa anaanza kwenda kufikiriwa. Mheshimiwa nimekuja mpaka na *document* yake hii hapa mana sio kama anataka kuvamia hili eneo tayari ana *document*. Sasa yale matumizi ya mwanzo kama nilivyosema katika mchango wangu kuweka kituo cha mafuta ya peroli pale ni kweli hata mimi nilipopaangalia kwa sababu mimi ninapopewa hoja nakwenda mpaka *site* kupaangalia ili nisije nikazungumza kitu ambacho hakina msingi.

Kituo cha Mafuta ya Petroli amekubaliana kwamba ameghairi kuweka, lakini afanye kama wanavyofanya wenzake ili tuweze kumsitiri mwenzetu huyu, leo Mhe. Mwenyekiti, ni aibu mambo mengine kunga ambayo hiyo hali yake sasa hivi mambo mengine kunga. Wewe mwenyewe Mhe. Mwenyekiti, unajua. Sasa Mhe. Waziri kama nilivyosema kwamba ukifika watendaji wako kawagombe kwamba hawakukutendea

haki. Hivyo mimi nataka maelezo kwa sababu hili suala linajulikana angalau ndani ya mwezi mmoja na mimi sitaki anishirikishe amwite yeye mwenyewe amshirikishe na kwa sababu hawa watendaji Mhe. Mwenyekiti, huyu tunaemzungumza hapa kawalea tena kawasomesha na sasa hivi wana vyeo vikubwa ndani ya wizara hiyo. Sasa hebu kidogo Mhe. Waziri anipe kauli ya ziada ili niweze kuridhika kuachia fungu hili.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, mimi namshukuru sana Mhe. Hamza kwa sifa alizonitandikia, *Inshaallha* Mwenyezi Mungu anijaalie kama hazijawa basi ziwe naomba dua hiyo mana ni sifa nzuri. Mtu mwenzio akikutakia sifa nzuri bwana ni vizuri ushukuru kwamba ameanza kukuombea dua, mana sifa nzuri kumwambia mtu ni dua hasa katika mwezi huu wa Ramadhani. Sasa Mhe. Hamza ana swaumu pale dua yake inapanda tu moja kwa moja.

Lakini hata hivyo Mhe. Mwenyekiti, nasemaje mimi keshanisaidia kazi, analijibu swali ambalo mimi nilikuwa nataka nilijue, aliposema kwamba huyo mwenyewe keshaghairi sasa hivi kwa kituo cha mafuta ya petroli hiyo ameshanisaidia kazi. Sasa mimi ni kwenda kupaona tu halafu nikafanya uamuzi basi hakuna tatizo jengine mana keshanisaidia kazi. Kwa sababu mimi nilifikiri mwenyewe anang'ang'ania bado aendelee kuwa na *petrol station* lakini hivyo alivyosema yeye basi keshanisaidia kazi *inshaallah*. Kwa hivyo, nitakwenda kupaona hapo pahala na nitamfata hasa kwake nizungumze naye anakusudia kufanya nini hapo mahala, kama hapana hatari kwa nini nisimpe na yeye ana haki, lazima nitampa. Inshaallah ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Mjumbe anapendekeza kama mwezi mmoja hivi imalizike, unasemaje juu ya hilo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, kama nitakwenda kesho na nitaona hapo mahala kwamba pazuri mwezi mmoja wa nini, si niamue tu. *(Makofi)*

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya huyo mwenye hilo eneo namshukuru sana Mhe. Waziri kwa kauli yake hiyo naomba tuendelee.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nisiwe mwingi wa fadhila kutokumshukuru Mhe. Waziri amejipanga vizuri na ana *experience* nzuri. Mhe. Mwenyekiti, amenijibu nimeridhika, lakini kuna sehemu ambayo hata mimi niweze kusema sisemi kama watendaji wake hawakumfahamisha vizuri. Mimi ni mmoja katika mtetezi wa wanyonge, Mhe. Waziri amenijibu suala la yule kijana lakini hakupata ufafanuzi mzuri Mhe. Waziri, naomba niwe mtiifu kwake kumpa ufafanuzi vizuri na sitaki niitengue Alhajj yake aliyokwenda Makka ili aweze kwenda safi na mara nyengine tena na mimi aweze kunichukua.

Mhe. Mwenyekiti, nilisema kwamba nimemtetea huyu mnyonge ambaye alikuwa Mhasibu katika sehemu hiyo simsemi yule aliyekuwa *owner* wa lile tatizo yule mimi simtaki. Kwa sababu yule ndiye sababu ya yote haya kufanya mwenzake huyu aondoshwe. Kulikuwa na *cashier*, mhasibu, sasa huyu mhasibu ambaye yeye

amesimamishwa alipewa barua rasmi ya kuomba kwenda kusoma na wakati ule alipokwenda kusoma haya madudu ndio yalikuwa yakifanyika. Sasa pale alipoondoka aliitoa barua vizuri halafu akasema kuwa mimi atakayeweza kunirithi sehemu ile ni huyu na ikatolewa kimaandishi.

Lakini cha kushangaza Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri wangu labda hajapata *good history* yule amekuja kusimamishwa aliyekuwa nje na kile kitendo chenyewe. Sasa hapa mimi ndio namlilia haki yake yule kijana kuwa huyo aliyetaka kupelekwa akakatishwa kwa sababu kafanya *forgery* nyingi, amefanya *forgery* ya *bank statement*, *forgery* za *cheque*, huyu aliyekuwa yeye hakutia mkono wake halafu yule aliyekuwa mrithi wake yeye hakusimamishwa kazi kasimamishwa kazi huyu masikini ya Mungu. Sasa ningeomba hapa Mhe. Waziri amuone kwa jicho la huruma huyu ambaye yeye hakuwepo pale amesimamishwa. Sitaki kuzuia fungu hata kidogo isipokuwa naomba anihakikishie huyu kijana kuwa atarejeshwa kazini kwa mujibu wa taratibu kwa sababu yeye hayumo katika yaumu shaka ya kitendo kile kilichofanywa.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: mhe. Mwenyekiti, mimi nakubali sana *concern* ya Mhe. Makame Mshimba, *concern* ni nzuri sana, kama mtu hakufanya kosa ni vizuri akaachiwa hayo nakubaliana naye sana. Lakini sasa hivi tumewapa wenzetu walichunguze hili suala je, katika hizo *document* zinazohusika hakuna mahala ambamo amesaini yeye hizo *document*. Sasa kwa nini tusitoe nafasi, tutoe nafasi. Maelezo yake hapa Barazani yatawafanya wale waliona kesi mkononi kuhakikisha kwamba wanakamilisha hili suala na ndio madhumuni ya chombo hiki, chombo hiki Mhe. Mwenyekiti, kiliitwa ngome ya wananchi ili wananchi wanapopata matatizo wanakuja katika chombo hiki na wanatatuliwa.

Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi alipoanzisha pale Kikwajuni alisema neno hilo. Kwa hivyo, nakubaliana naye lakini mimi siwezi kuvamia madhali tumepeleka kwenye vyombo vya sheria wao wanafanya uchunguzi wao. Kwa hivyo, mchango wake ndani na Baraza hili utasaidia kutoa huo ukweli wa hilo suala kama nilivyosema hili suala halijathibitishwa, lithibitishwe na ikawa hahusiki kwa nini aendelee kuteseka akae nje, tena nakubaliana naye na *concern* yake na mimi namuunga mkono kabisa katika hilo, lakini tuache chombo kifanye kazi.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, sikusoma sheria lakini nina ufumbuzi wa kujua sheria. Huyu mtu ana miezi 11 na sheria inasema miezi sita tu awe kila kitu ameshaamuliwa kama wanasheria wapo watanisaidia kama nakwenda *wrong*, sasa hivi ana miezi 11 na zaidi. Lakini vile vile tukubaliane kitu kimoja Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Mhe. Waziri nyinyi hamumuelewi ana tabia moja ya ukweli mimi namfahamu, anasema kwamba tuachie sheria na mimi sheria sitaki niipinge ni moja katika muhimili nao tuuheshimu. Lakini nina *reference* ya kesi kama hizi sheria imefuata mkondo wake ilifika limit time ya kusema kwamba huyu mtu sasa alipwe fedha serikali ikawa ngumu kulipa, wasi wasi wangu hapa. Mimi najua kama ningekuwa wakili wake nashinda tu sina wasi wasi kwa sababu hana doa.

Lakini wasi wasi wangu Mhe. Mwenyekiti, kuwa baadae serikali itakataa kumlipa mafao yake yale yaliyokuwa bakaa hilo ndio wasiwasi wangu Mhe. Mwenyekiti. Sasa kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri *concern* yake nimeikubali kuwa chombo cha sheria kikubali, lakini baadae Mungu akimjaalia akiwa katika wizara hii awe *very sharp* ya kuja kumlipa yule mtu mafao yake yote aliyokaa huko nje. Hilo Mheshimiwa na mimi naomba kwenye *hansard* likubalike hilo kama wenzangu walikuwa wakidai *hansard* ndio kumbukumbu zetu basi na mimi naomba.

Mhe. Mwenyekiti, kwa taadhima naomba tuendelee.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia kuhusu masuala ya maji Moga Mwembe Mkali na Kinyasini pamoja na Banda Maji kuhusu ahadi za Mhe. Rais pamoja na mawaziri waliopita ambao walikuwa ni mawaziri wa Maji na Nishati. Nilimueleza Mhe. Waziri kwamba anieleze angalau kwa sasa lini pengine visima hivi vitaanza kuchimbwa kutokana na kwamba sasa hivi muda wa miaka arobaini na tisa na nusu ni muda mkubwa kwa binadamu kukosa haki yake hiyo ya msingi ya maji. Sasa kila siku katika bajeti zinazopita naziona hapa kwamba visima hivi vinatajwa lakini uchimbaji wake hautekelezwi Mheshimiwa.

Kwa hivyo, kwa kuwa sasa hivi anasema kuna mradi wa Ras-el-Khaima angenambia labda lini, pengine hata tukiingia mwezi Januari katika sherehe za miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar kwamba wananchi hao kwa mara ya mwanzo waanze kufurahia haki yao hii ya kupata maji safi na salama. Hapa ningeliona kidogo Mhe. Waziri amenitendea haki mimi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Chaani.

Lakini jengine kuhusu masuala ya umeme Moga Kirama. Mhe. Mwenyekiti, katika vikao mbali mbali nimekuwa nikiuliza maswali mengi tu kuhusiana na umeme wa Moga Kirama ambako kulikuwa na ahadi ya Mhe. Waziri aliyepita, mawaziri wawili waliopita hivi juzi tu wamenambia kwamba umeme wa Moga Kirama bajeti ijayo tutaupeleka sasa hivi tukishapitisha bajeti hii ni ya tatu. Mhe. Waziri nilimwambia kwamba, sisi tuko tayari kuchangia kwa sababu huko nyuma tulichangia tukatafuta nguzo zetu wakakaa mpaka nguzo zile zikapitwa na wakati kwa maelezo yao kuwa nguzo zile hazifai. Kwa hivyo, tumekula hasara kwa mara ya mwanzo.

Juzi wakati nikichangia bajeti hii nilimwambia Mhe. Waziri kwamba sisi kwa kuwa tulitaka tuchangie tuko tayari kuchangia na nikamtaka atwambie kuanzia lini yeye atakuwa tayari kutupelekea umeme. Kwa hivyo, sisi fedha za kuchangia tunazo katika mifuko yetu atwambie lini tumpelekee fedha na yeye atwambie lini kazi yetu ya umeme kule Moga Kirama itaanza hilo tu mheshimiwa sina nia ya kuzuia fungu. Lakini kwa majibu rahisi mepesi tu kutokana na shida zilizopo anavyojibu mimi naona hazinipi moyo, haya matatizo ni makubwa na ya muda mrefu kwa hivyo ilikuwa angalau na majibu yake basi nayo yawe mazito kidogo kama mimi ninavyoonesha hisia yangu dhidi ya watu wangu hawa namna wanavyopata shida. Mhe. Mwenyekiti, naomba nipate maelezo ya ziada.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, nilipoanza kujibu hoja pale nilisema kwamba nimezungumza na wenzangu na kuwaambia ahidini mtakaloliweza na msiloliweza bora mseme kwamba hili hatuliwezi. Sasa katika hali hiyo Mheshimiwa alizungumza kwamba kule kuna ahadi nyingi zilitoka, naogopa kusema kujifanya kwamba mimi ndiye hodari kuliko wenzangu waliotangulia. Ila mimi namwambia kwamba, mimi nitasimamia suala lake la maji pale na ndio maana nikasema Ras-el-Khaima tushawapangia pale hivi sasa wakachimbe kisima ili tupate maji pale. Labda ninaloweza kulifanya ni kupangua *schedule*, sasa nani utampangulia *schedule*, kumuondoshea kwake kumpelekea yeye ni tatizo jengine hilo.

Lakini pale tunakwenda kuchimba kisima ndani ya siku hizi tulizonazo, Ras-el-Khaima tayari wapo wanafanya kazi ya kuchimba visima hapa, wako tayari kabisa. Hilo suala mimi nitalishughulikia aniamini kwamba nitalishughulikia. Yeye peke yake kunijia kwa mambo kama hayo ndio tunashirikiana.

Mhe. Mwenyekiti, hao ni wenzangu bwana, na mimi nilikuwa Mwakilishi wa jimbo nayaelewa wanayoyapata hawa vizuri kabisa nayaelewa wanayoyapata, na ninajua kwamba wanashindwa wakati mwengine inapokuwa suala limekaa muda mrefu umeahidiwa halijatekelezwa unashindwa hata kupita katika kitongoji kile naelewa mimi hilo suala, naelewa vizuri sana.

Kwa hivyo, Ras-el-Khaima watakwenda kuchimba kisima katika eneo hilo, wakimaliza tu hapa mjini watakapokwenda vijijini watakwenda Chaani mana sasa hivi wako mjini. Kwa hivyo, Mhe. Ussi aniamini hivyo kwamba kisima kule kitachimbwa, Mwenyezi Mungu anijaalie anipe uhai na yeye ampe uhai katika bajeti hii hii tutachimba kisima Chaani.

Kuna suala la umeme. Suala la umeme hapa nataka kusema pamoja na faida ya Wajumbe wenzangu, unajua Waheshimiwa hawa wanakula hasara sana kwenye masuala ya umeme kwa sababu ya hamu, hamu ina matatizo yake Mhe. Mwenyekiti. Wanakwenda kununua nguzo lakini zile nguzo *lifespan* yake ni miaka miwili tu. Lakini sasa kwa sababu wanataka kupeleka umeme mahala anasema mimi nitanunua, ananunua, ukinunua sasa watu wa *ZECO* wanasema hapana nguzo sasa hivi lazima ziwe standard, tutumie nguzo ambazo ni *standard* tusitumie nguzo hizi.

Tumepata matatizo juzi tu hapa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais amekwenda kutembelea Michamvi kuloe kakuta nguzo chungunzima zimekatika katika kwa sababu *lifespan* yale ni miaka miwili. Nguzo ya umeme ambayo watu wa umeme wanataka itumike sasa hivi haipungui *lifespan* yake miaka 20 angalau tunapata wakati mzuri. Sasa katika hali hiyo namuomba Mheshimiwa kwamba hili suala bado sitaki kumjibu hapa moja kwa moja bila ya mimi kushirikiana na yeye, kwanza nipeleke mafundi wangu wakazione hizo nguzo zake alizoambiwa hazifai kweli ni nguzo zilizokuwa haziko katika *standard*, mimi nitashirikiana na madhali keshasema yuko tayari kutoa mchango hiyo minalfaidhina, yeye akitoa mchango na sisi tukitoa mchango basi tutakwenda vizuri tu. Hilo namuahidi mimi Mhe. Ussi nayajua matatizo yake anayoyapata Chaani, pamoja na kuwa si jimbo

langu lile hizo habari nazipata mimi, natembea sana huko na najua matatizo aliyonayo ni haki yake tutamfanyia *Inshaallah*.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Mhe. Mwenyekiti, hili suala la visima vya maji sasa hivi sina mashaka nalo ila suala la umeme. Kwanza nataka nimwambie kwamba suala la nguzo tumeachana nalo baada ya wataalamu wake kutueleza nguzo zile kuwa hazifai. Sisi si wataalamu wa umeme ni wataalamu wa mambo mengine hatujui mambo hayo. Kwa hivyo, nguzo za Moga Kirama hizo tushaachana nazo, tulichokuwa tunamwambia sisi kwa sasa tunazo fedha nyingi ambazo hizo tutashirikiana naye katika kumaliza hili tatizo. Nguzo zile tushaziacha kabisa hazipo katika hesabu yetu tunasubiri nguzo ambazo zinaishi kwa muda mrefu zinazopatikana katika Shirika la Umeme na ndio maana tunawasubiri wao.

Sisi tunazo fedha za kuanzia za kuchangia jambo hilo kwa hivyo, yeye tusijadili tena nguzo zilizopita, sasa hivi tujadili nguzo zake imara zilizopo fedha tunazo atwambie tu lini tutaanza hiyo kazi, kwa sababu muda mrefu sana. Kwa hivyo, hatutaki nguzo zetu sisi ambazo tumeuziwa zilizokuwa feki tunataka hizo mpya za kwake yeye na pesa tunazo atwambie lini tutaanza hii kazi. Kwa sababu tatizo hili la muda mrefu Mheshimiwa, watu kukaa kwa muda wa miaka 49 na nusu kwamba huduma wenzao wanaipata wao wakawa hawapati inakuwa si kitu kizuri.

Sasa atueleze tu kwamba lini tukaanze hiyo kazi kwa pamoja sisi tuko tayari mbona Mheshimiwa. Kama atanambia kwamba tutaanza lini kwa sababu hicho kitu kinajulikana cha miaka mingi, kila siku yeye ananiahidi kwenye bajeti, bajeti iliyopita ameniahidi, kwenye vitabu vyake vyote toka tuanze mwaka 2010 tulipoingia hapa mpaka leo vitabu vyote vinazungumza bajeti ijayo, bajeti ijayo. Sasa ina maana Mhe. Waziri mpaka hii leo hajajua tu kwamba pengine kazi ya Moga itaanza lini au halitilii umakini hili suala na anaona pengine suala la kawaida tu halina uzito wowote. Kwa sababu mpaka leo tunakuja bajeti hii ya tatu tunapitisha. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi Mhe. Waziri nilikuwa nataka atwambie angalau tutaanza lini basi tumpelekee hizo fedha sisi tuko tayari Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, maneno yake yanazidi kunitia tama kuona kwamba huu mradi kumbwe utakwenda, anaposema kwamba mapesa mengi wanayo Mheshimiwa mimi ananitia tama kwamba huu mradi utakwenda. Kwa hivyo, watu wangu wa *ZECO* wamesikia pale na nina hakika wako tayari kuonana naye hata kesho au keshokutwa wakatizame kwa pesa zake nguzo ngapi atapata, na kama nguzo atakazozimudu yeye zinafika robo tatu naji-*commit* kabisa kama zinafika robo tatu ya hizo zinazohitajika basi robo moja itatoa *ZECO* watamalizia. Mimi niko tayari kufanya hivyo na washasikia pale. Hilo ni agizo na Meneja ananisikia robo moja watoe *ZECO* robo tatu atoe yeye, tuko tayari sisi *Inshaallah* na mambo mengine tuta-*negotiate* kipi na kipi tusaidiane kama tunavyo-*negotiate* katika mambo mengine kipi tusaidiane, kipi hivi tutafanya hilo Mhe. Mwenyekiti.

Mimi ananitia tamaa sana kwa maneno yake kuwa huu mradi kumbe wala si wakunisumbua mimi nikapata masuala hapa. Mapesa anayo bwana sio mchezo.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Mhe. Mwenyekiti, naona leo kwa mara ya kwanza Mhe. Waziri ananipa moyo kwa hivyo naomba tuendelee, tutamsubiri keshokutwa hapa.

Kifungu 0401 Idara ya Mipango Sera na Utafiti 184,377,000/-
Kifungu 0402 Mamlaka ya Maji Zanzibar

Mhe. Farida Amour Mohamed: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilizungumzia kuhusu suala la wananchi wanaoishi katika Kisiwa cha Uvinje Jimbo la Gando, Wilaya ya Wete. Nimemsikiliza kwa makini Mhe. Waziri alipokuwa akijibu masuala hayo lakini sikuridhika na majibu yake. Kwa sababu katika tatizo lake alilolizungumza ni kuhusu kukamilika kwa miundombinu ya barabara ya Ukundwi. Barabara ile tayari imeshapigwa *grader* mwaka mzima na karibu itatiwa lami, na kwa kuwa hii hali ni ya hatari sana kwa wananchi wale wanaoishi katika Kisiwa cha Uvinje na baadhi ya watu wanaoishi katima maeneo ya mijini katika tatizo hili la kukosa maji hasa kwa mwezi mtukufu huu wa Ramadhani huwa wanapelekewa maji kwa vigari.

Sasa wale watu wa kisiwa watatumia mbinu gani ya kupelekewa maji angalau na wao kuwasaidia katika maisha yao, upepo huu wapande mitumbwi wende Wete wakatafute maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na mwezi wa Ramadhani matumizi ya maji yanaongezeka. Sasa hapa namuomba Mhe. Waziri anipe angalau majibu mazuri yatakayoleta matumaini kwa watu hawa wa Kisiwa cha Uvinje kwani wamo katika hali ngumu sana ya maisha. Mhe. Waziri namuomba sana atumie hekima na busara zake atafute majibu mazuri angalau ya kuwatia moyo hawa wananchi waone kama serikali yao inawajali na inawaonea huruma.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, *concern* ya Mhe. Mwakilishi na hasa kwa kuwa mwanamke nafahamu namna yanavyomuuma, mana katika utamaduni wetu wanawake ndio wanahangaika sana katika masuala ya kutafuta maji kuliko sisi wanaume. Sisi huuliza tu, maji ya kukoga umeniwekea? Ndio masuala yetu hayo. Lakini wanawake wao ndio wanaohangaika kutafuta maji hapa na pale. Kwa hivyo, masuala yake ni muhimu sana na ni kweli.

Lakini sasa Mhe. Mwenyekiti, analoliomba ni suala la bu, ba, leo kwa kesho mana Ramadhani ndio tunayo hii. Kweli barabara ile imeshapigwa *grader* lakini kazi ya ujenzi wa barabara ile haijamalizika bado na kwa miporomoko iliyopo pale bado matatizo ya mabomba yataendelea kutokea hasa kwa sababu haijamaliza, ikimalizika tutajua kuwa mahala gani kuko vizuri na mahala gani hakuko vizuri. Sasa labda ningelikuwa na boti nikaweza kuchukua maji kwenye boti nikayapeleka Uvinje, lakini bahati mbaya sina boti mimi.

Je, watu wake watakubali kwamba tutafute gari la maji tuwashushie pale pwani wawe wanakuja wakichukua maji kupeleka kule. Hilo mimi sina tatizo nalo kama wataliweza

watu wake, lakini kwa kusema kwamba kule nipeleke boti siwezi kumwambia uongo Mheshimiwa sina boti la kupeleka maji mpaka kule, lakini mpaka pale kwenye bahari naweza nikapeleka maji kama wanaweza kuja kuchukua pale kupunguza safari ya kwenda Wete. *Inshaallah* tutatafuta gari tutakodi tutapeleka maji pale.

Mhe. Farida Amour Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, naomba nimshukuru Mhe. Waziri kwa angalau kujenga ile imani ya watu wangu wa Kisiwa cha Uvinje. Sasa kwa vile wao wanataka angalau wapate msaada wa aina yoyote wa kuwarahisishia zile kazi zao, naomba awafanyie hilo. Tuendelee.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilitaja vijiji vingi katika Shehia zangu tano za Jimbo la Mtambwe ambavyo vina matatizo ya maji. Mhe. Waziri alipojibu alizungumzia Shehia ya Mtambwe Kusini tu na kidogo akaihusisha na mradi wa *TASAF* ambao watu walichagua barabara badala ya miradi mingine barabara ambayo mimi mwenyewe katika akili yangu siioni. Sasa sikupata jibu la kuridhisha hasa kuhusu maji kwa huku Mtambwe Kusini. Hilo ni moja naomba nipate maelezo.

Halafu pili, kitabu chake kimesema kwamba kuna vijiji ambavyo havikupata maji katika bajeti iliyopita na vilikuwemo, kitabu kinaeleza kuwa vile vijiji ambavyo bado vitashughulikiwa katika kipindi hiki cha fedha au ni siku za mbele zijazo kwa Mtambwe Kaskazini. Naomba majibu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, unajua kuahidi hapa kwa sababu tu hoja yako ipite si vizuri, ni vizuri uone hasa hilo tatizo uweze kujua namna ya kulitatua tatizo hilo. Lakini hapa unaahidi kuwa mimi nitafanya, mimi nitafanya si uzuri. Watu wa Idara ya Maji wapo mimi nishamjibu hoja, hoja haikumridhisha mimi na yeye Mheshimiwa niko tayari nitakwenda Pemba nitakaa kama wiki mbili twende katika maeneo mbali mbali yake yeye, ya Mhe. Abdalla Juma na wengineo ili nione hasa hali halisi yale masuala yenyewe ili na mimi niweze kushirikiana na wenzangu katika kufanya uamuzi. Kwa hivyo, sitaki kushindana naye katika hilo, kama anaona kuna matatizo lakini ninachokijua mimi ni kwamba ilikuwa maji yapelekwe na *TASAF* na bahati mbaya wao kipaumbele chao kilikuwa ni njia. Kwa hivyo, sijui kama wamejenga hiyo njia au hawakujenga, lakini najua kipaumbele ilikuwa njia.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nilisema katika jibu langu jukumu la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kupeleka maji kwa wananchi, hilo nalikubali kabisa na katika SMZ wizara yangu inahusika na jukumu hilo. Kwa hivyo, mimi na yeye Mheshimiwa bora tushirikiane kwa vitendo kwenye suala hili tusilizungumze hapa tu itakuwa tunababaishana, bora anipeleke tukaona mimi na yeye halafu tutafanya uamuzi *Inshaallah*.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kusema kuwa twende tukaone huko Kusini kulivyo, lakini ningeliomba tu nijue ni lini.

Na pili, kwa huku Mtambwe Kaskazini ambako yeye mwenyewe kwa mujibu wa majibu yake ni kuwa safari hii itashughulikiwa. Lakini katika suala langu juzi niliambiwa kuwa kuna mfadhili atapelekwa huko mfadhili ambaye mimi simjui. Kwa hivyo, na hapa napo nataka nipate ufafanuzi wa kutosha nijue tunakoendelea.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, mimi sina zaidi isipokuwa huko Kaskazini nitamfuatilia huyo mfadhili na kwa huko Kusini tutakwenda mimi na yeye akanioneshe tufanye kazi. Kwa sababu siwezi kujibu hapa nataka hii bajeti ipite hapana, tunatakiwa tufanye kazi.

Mhe. Mwenyekiti: Basi mtafute siku muwafaka mwende huko siku ambazo hazitakuwa za vikao vyangu vya hapa. Nadhani mwaka huu.

Mhe. Saleh Abdalla Hamad: Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata jibu lakini sijajua ni lini. Kwa sababu jambo linaloniumiza hakukaliki na kule hakwendeki bajeti inamaliza hii. Nataka nijuwe ni lini tuondoke twende.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, kama ingelikuwa baada ya kumaliza hotuba yangu wa Wizara yangu ya Wizara ya Kilimo utaniruhusu niondoke na yeye twende ningekwenda la vyenginevyo itabidi tumalize kikao hiki cha bajeti halafu tupange safari ya kwenda hakuna njia nyengine.

Mhe. Mwenyekiti: Nashauri bora tumalize vikao hivi maana nataka muuelewe tu Mhe. Waziri Ramadhani Abdalla Shaambani ni mmoja kati ya *spear part* ya Serikali. Kwa hiyo, tusubiri tumalize kwa sababu tunamuhitaji sana kwa mambo mengine huyu.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante Mhe. Mwenyekiti,nilizungumzia sana kwamba Serikali yetu ingelikuwa binaadamu basi tungemwita mlemavu kama utakuwa unakumbukumbu nzuri. Juzi wakati nilipokuwa nachangia nilisema kwamba ingelikuwa hii Serikali ni binaadamu basi tungemwita ni mlemavu.

Nilisema hivyo kwa msingi kwamba wakati Mhe. Waziri anazungumzia kuhusu vyanzo vya maji amezungumzia sana kwamba kuna uwezo wa maji kutoka chini ya Ardhi tu hakuna uwezo wa kupta maji kutoka baharini *distilled water* kwa *soft water* hatuna uwezo huo. Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi katika mchango wangu nilisikitika sana kwamba wenzetu wengine wamepata uhuru juzi hapa wamemudu kufanya mambo mengi nchi ambazo juzi juzi tu zimepata uhuru.

Sisi tunashinda kuweka ma- *distillery* hayo ya kuji-*distilled sofy water*. Sasa nilihoji kwamba ukizungumzia *ZAWA* Mhe. Mwenyekiti, unazungumzia *two in one* maana yake unazungumzia maji safi na maji taka. Sasa kila upande *ZAWA* wamekuwa walemavu. Kwa mfano wanategemea hivi vyanzo vya chini ya ardhi ambazo sasa kutokana na mabadiliko ya tabia ya nchi hazikidhi haja ya kutosheleza kwa sababu maji yanapatikana chini sana kiasi kuwa ni tatizo.

Ni lini *ZAWA* kwa sababu hamna uwezo wa kuyatoa maji chimvi na kuyafanya yakawa ya kunywa na kutumia.

(a) Ni lini maji taka mtaweza kuya- *recycle* kwa jenga *water treatment plan* ambayo yale maji tuta *recycle* kutumia tena sisi binaadamu kama wanavyofanya nchi za wenzetu hata hizi nchini zilizoko kusini mwaka Jangwa la Sahara. Ili haya maji taka tuya *recycle again* tuweze kutumia kwa mwagiliaji pamoja na kilimo ili

tuweze kutekeleza mpango huu wa kuondosha umasikini na kuongeza kipato wa *MKUZA* ili tuweze kuutekeleza. Ni lini mtajenga mitambo ili haya maji taka yawe safi tuweze kuyatumia kwa umwagiliaji ili kutekeleza *MKUZA II* ambao una sehemu ya kupunguza umasikini na kuongeza kipato.

(b) Nilisema kwamba unapopita Mji Mkongwe siku hizi ikiwa una nguo zako za kusalia basi nakuhakikishia itabidi ukabalishe kwa sababu mnashindwa kudhibiti miundombinu ya maji taka. Kutokana na maji yanamwagika ukipita yanakurukia kwenye nguo za kusalia huku yakiwa yanakinyesi na mambo mengine. Sasa ni lini na mkakati gani mmeuandaa ili kudhibiti yake maji taka yasitumwagikie ovyo na kuanza kuondoa ibada zetu hususan katika kipindi hiki cha mwezi wa Ramadhani.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, mchango wa Mheshimiwa mzuri sana. Lakini hilo suala la *recycle* maji, kwanza inabidi kutengeneza miundombinu ya kuyakusanya hayo maji taka, maana maji taka yanatoka mahotelini majumbani wanayotumiwa na watu wale yakusanywa kule kwa utaratibu maalumu kwa kwenda kuya- *recycle* yanatoka katika viwanda vile vile halafu na mengine yanapatikana vile vile kutoka katika mvua zinazonyesha za kawaida.

Kwa hivyo, suala la mvua tunaweza kufanya utaratibu wa kuyakusanya maji ya mvua mahala baada ya kwenda baharini wenzetu kule China huwa wanayakeka kule baada ya kwenda baharini huwa wanayaweka pahala wanagenja *lambo* kubwa wanayaweka halafu yale yakizama chini na yakizama yanaweza kujitegeneza *water table* ya maji iliyoko ardhi. Kwa hivyo yanajisafisha *natural* kabisa kwa kutumia ile chunguo za Mwenyezi Mungu alizoziweka chini ya ardhi ambayo yanatumika.
Sisi kwetu kweli yanakwenda baharini lakini hiyo tunaweza kufanya lakini inabidi tufanye utaratibu mzuri wa kuwaelimisha watu wetu masuala ya kukusanya maji na kupata maeneo ya ardhi ambayo unaweza ukayakusanya maji ya mto Mwanakombo, sijui ya mto gani baada ya kwenda baharini unakusanye mahala yazame yende chini na hapo mahala pasiwe panatumika tena ili maji yende chini pale na ukinyanyua *water table* yetu kuondoa tatizo hili la kuondoa tabia ya nchi.

Kwa hivyo, mawazo yake ni mazuri lazima tuseme tukubali si ulemavu gharama hata hiyo *distillation*. Hata hiyo *distillation* sisi tumeanza *project* ndogo ndogo za Pemba kuna kisiwa kile cha Kokota na hapa Unguja Chake pale maji wanatengenzwa. Sasa sio ulemavu hivyo mimi kama nataka kuvaa koti la laki na viatu lakini siwezi kuvimilikia itakuwa ni mlemavu, si ulemavu. Kwa hivyo, Mhe. Muasisi ajue si umelamavu ni *struggles* za kunyanyua uchumi wetu ili uchumi wetu uweze kunyanyuka na kuweza kufanya mambo hayo.

Hivi sasa tunajaribu kutengeneza hii miradi ya maji ili kujitosheleza kwa maji na mimi nina matumaini kama tunaweza kuja kufanikiwa *inshaallah* Mwenyezi Mungu akipenda. Kwa hivyo, tutizame hii miradi yetu tena wala sio mbali mwisho mwaka ujao tu tutajua tumefika hatua gani. Mhe. Ali Juma Shamuhuna alipokuwa waziri hapa alijitahidi sana kwenye masuala haya ya kutaka kutatua tatizo la maji, kijiti kaniachie mimi sasa.

Sasa na mimi najaribu kushirikiana na wenzangu kule tuone kwamba tunaweza kutatua tatizo hili la maji katika nchi yetu. Tunaweza kutatua kwa hiyo si ulemavu Mhe. Mwenyekiti, hilo ni jibu suala la uwezo. Lakini kama tuna uwezo tunaweza tukafanya.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, tendo hukidhi haja maridhawa siku zote kuliko neno. Haja ikishughulikiwa kwa matendo hupatikana wepesi. Lakini ikishughulikiwa kwa maneno hutolewa kama sadaka. Nashukuru kwamba Mhe. Mohammed Aboud kazunguka kulinisiliza.

Mhe.Mwenyekiti, nimelazimika kusema hivyo kwa sababu kula uhondo kunataka matendo, pasipo matendo hula muvundo siku zote. Pamoja na gharama Mhe. Mwenyekiti, Jimbo la Chake Chake lile la Mhe. Omar Ali Shehe lina mtaro mkubwa ule wa msingini..

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa Mjumbe hebu tusaidiane maelezo ametoa umaridhika nayo au hurudhiki nayo. Sasa ukitoa maelezo marefu muda hakuna.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, katika hili nilifikikiria tu kwamba waziri anieleze kwa mfano yale maji yameshachujwa katika ule mtaro wa kutoka msingi mpaka huku chini banda la taka ambayo tayari mradi ule uligharimu pesa nyingi na maji yale yameshapungua uchafu na baadae yakeshachujwa yanamwagika baharini kule huku yameshafanyiwa usafi lakini yanaachiwa tu kumwagika baharini ni lini watayafanyia utaratibu yale kuyachukuwa kusudi yaweze kutusaidia kwa kuwapa mifugo yetu pale katika mtaro uliopo Chake Chake. Ni lini wataanza kuweka miundo mbinu angalau ya kuvuna haya maji ya mvua lini ili isionekane kama Serikali yetu yetu ni lemavu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, maelezo labda ya kukubaliana na yeye tu kwenye suala hili. Mawazo yake Mhe. Mwenyekiti, nimemwambia ni mazuri tatizo letu ni uwezo tu basi si kama maelezo yake hayana maana ni muasisi na anayasema kwa uchungu hayo.

Na kayasema kwa uchungu kabisa kwa hivyo kumwambilia lini tutafanya suala linahitaji fedha bajeti ndio inapita hii hamna pesa hizo za kufanyia kazi hizo. Sasa kwa hivyo, sijui niahidi vipi hapa sitaki kuahidi jambo ambalo siliwezi kwa sasa hivi. Nayachukuwa kwa kuyafanyia kazi.

Kifungu 0402 - Mamlaka ya Maji Zanzibar 2,200,000,000/=
Kifungu 0401 - Idara ya Ujenzi

Mhe. Mbarouk Wadi Musssa: Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu huo huo wa maandishi huo niliuliuzia kuhuhusu ile kadhia iliyokuwepo ya watu wanaodai nyumba zile ambazo wamepewa na marehemu Mzee Karume. Mhe. Naibu Waziri alijaribu kulijibu hapa lakini halikuwa na ufafanuzi mzuri.

Lakini mwaka jana Mhe. Waziri katika hotuba yake hapa alitwambia kwamba lile suala kukamilisha. Sasa katika kipindi cha mwaka mzima nilikuwa nataka kujua kwa sasa ile ripoti imefikia wapi na ufumbuzi wa tatizo lile limefikia wapi.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme tu kwamba ripoti kama nilivyokwisha kusema katika majumuisho yangu maana kuna mtu aliuza na nikawambia.

Kusema kweli mwaka jana ripoti nilimwambia kuwa iko katika meza yangu. Kuondoka hapa nikaitoa na kupitisha katika vikao mbali mbali na vikao mbali mbali wameitizama. Hivi sasa watu wa Kamati wa Makatibu Wakuu wanatakiwa kuipangia siku kuimaliza ili ije katika Baraza la Mapinduzi ndio lililobaki.

Sasa kweli amesema mwaka mzima lakini kuna mikutano mingi sana na kuna nyaraka nyingi muhimu ambazo tunazishughulikia na katika suala hili ni lazima tutizame vizuri sana tusije tukalivamia, wengine kweli wamepewa nyumba zile na Marehemu Mzee Karume na wengine pengine hawakupewa hatuna uhakika. Lakini ripoti imetoa mapendekezo mazuri sana mimi nimeisoma na ipo na inafanyiwa kazi.

Kwa hivyo, asuburi kwenye bajeti ya mwakani hajui niuliza swali hili yatakuwa yameshamalizika kabisa suala hili hatoniuliza tena.

Mhe. Mbarouk Wadi Musssa: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri mimi sijaridhika na hayo majibu. Maana yake tukiangalia Mhe. Mwenyekiti, mwaka jana alisema kuwa ripoti imeshakuwa tayari na mda mchache sana yaani lile tatizo litakuwa lishatatuka.

Lakini inaonekana na mwaka huu tupokea tena maekezo yale yale ya mwaka jana. Na hili Mhe. Mwenyekiti, hili tatizo liko pande mbili kuna upande mmoja wa Idara yenyewe ya ujenzi ya kukasa mapato kwa sababu nyumba zile hazichukuwi kodi hawalipi wale watu. Lakini ni nyumba zake ile idara.

Lakini upande wa pili ni wale watu wanaokaa pale hawajajiua hatima yao ni nini. Maana yake wamekuwa kama wananinginia. Sasa mimi nilikua naona ni jambo la singi sana kupatiwa ufumbuzi na ndio maana kukanduwa ile tume ile kamati. Mimi nilitegemea kamati ile itakapotoa ripoti yake inatakuwa ni *final* kwamba imeshatoa na uamuzi ni huo. Lakini cha kusikitisha ndio kwanza sasa inakwenda kujadiliwa kwa matibu wakuu, sijui itakwenda kujadiliwa wapi tena italetwa Barazani tuijadili au vipi baadae tupitishe kama ni Mswada au Sheria au vipi sina uhakika. Lakini Mhe. Waziri hebu atwambie hasa ni muda gani sasa tatizo hili litakuwa limetatuka, maana asitwambie mwakani kwamba bajeti ya mwakani hatutomuuliza tena hatumuulizi kwa sababu ya bajeti tu. Tunamuuliza kwa manufaa ya wananchi pale pana kodi ya Serikali haikusanywi lakini kuna wananchi wanaishi katika zile nyumba hawahajua hatima yake ni nini. Hebu Mhe. Waziri atwambie hasa ni lini litakuwa tayari tatizo hili litakuwa limetatuka.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, hili suale la lini zuri sana na nalipenda kwa sababu tunatakiwa tutekeleze. Kwa hivyo, namwambia ndani ya miezi mitatu suala hili lishatekelezwa.

Mhe. Mbarouk Wadi Musssa: Mhe. Mwenyekiti, waziri amekiahidi chombo hiki cha wananchi ndani ya miezi mitatu litakuwa limetatuka. Tutakuja kuulizina tena humu tuendelee.

Kifungu 0501 - Idara ya Ujenzi 584,550,000/=
Kifungu 0701 -

Mhe. Jaku HashimAyoub: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nimpongeze Mhe. Waziri kwa itikafu yake aliyokaa kwa jinsi huu mteremko unavyomteremkia neema hii, bajeti hii inawachangiaji wengi lakini anakula papai kwa kijiko au sijui Mhe. Haji Omar Kheir amemuazima watu wake watatu wale aliokuja nao katika bajeti yake.

Mchango wangu Mhe. Mwenyekiti, toka kuingia ndani ya Baraza lako hili nilikuwa na kilio cha muda mrefu kutoka kwenye michango hadi kwenye masuala na majibu. Leo asubuhi nilikwenda kutafuta *hansard* hizi mapema Mhe. Mwenyekiti, kuhusu barabara ya Forodhani kufungwa. Kwa masikitiko makubwa sana sisi tumetumwa na wananchi barabara ile hakuna sababu ya msingi mpaka leo kufungwa na kinachotia uchungu wageni wanaitumia barabara ile na kupita magari makubwa makubwa ya mizigo.

Mimi sitaki kupoteza muda Mhe. Waziri mimi namjua mfatiliaji na akiifunga barabara ile anahangaika yeye mwenyewe kwenda Malindi kutafuta samaki. Barabra imekuwa gumzo kubwa Mhe. Mwenyekiti, hapa nikiisoma hii *hansard* itakuwa vichekekesho Mawaziri wawili kugonga kauli Dr Mwinyi Haji aliahidi barabara hii kufungua kutoka eneo la msikiti wa Ijumaa na nyumba ya Forodhani akaifungua lakini baadae ikaja ikafungwa, ikawa mawaziri hawa wanagongana wananchi tutawatatulia vipi katika kauli hizi. Naomba maelezo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub suala lake kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, tunaendesha nchi kwa pamoja hatuendeshi nchi mtu mmoja mmoja. Kutokana na matatizo yanayojitokeza Mji Mkongwe nisema hapa kwamba imeundwa kamati ya pamoja kushughulikia masuala haya ili tuone kwamba msongamano wa magari katika mji Mkongwe haupo. Kamati imetoa mapendekezo yake na hivi sasa matatizo hayo yanashughulikiwa sasa si suala la mji Mkongwe pekeyake ni suala la pamoja Mji Mkongwe, Polisi, Bandari na wengineo.

Mhe. Mwenyekiti, kama unaondoka hapa ofisini kwako saa 7 kabla ya kuja boti ingia mahakamani uelekee kule Mji Mkongwe nadhani utafika Malindi baada ya saa moja au saa moja na nusu, huo ni upande mmoja ukiondokaa hapa saa saba meli kule inashusha

watu basi utafika kule baada ya saa moja au saa moja na nusu na utasimama sana kutokana na msongamano.

Mambo kama haya yakitokea Mhe. Mwenyekiti, yanahitaji kufanyiwa kazi kutokana na msongamano wa magari, ndio tukaunda hii kamati ifanye kazi. Lakini nisema Serikali siku hizi tumeanzisha utaratibu wa kuziondoa ofisi zetu katika mji Mkongwe ili kupunguza ule msongamano wa magari kule, hii itasaidia kupunguza msongamano, hii *world heritage* itakuwa haina maana ikiwa watalii wanakuja kule akawa wanachukuwa muda mrefu maana inakuwa kila mara inabidi aruke gari na wenzetu wanaogopa wale. Lazima tupunguze kule gari mji Mkongwe wazungu wengine wanaogopa sana na ndio maana wanapoondoka huko wanajiwekea bima wale kwa sababu wanaogopa sana mambo haya ya kuja kukongwa na gari lazima tulishughulikie hili suala kusema ukweli.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub hili suala tunamuomba ashirikiane na sisi na kamati na sisi watu tunayaona hayo matatizo na lazima tuyashughulikie huwezi kuliona tatizo na ikawa unatikisa kichwa tu ufanye kazi. Kwa hiyo, tumeona kwamba tuzuie hiyo kidogo tuzuie magari katika eneo hilo la Mji Mkongwe. Mhe. Ismail Jussa akenda kwake isiwe tena anakimbia gari tu kila mara aende zake kwake kwa asulama na amani.

Mhe. Jaku HashimAyoub: Mhe. Mwenyekiti, msongamao ule kama unasababishwa basi unasababishwa na Bandari pale kipande kidogo tu sana, kama Serikali itakuwa makini lile eneo linadhibitika njia zipo. Hili suala la tangu mwaka 2011 hadi leo na kauli za mawaziri zimeshatoka humu, mimi siwezi kusema muongo na huu mwezi wa Ramadhani na kiongozi ni kioo cha nchi hii. Ikiwa leo wananchi wanatusikiliza tunatoa kauli hii kesho tunageuka tunafanya nini. Mimi nakuomba sana mzee wangu hili suala najua si mkaidi kwa vile ulikuwa mwalimu mimi nafikiri tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Kuna maelezo zaidi, kuna rai ni kumshirikisha Mhe. Jaku Hashim Ayoub vile vile akatoa maoni yake maana anasema njia zipo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, wazo lako zuri la kumshirikisha Mhe. Jaku Hashim Ayoub katika hizi kamati maana yake nchi zinaongozwa kwa pamoja haongozi mtu mmoja mmoja itakuwa vizuri tutamshirikisha katika hizi kamati yeye akapata upendeleo maalum akawemo kwenye kamati.

Lakini namwambia tu kama magari Mji Mkongwe yatakuwa mengi basi *world heritage* itapote na itakuwa sio tena *world heritage*. Maana Mji Mkomgwe tunategemea kwamba watu wanakuja kujifunza maana watu wanakuja kufanya *research* hapa wanatoka katika vyuo mbali mbali duniani wanakuja kufanya *research* zao.

Sasa ukisema kuna masuala ya msongamo wa magari na nini na ende Cuba akaone wanao mji Mkongwe kule, kwenye mji Mkongwe haipiti gari kabisa wamezuia kabisa. Gari zinapita katika maeno ya pembeni kabisa sisi tunaziruhusu zipite. Lakini kwa utaratibu maalum iwe *one way* tunakwenda huku tu basi ndio tunavyofanya hivyo. Kwa

hivyo, Mhe. Jaku Hashim tukifanya anavyotaka yeye tutapoteza ile hadhi ya ule urithi wa kimataifa tutapoteza kabisa.

Mhe. Jaku HashimAyoub: Mhe. Mwenyekiti, tuangalie umuhimu wa wananchi na umuhimu wa Mji Mkongwe. Tuangalie kipi muhimu mji Mkomgwe au wananchi wa nchi hii kimetawala kitu gani. Jengine ningelimuomba kama hataki gari basi japo vespa. Vespa hazina foleni angeruhusu kupita na katika kushirikisha amshirikishe Mheshimiwa Mwakilishi wa mji Mkongwe sio mimi peke yangu yeye ndie mwenye jimbo.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi nadhani yote mawili ni muhimu, wananchi ni muhimu sana na urithi wa Mji Mkongwe ni muhimu sana. Na nadhani yakifanyiwa kazi kwa pamoja ndio itapatikana faida zote mbili kwa ajili ya wananchi na pamoja na urithi wenyewe. Mhe. Jaku Hashim Ayoub kuwa karibu na Mhe. Waziri na Mheshimiwa Mwakilishi wa Jimbo mimi nadhani usiwe mbali ili mtafute rai jambo hili liondoke, tuendelee.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia kwenye mamlaka ya Mjimkongwe nilisema kwamba kuna malalamiko makubwa kwa wafanyabishara Forodhani wao wanalipa kodi kubwa na huduma hawazipati, nimesilikiliza vizuri Mhe. Waziri alipokuwa akijumuisha na alisema kule maji yamekatwa kwa sababu ya deni kubwa liliopo. Je, mimi nataka niulizie tu deni hili linasababishwa na wafanyabishara au ni Serikali kupitia mamlaka ya mji Mkomgwe.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, sikumpata vizuri lakini nasema tu kwamba huduma ya maji katika bustani ya Forodhani yaani maji yapo. Tatizo ni deni kubwa pale, leo ikiwa nje tunawaambia watu kama hukulipa tunakukatia maji, sasa pale leo panadaiwa mamilioni ya pesa. Lakini tukubaliane angalau tupate ile *schedule* ya kulipa. Tukuweka *schedule* basi tutajua kwamba wanatulipa kidogo kidogo lakini maji Forodhani yapo. Hilo ndilo ninalomjibu mimi. Kwa hivyo, kama ni huduma hiyo tu ya maji basi *alhamdulilah* pale maji yapo.

Lakini sasa nayo Idara ya Maji *ZAWA* ilipwe maji yameshakwenda sana kwa sababu. Kama kuna huduma nyengine huyo nitaichukuwa na kuipeleka kule kwenye Baraza linalohusika na ile bustani ya Forodhani Mheshimiwa akiniorodheshea mimi nitalifanyia kazi na nitawapelekea watu wa Baraza na litafanyiwa maamuzi hilo. Lakini kwa maji pale yapo isipokuwa hayatoki kwa sababu yanadaiwa.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, nakushuru sana. Mimi nilimuuliza Mhe. Waziri nilitaka kujua wanaodaiwa ni wafanyabiashara au Serikali, naomba anipe maelezo ya ziada. Hili linasababishwa na hawa wafanyabishara wanadaiwa au ni sehemu nyengine.

Kwa sababu mimi shahidi nilikwenda pale kuna vyoo pale hata ndani ya vyoo hamna maji ni tatizo, tulishuhudia sisi wenyewe na Waheshimiwa wenzangu pia walikuwepo, sasa nilikuwa nataka kujua wanadaiwa ni hawa wafanyabiashara au ni sekta nyengine.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, tunamdai yule mwenye bustani ile ya Forodhani ambaye huyu ndio tunaemdai. Sasa wafanyabiashara ni vizuri kulalamika kwa sababu haya maji hawayapati, lakini ni vizuri na kile chombo pia kinachohusika. Lakini sio lazima walipe zote tukubaliane *schedule* tu mwezi huu utalipa hivi na mwezi huu utalipa basi tutakwenda vizuri. Lakini unadaiwa mamilioni ya pesa yanadaiwa pale.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri aniambie hawa wanaodaiwa ni taasisi gani mpaka wapewe adhabu hawa wananchi ambao walipa kodi. Akinijibu hapo basi tuendelee.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, maji pale yanadiwa tangu pale ujenzi wa ile bustani yenyewe walitumiwa mji pale wakahuisha bustani na kila kitu. Kwa hivyo, waliojenga pia wanadaiwa.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, naona Mhe. Waziri hakuniweka wazi labda kuna kitu kinafichika pale. Lakini mimi sioni sababu ya kuwaadhibu wananchi ambao wanalipa kodi sahihi, wanalipa kodi lakini huduma hawapati na ile hifadhi ya mji Mkongwe ili uwe mzuri ni pamoja na kupatikana kwa maji. Kwa hivyo, Mhe. Waziri atuweke wazi hapa ili tupate kuendelea na shughuli yetu hii. ni nani anadaiwa.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, Mheshimiwa keshasaidia sana katika suala lake hili kuwa wanaodaiwa wameshasikia na keshawatetea wanaodai pale ambao wanaofanya biashara pale katika suala lake hili si tuko *live* sasa hivi kwenye *TV* watakutana pale Bodi wafanye maamuzi juu ya suala hili wameshasikia maana maji hayapatikani pale wanadaiwa basi.

Mhe. Mwenyekiti: Nafikiri Mheshimiwa mjumbe anachokihitaji huyu anaedaiwa ni nani. (*Makofi*).

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, anaedaiwa ni muendeshaji wa ile bustani na aliejenga ile bustani. Mwenyewe keshasikia huko.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nadhani bustani ya mji Mkongwe inamilikiwa na Baraza la Manispaa au Mamlaka yenyewe ya Mji Mkongwe. Sasa hao wote wenye taasisi wamo humu ndani. Kwa hivyo, watuambie kama ni Mji Mkongwe ndio yeye mwenyewe, kama ni manispaa waziri yupo. Maana yake angalau tungejua nani anayemiliki.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu unajua hilo tatizo alilolizungumza mheshimiwa kwa pahala kama pale mpaka wageni wanakuja chooni hakuna maji ni aibu, hebu tuambiwe nani muhusika. Mimi nafikiri labda kama mawaziri hawajui Mji Mkongwe wa nani basi mimi ni wangu, bustani yangu ile. *(Makofi/Vicheko).*

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, kama ni manispaa umeshasikia mwenyewe kasikia, kama ni Mji Mkongwe keshasikia mwenyewe tushasikia kama ndio sisi. Lakini tukilipa yale maji ndio watapata pale maji, lakini tupunguze deni. Mhe. Mwenyekiti, tena mimi wala sitokulipa zote, tutengeneze *instalment* tu basi. Kama alivyosema Mhe. Hamza Hassan kama ni mimi au kama ni manispaa au kama ni nani tutengeneze *instalment* ya kulipana. Mimi natetea ZAWA kwa sababu ZAWA hii waheshimiwa ndio wanaibana kwa ajili ya maji na wanakuwa hawana uwezo wakati mwengine na wanadai pesa zao.

Mhe. Mwenyekiti, sisi hapa ZECO wanatengeneza utaratibu sasa hivi wa kupa deni la TANESCO. Tulipeni, siku hizi bwereree hakuna. Kwenye ofisi zote sasa hivi tunaziwekea mita za TUKUZA. Mambo yale ya kuwa tutumie mahala kwa bwereree tuyawache sasa na tubadilike sasa.

UTARATIBU

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, kanuni inatuelekeza kwamba waziri au mjumbe yeyote aliyoeuliza swali ambalo ana madaraka nalo, atakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kwa ukamilifu kwa usahihi na kwa ufupi, isipokuwa kwamba swali alililoulizwa waziri mmoja anaweza kujibiwa na waziri mwengine au na Mwanasheria Mkuu.

Kwa hivyo, swali la Mhe. Mjumbe pale alitaka kujua kwamba anayedaiwa, swali la msingi linasema anayedaiwa mamlaka ipi inayodaiwa, lakini waziri anaonekana anashindwa kuitaja ile mamlaka. Sasa kama kuna waziri mwengine au Mwanasheria Mkuu kwa mujibu wa kanuni yetu wamsaidie Mhe. Waziri ili aweze kulijibu mara moja tupate kuendelea, kwa sababu tunabakia hapa hapa Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi).*

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, bustani ya Forodhani inaendeshwa na chombo hicho alichokisema Mhe. Waziri, kuna bodi pale ndio inayosimamia uendeshaji wa bustani ile tokea ilipojengwa. Mimi nimefurahi sana Mhe. Waziri kwamba umezungumza kuwa wanadaiwa hizo *bill* za maji tokea wakati wa ujenzi wake. Kwenye hicho chombo tumo watu wa manispaa, tumo watu wa Mji Mkongwe, tumo na watu wa *private sector* wengine.
Kwa hivyo, mimi nafikiri wazo la Mhe. Waziri tumelichukua, yeye anatete ZAWA sasa. Basi tutakaa pamoja hicho chombo ambacho tumo sote na yeye pamoja tuweze kulipitia hili deni la ZAWA tulipe ili maji yaende pale na bustani iimarike. Mhe. Mwenyekiti, tunachukua jukumu hilo.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hivyo, jibu la anayedaiwa ni bodi inayoendesha bustani ile ambayo ndani yake wamo manispaa, Mji Mkongwe pamoja na *private sector*. Ndivyo.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru tena kwa mara nyengine na kwa sababu huu mjadala umekuwa mrefu. Mhe. Waziri kasema hiki chombo lakini hakutaja ni chombo gani.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kwa sababu wananchi wa pale wanalipa kodi na ni kodi kubwa wasiadhibiwe kwa taasisi nyengine, wanalipa kodi wapate huduma ili ziwaendeshee shughuli zao vizuri. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri tusilifumbie macho tulishughulikie. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi nimebakia hapo hao katika Mamlaka ya Uhifadhi wa Mji Mkongwe. Mimi katika mchango wangu niliangalia katika kitabu cha Mhe. Waziri kwenye ukurasa wa 33 kwenye kifungu cha 90, kuelimisha jamii juu ya uendelezaji wa mradi wa Mambo Msiige. Sasa mimi nilikuwa nataka kujua tu mradi ule ni wa serikali, wa mtu binafsi au wa kampuni. Maana yake ikiwa wizara ndio inachukuwa bidii sasa ya kuelimisha jamii kwa mradi ambao sio wa kwao, nahisi tutakuwa tunatumia fedha za wananchi kwa maslahi ya upande mwengine.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka kujua kama ule mradi ni wa serikali na kama sio wa serikali basi je, wizara itaielimisha vipi jamii kwa kutumia fedha za walipa kodi.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, Mradi wa Mambo Msiige, ujenzi wa hoteli ile pale ni sawa sawa na mradi uliokuwa umeshakuwa tayari unafanyakazi kama Serena ambao ni *private company,* ni sawa sawa na mradi uliopo kule Kiwengwa kama *Blue Bay* na mingineyo. Lakini siku zote wizara inakuwa na malengo yake ambayo haitaki yapotee. Katika hoteli ile sisi tunatakiwa tulinde, kusimamia *heritage* ni kazi ya Mji Mkongwe ambayo ndio serikali ili iende kwa mujibu wa sheria.

Kwa hivyo, suala hili inaweza kuwa Mji Mkongwe wanalifahamu peke yao, lakini wananchi wa eno lile hawalifahamu, ambapo katika zile sera zetu wanaitwa wao ni wa, hili neno asilolipenda Mhe. Haroun Suleiman, wanaitwa wadau, yaani wahusika wa ule mji. Kuna vikao tunavifanya na wahusika wa ule mji na kuzungumza nao juu ya kuwaelimisha kwa nini tunafanya vile, ni kazi yetu kama serikali kuona kwamba ile *heritage* inaendelea kulindwa katika maeneo yale na una mipaka yake bila shaka.

Kwa hivyo, sisi tunachokifanya sio tunamtetea yule mwekezaji pale, hapana. Sisi tunalinda huu Mji Mkongwe usiwe mji wa majumba mabovu na tunakwenda tukisimamia pale ili kuona kwamba zile taratibu zitakazokuja kufanywa baadae zifanywe kwa mujibu wa ile ramani iliopo. Sio sisi tu, hata *UNESCO* wenyewe, nadhani tulikuwa tuna makubaliano walete mtu hapa. Sijui kama hajafika huyo mtu, kwa sababu ilikuwa tayari keshaagizwa aje kutizama ule ujenzi namna unavyoendelea pale. Tunalinda wale *heritage* ili ule mji uendelee kuwa na ari.

Mhe. Mwenyekiti, sasa sisi kama serikali ambao tunahusika kulinda tukiacha tu hivi hivi, mtu akenda pale akaporomoa jumba la viyoo ghorofa 18, sio pale. Kama mtu anataka kujenga jumba la ghorofa 18 huku nje tunayo maeneo aje achukuwe atajenga ghorofa 30, 40 au 50 hakuna tatizo lolote huku nje, lakini kule tuwe na mpaka wetu wa ile *heritage* ibakie na ule mji ubakie katika sifa yake katika *world heritage*. Vinginevyo, itabidi labda tuondoke kwenye *heritage*. Hatutumii pesa za wananchi, tunaondoka na tutawaachia hilo

suala bila ya shaka lolote. Kwa hivyo, Mhe. Mjumbe namwambia kwamba sisi tunafanya hivyo kwa sababu ni jukumu letu kuona kwamba ile *heritage* inakuwepo pale.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na maelezo ambayo ameyatoa Mhe. Waziri, mimi bado sijamfahamu Mhe. Waziri na sijamuelewa kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, lile eneo la Mambo Msiige hata kama utakumbuka hapa tulipounda kamati teule ni moja katika eneo ambalo lilikwenda kuchunguzwa. Lakini maelezo ambayo yalitolewa hapa na kamati teule ni kwamba eneo lile libakie kwenye mikono ya wananchi kwa kupitia serikali, maana yake libakie serikalini lisitolewe.

Mhe. Mwenyekiti, hayo ndio yalikuwa maamuzi ya chombo hiki cha wananchi. Serikali ilileta ripoti yake hapa ya utekelezaji wa ile na ilitupiliwa mbali juu ya suala lile, lakini bado inaonekana serikali haikuweza kusikiliza yale ambayo wananchi walikuwa wanayataka, matokeo yake wamelazimisha kile kitu kwamba kiendelee. Sasa wananchi wanaendelea kutozwa kodi kwa ajili ya kwenda kutolewa elimu tena juu ya jambo lile. Mimi naona kama serikali inafanya kinyume nyume, kwa sababu sasa tunaanza kutumia fedha kwa manufaa ya mtu.

Mhe. Mwenyekiti, ukisikiliza maelezo ya Mhe. Waziri maana yake sasa tukae tumsimamie maana yake asije akajenga. Hiyo ni mikataba ambayo mngekuwa mmefanya na yeye kama ni mwekezaji ndio angepaswa asimamie hiyo ili kuona kwamba ule uhifadhi unabakia, kwa sababu mnampa masharti, lakini ikiwa sasa serikali itaanza kutumia fedha za kwenda kutoa elimu kwa sababu kuna mwekezaji anaekeza pale ili watu wamuelewe, mimi nahisi hivi tunatumia fedha kinyume na utaratibu. Mimi nazuia fungu hili Mhe. Mwenyekiti, mpaka nipate maelezo mazuri ya serikali katika hili.

Mhe. Mwenyekiti: Uzuiaji nilielekeza kwamba huwezi ukazuia upate maelezo. Kwa hivyo, tupate maelezo zaidi kutoka kwa Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, ujenzi unaoendelea pale, kama alivyosema Mhe. Waziri ni ujenzi wa hoteli ya kimataifa ya nyota tano. Hilo analosema Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Mtando *interest* ya wananchi kwa sehemu ya bustani ipo kama ilivyopangwa na hilo jukumu kapewa huyo mwenye hoteli, sasa hivi anaona pamezungushiwa tu kwa sababu ya bati, lakini imemegwa sehemu ile kwa hivyo bustani itakuwepo kama ilivyopangwa, isipokuwa imepunguzwa tu. Hayo makubaliano yameshafikiwa, michoro imeshachorwa na ujenzi unaendelea vizuri kabisa. Kwa hivyo, hiyo sehemu ya hoteli ipo na sehemu ya bustani ile itaendelezwa na itakaribia Forodhani itakuwepo hilo halina utata, ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Nafikiri maelezo yanatosha, wamejitahidi mawaziri wangu wawili. Nadhani tuendelee.

Kifungu 0701	Hifadhi ya Mji Mkongwe	299,296,000,

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa tena nafasi hii ili nikapata maelezo ya ziada kutokana na mchango wangu nilipokuwa nachangia, katika suala zima ambalo hata ujumbe wa Baraza la Wawakilishi ukiongozwa na wewe mwenyewe Mhe. Spika, ulipata nafasi ya kwenda Uholanzi kutokana na mualiko ambao uliletwa.

Mhe. Mwenyekiti, nilisema kwamba katika kitabu cha Mhe. Waziri hakueleza sana au hakutoa ufafanuzi katika suala la maendeleo ya nishati, gesi na mafuta. Lakini namshukuru kutokana na maelezo yake, maana alisema kwamba kitabu ni kikubwa kama angeeleza kila kitu basi muda usingetosha, lakini kutokana na maelezo yake anasema kwamba hili suala kwa sasa hivi linakwenda vizuri, lakini liko nje ya mikono yake na linashughulikiwa na Mwanasheria Mkuu. Sasa nadhani Mhe. Mwanasheria Mkuu angetusaidia basi maelezo, kwa sababu unajua mambo haya ni wazi watu wanatakiwa wayajuwe, sio siri. Kwa hivyo, mimi nadhani angalu tungepata ufafanuzi kuhusu hili suala liko katika hatua gani, ahsante.

Mhe. Mwanasheria: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mhe. Hamza Hassan Juma pamoja na waheshimiwa wajumbe kwa hamu yao ya kufuatilia suala hili, bila shaka ni kwa niaba ya wananchi na kwa maslahi ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, pili kama alivyosema Mhe. Waziri kwamba suala la mchakato wa kuweka utaratibu wa Zanzibar kushughulikia suala la nishati ya gesi na mafuta limekabidhiwa kwa kamati maalum ambayo inaongozwa na Wanasheria Wakuu. Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba kamati hiyo inaendelea kufanyakazi zake, hapa katikati ilikwama kidogo, lakini ilikwama kwa sababu ya sisi wenyewe kama Zanzibar kukwama kule kulitusaidia kidogo. Kwa sababu kulikuwa na suala la tutakapopitisha hizo sheria na tutakapoamua kugawana, tutakapoamua kutenganisha mamlaka ya usimamizi Zanzibar eneo lake litaishia wapi na Tanzania Bara eneo lake litaishia pahala gani.

Mhe. Mwenyekiti, nakumbuka katika bajeti sijui kama ni ya Ofisi ya Makamu wa Pili, lilikuja suala la Kisiwa cha Fungumbaraka, eneo lile lilikuwa lina utatanishi kuhusiana na kwamba je, kisheria hasa liko upande gani na lile eneo kwa wanaofuatilia linaingia kitalu nambari 8, nadhani na sehemu ya kitalu nambari 7 vile vile. Kwa hivyo, ilikuwa ni lazima tulipatie ufumbuzi wa kisheria wa uhakika. Kusema kweli tuliifanya kazi hiyo na sasa tuna uhakika na kwa hiyo itapunguza au itaongezea Zanzibar kwa uhakika kilomita 60 zaidi ndani ya bahari, kwa hivyo hata pale tutakapo kubaliana kwamba eneo la Zanzibar ni hili, sasa tutakuwa na uhakika wa kwamba ni vitalu vipi ambavyo vimeshagaiwa vitakuja upande wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, pia kuna suala ambalo linahitaji utaalamu vile vile, vitalu vilivyogaiwa sasa hivi vya upande wa ndani ya nchi kavu, yaani *off shore block* ambazo kwa sasa hivi ziko mbili, ukiangalia utakuta kwamba zimeingia upande wa Zanzibar na

pia upande wa Tanzania Bara. Kwa hivyo, nilazima pia yapatikane maelekezo na ushauri wa kitaalamu wa namna gani *block* zile kama tutatenganisha ya Zanzibar itaishia wapi ya *off shore* na za Tanzania Bara zitaishia pahala gani.

Kwa hivyo, baada ya kuezeshwa naomba niwahakikishie kwamba tunachoandaa sasa hivi ni kupata wataalamu ambao wataweza kutusaidia kuweka hayo maeneo ambayo lipi litakuwa ni eneo la Zanzibar na lipi litakuwa ni la Tanzania Bara na tuna ahadi ya kupata wataalamu kutoka katika nchi mbili tofauti wa kutusaidia katika kazi hii.

Kwa hivyo, kazi hii inaendelea, lakini sehemu tuliopo sasa hivi ni muhimu tuwe na uhakika na tutakapokuwa na uhakika tutaweza kuondoa hili tatizo ambalo mchakato wote mzima umekusudia kuliondoa, nalo ni kujua kila mtu eneo lake ni lipi tutakapoweka taasisi, tutakapoweka sheria tutajua kwamba litaishia katika eneo gani. Lakini wakati huo huo tunategemea katika kipindi cha wiki hizi hizi mbili kukutana, ili kukubaliana kwamba ule utaratibu wa kuanzisha ile taasisi ya Zanzibar na pia kuanzisha sheria ya Zanzibar na hata sera ya Zanzibar, kwamba ni vyema tuwe na makubaliano ya maandishi ambayo kimsingi tumekubaliana, kwamba itatoka ili tuweze katika kipindi kifupi kijacho tuweze kukamilisha hizi hatua zilizobakia. Nadhani yatasaidia Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwanza tunaishukuru sana Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa jitihada zao za kusimamia mambo mbali mbali ambayo yanayohusu maslahi na rasilimali za Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nina ushauri na ushauri wangu huu waswahili wanasema kwamba 'mtu akitafunwa na nyoka basi akiona unyasi anashtuka'. Mhe. Mwenyekiti, sisi mpaka sasa hivi nadhani bado hatujaandaa sera ambayo inahusiana na masuala ya nishati, au kama itapataikana ya mafuta au gesi. Kwa sababu sasa hivi kwa kuwa Zanzibar tayari imesharuhusiwa na jambo lililobakia ni mchakato tu wa kisheria kuangalia hiyo mipaka ili yasije yakatutokezea kama yaliyotokezea Mtwara. Watu baada yakugundua kwamba ndani ya eneo lao ndio ile rasilimali ilipo, hatuoni kwamba sasa hivi ipo haja ya kuandaa mapema ile sera ambayo itakayoainisha nishati hizi sehemu yoyote zitakapopatikana basi ni namna gani wale wananchi waliokuwa karibu na eneo lile, lakini vile vile ile nishati itakuwa ni ya kitaifa. Kwa sababu tumeona ya wenzetu wa Mtwara yaliyotokezea ili na kwa upande wa Zanzibar yasije yakatokea.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, suala hili hapa walipofikia, maana yake wameganda kidogo, walipofikia ni pahala ambapo kuna eneo inaonesha limegandana au tuko pamoja. Kwa sababu kama itafika pahala kwenye mazungumzo kila mmoja atavutia kwake, hatutoacha *option* ya kwamba hizo *block* zilizokuwepo baina ya Zanzibar na wenzetu Tanzania Bara zikaendeshwa kwa pamoja. Kwa sababu tukisema kwamba tusubiri watu wang'ang'anuane mpaka kila mmoja akubali kwamba hili langu na hili lako, tunaweza tukachukua muda mrefu na huu mchakato sasa hivi umeshakuwa unatuumiza vichwa.

Je, Mhe. Mwanasheria Mkuu haoni kwamba ikijakufika pahala wakiwa wamevutana sana katika haya maeneo ambayo yako pande zote mbili, hatuoni kwamba hili likabakia

likaendeshwa kwa pamoja katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ili yale yaliyobakia yaendelee kila mmoja afanye utafiti na yake, ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, wacha nitowe ushauri. Mhe. Mwanasheria Mkuu usijibu hapa, isipokuwa chukua ulifanyie kazi. Tunaendelea.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, mimi katika fungu hili la 0801 Mhe. Mwenyekiti, mimi kidogo nataka maelezo kwenye kifungu 220700 kuhusu matengenezo ya ofisi na nyumba, kwenye fungu 220701 matengenezo madogo ya ofisi pana shilingi milioni 6 zimetengwa na fungu 220702 matengenezo makubwa ya majengo yaani ya ofisi vile vile shilingi milioni 34, nilikuwa nataka maelezo kwa sababu naona jengo ni hilo hilo moja lakini mafungu yametengwa mawili. Nilikuwa nataka maelezo katika hapa.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi akaelewa kwamba Idara ya Nishati ni mpya na haina ofisi ya uhakika iliyokubwa, wako katika mabanda ya maonesho pale Mwanakwerekwe. Kwa hivyo, yale mabanda ya maonesho wana matengenezo madogo madogo wanataka wafanye pale. Lakini pia kuna banda moja pale ambalo wanakusudia kulifanyia matengenezo makubwa ndio maana wakatenga kote kote, matengenezo madogo na matengenezo makubwa.

Mhe. Mwenyekiti, hii karatasi inaendana na maneno yangu ninayosema, kuna banda pale la Shirika la Umeme ambalo wanachukua wao, hili watalifanyia matengenezo makubwa kwa kutanua ile ofisi yao.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na maelezo ambayo ameyatoa Mhe. Waziri, mimi hoja yangu ni kwamba ukiangalia hiki kitabu kinaonesha namna ya mtiririko wa wa fedha zilivyokuwa zinaingizwa katika kipindi cha miaka mitatu, mote humo muna matengenezo madogo na matengenezo makubwa, lakini ukiyaangalia yale matengenezo yalikuwa kama yanalingana.

Kwa mfano mwaka 2010/2011 walikuwa wana shilingi milioni 1,375,000 katika matengenezo madogo na shilingi milioni 3 katika matengenezo makubwa. Mwaka 2011/2012 kulikuwa kuna shilingi milioni 1,500,000 matengenezo madogo na matengenezo makubwa kuna shilingi milioni 3,100,000. Mwaka 2012/2013 kuna matengenezo madogo shilingi milioni 3 na matengenezo makubwa shilingi milioni 3. Sasa maelezo ya Mhe. Waziri ni kwamba mwaka huu wanategemea kuchukua jengo jengine kwa ajili ya matengenezo makubwa. Sasa hizi nyengine zilikuwa zinafanyia kazi gani, ndio maana nikaona kwamba haya mafungu yanaonekana ni mafungu ya kupachikwa pachikwa. Kama wanakwenda kufanya matengenezo makubwa ya jengo moja, basi lilikuwa linatosha fungu hili la shilingi milioni 34, kwa ajili ya matengenezo makubwa wala halina tatizo. Lakini hili fungu dogo la matengenezo madogo ya kazi gani wakati mnajua mnahama hapa mnahamia hapa kwa ajili ya kwenda kufanya matengenezo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, mazungumzo aliyozungumza Mhe. Mbarouk Wadi Mussa kwamba hizi pesa zinapachikwa pachikwa, sio sahihi. Namuambia kwamba hii ofisi ni mpya na hii ofisi kwanza ilianza na mtu mmoja tu, ilianza pale ofisini kwetu, wakati huo walikuwa wanatengeneza hii ofisi wanayoitumia sasa hivi Mwanakwerekwe, kidogo kidogo wanaitengeneza. Sasa hivi wameshafika Mwanakwerekwe. Sasa humu walimo wanaona angalau sasa hivi wame *settle* ndio wanafanyia matengenezo madogo kuiboresha zaidi. Lakini halafu wanatoka humo sasa hivi wanatanua, wanachukua hili banda ambalolilikuwa la Shirika la Umeme kwa kulifanyia matengenezo makubwa ile ofisi imefika pale, mpaka hapo tutakapopata uwezo na sisi, Wizara ya Fedha, Uchumina Mipango ya Maendeleo itakaporuhusu kujenga ofisi yetu mahala ambayo ikai-*accommodate* mambo yote tunayohitaji. Kwa hivyo, hazipachikwi zinafanyiwa kazi.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, jana wakati nachangia nilizungumzia jinsi Shirika la Umeme wakati linapeleka wanawake Makaani Pwareni wamekata vipando vingi sana vya wakaazi wa Vitongoji, Umangani, Kibokoni, Uwandani, Changuu nakadhalika. Kwa bahati mbaya sana hawakuwashirikisha wakulima katika kufanya makisio ya mazao yao. Sasa ingawa Mhe. Waziri katika kujibu alisema kwamba kazi ile ni ya watu wa mawasiliano. Lakini sisi wananchi tunajua kwamba wanaoshughulika na mambo ya umeme ni watu wa Shirika la Umeme ZECO. Sasa anapotuambia kama ni Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano sisi hatutambui, ninachomuomba Mhe. Waziri anithibitishie hapa kwamba keshafanya mazungumzo na huyo waziri wake wa mawasiliano ya kuwalipa wale watu wa Vitongoji na kama keshafanya ni lini watawalipa

Suala jengine nilizungumzia katika suala hili la ZECO kwamba TUKUZA kule Pemba vituo ni kidogo sana, nikamuomba afanye uwezekano wa kuweza kutuekea vituo katika maeneo ya mashamba kama vile kuweka pale Vitongoji, Umangani, Kibokoni na maeneo mengine ya Wawi, Uwandani na hata Ng'ambwa na wao wanahitaji hivi vituo kwa sababu kutoka Ng'ambwa mpaka kufika Chake Chake ni tabu sana, je ni lini wataweka vituo hivi ili kuondoa usumbufu kwa wateja wao katika suala la kununua TUKUZA.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli suala hili sio pahala pake hapa, ni suala letu. Katika mwezi wa Januari kulitokezea *break down* Kware ya Vitongoji, kwa hivyo mitambo yote miwili ilikuwa haiendi, mtambo wa kufanyia kokoto na mtambo wa kupikia lami kwa sababu ilikuwa zikiendeshwa na jenereta. Kwa hivyo, tulichukua hatua za dharura kupeleka umeme uliosababisha kupita katika maeneo ya watu.

Mhe. Mwenyekiti, ni tofauti na alivyosema Mhe. Mwakilishi, walishirikishwa kikamilifu kwa kupitia wizara ya kilimo ya kutathmini mazao na fedha zao zimeshaorodheshwa kila mmoja anajijua hasa ana kiasi gani. *Inshaallah* mara baada ya bajeti hii katika mwezi wa Agosti basi watalipwa fedha zao zote, ahsante.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, unajua kwa kawaida sisi walimu hatutakiwi tuseme sio au hapana, lakini sitaki niseme kwamba hakusema kweli. Mimi Mhe. Mwenyekiti, ni miongoni mwa muathirika nimekatiwa miti yangu, anajenga hoja Mhe. Waziri kwamba wana habari na ni kiasi gani wamefanyiwa makisio. Mimi nikiwa mmoja kati ya waliokuwa na mashamba makubwa katika eneo hilo, basi sina habari nitalipwa kiasi gani na wala sikushirikishwa katika suala zima hili.

Kwa hivyo, nadhani Mhe. Waziri ili afanye haki kabisa katika kufanya malipo, a-*review cost estimate*, kwa sababu kuna watu wamefanyiwa makisio hawapo, kwa hivyo kuendelea kwenda kuwalipa watu wakati mali iliyokatwa ni nyingi au kulipa fedha za ziada itakuwa si matumizi mazuri ya fedha za walipa kodi wanchi hii na wale ambao watapunjwa itakuwa ni kuwadhulum, ambapo leo ni waziri lakini kesho utakuwa ni kiumbe wa Mwenyezi Mungu ambaye utahojiwa huko tunakokwenda.

(a) Mhe. Spika, mimi nadhani tu-*review* ile *cost estimate* yake na lini ata-*review* ili nikupatie watu na wakija wataalamu wako, ili waweze kufanya hizo *cost estimate* tena. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nafikiri (b) bado halijajibiwa hilo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, ushauri ni kwamba mka-*review* hiyo *estimate*, kwa sababu kuna wengine walikuwa hawapo. Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, ushauri tunauchukua. Lakini napenda kumhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba kamati zilikuwa ni mbili moja ya kilimo pamoja na watu wa umme na ya pili ilikuwa ni ya wizara yetu ya Miundombinu na Mawasiliano, watu wa umeme pamoja na raia wake. Kwa hivyo, yeye kama hakuwemo na alikuwa na kipando basi tutatoka naye, ili twende tukaone hivyo vipando vyake kweli vimepitiwa katika eneo lile au laa. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, nafikiri tuendelee.

Kifungu 0801 Idara ya Nishati

UTARATIBU

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, nimejibiwa hili la (a) na naona tunaendelea na lile suala la TUKUZA kuombwa vile vituo katika maeneo ya Umangani, Uwandani, Gombani na Ng'ambwa bado.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, umefahamika, ingawa hoja hiyo ni ya nyongeza na imekuwa ya nne sasa na ninayo nasafi hata ya kuikataa, lakini tuache akusaidie Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, ushauri wa Mhe. Mjumbe si baya ni mzuri na tunauchukua. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea.

Kifungu 0801 Idara ya Nishati

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, hoja zimekwisha na samahani sana, tuendelee.

Kifungu 0801	Idara ya Nishati	235,868,000/=
Kifungu 0802	Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma	500,000,000/=
Kifungu 0901		

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana nataka kuweka *hansard* yangu vizuri nikubaliane na Mhe. Waziri kwamba amenijibu vizuri kuhusu habari ya haki kiwanja cha Pwani Mchangani na wenyewe wazee niseme wameridhika.

Lakini kuna kitu kimoja wameniomba sana wazee, kwamba awaahidi kuwa lini waende wakamuone baada ya matamshi yake mazuri na wazee wale wameridhika, lakini wameomba wamuone *physical* na yeye hawa wanyonge, basi lini na Mhe. Waziri anipe ahadi kuwa ajili ya kuona nao hawa wazee na halafu akeshakunijibu, basi mimi niweze kuseme kuwa nitajibu na mimi kumpa maeneno mazuri. Mhe. Mwenyekiti, naomba nipate jibu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, suala hili linakuja sawa na yale mengine ya kutoa siku lini wakati hapa tunaendelea na Baraza.

Kwa hivyo, ni vyema atuache kwanza tumalize suala la Baraza na halafu mimi na yeye kwa sababu Mhe. Mjumbe yuko karibu sana na mimi, basi tutapata siku gani wazee wale wafunge safari waje, maana hatujui hapa Barazani patatokea kitu gani, kwa sababu naweza kumwambia walete siku fulani na nikapata dharura za hapa Barazani na nimeshawatoa tangu shamba wazee wamepoteza nauli zao na wala si uzuri. Mhe. Mwenyekiti, nadhani ni vyema tusubiri tumalize Baraza na aweke kwenye *diary* yake kwamba anayo kazi hiyo na yeye kwa upande mmoja.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, awali nilisema kuwa ninaridhika na majibu yake Mhe. Waziri na nimshukuru Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu wake pamoja na wakurugenzi wote kwa kuwajali wanyonge na kutoa maneno matamu kama haya leo hii. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, pale mwanzo nilipochangia sikusema kama ninaunga mkono, isipokuwa nilinyamaza na nilipigwa na kigugumizi, lakini naomba niweke *hansard* yangu vizuri na naomba niseme ninaunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi tena kwa ajili ya kupata ufafanuzi wa ziada. Kwa hivyo, hapa kidogo naomba ikiwa Mhe. Mwanasheria Mkuu, Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Waziri mwenyewe wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati wanisikilize kwa vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, wakati Mhe. Waziri alipokuwa akinijibu hoja zangu nilipozungumzia suala la mwananchi mzalendo anaendelea kukangamizwa na kudhulumiwa na mwekezaji wa *Cristal Resort* kule Paje. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli Mhe. Waziri alieleza kuwa suala hili liko mahakamani, nataka niseme mbele ya Baraza lako hili tukufu kwamba suala ambalo liko mahakamani ni la kumzuia kujenga ukuta ile sehemu ambayo kama anaingia yeye katika eneo lake. Lakini eneo nililolizungumza mimi na hilo suala la geti sawa liko mahakamanai.

Sasa suala ninalolizungumza mimi Mhe. Mwenyekiti, huyu mwekezaji wa *Cristal Resort* amejenga vibanda au majengo ambayo anakodisha watalii wanalala na anakusanya fedha ndani ya eneo la mwananchi mwekezaji ambaye ni mzanzibari na eneo hili anaendelea kulitumia kwa muda mrefu na wala hili haliko mahakamani.

Kwa hivyo, sisi tulipokwenda Mhe. Mwenyekiti tulipokwenda na Kamati yako ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa wakati tulipopata malalamiko ya wananchi wa eneo lile yule mwekezaji alikiri na tulimuuliza je hizi nyumba vipi? Alisema hizi nyumba kweli ni zangu, lakini zimo ndani ya eneo la Mudrik.

Mhe. Mwenyekiti, kama huyu mwekezaji wa *Cristal Resort* ameweka *Court Injunction* asiingie ndani, lakini hajazuia kwamba asilitumie eneo lake sasa anapokwenda anakuwa anamzuia. Sasa suala hili Mhe. Mwenyekiti haliko mahakamani.

Nadhani na ndio hapa nikasema Mhe. Mwanasheria Mkuu na Waziri wa Katiba na Sheria wanisikilize vizuri, ili waweze kunisaidia hizi *Court Injunction* wakati mwengine hawa wawekezaji wanakuwa wanazitumia na halafu yale maeneo wao wanayatumia, lakini wale wenyewe maeneo husika hawapati na hichi ni kitu ambacho si halali.

Kwa maana hiyo, kama kuna *Court Injunction* hasa kwenye hayo mageti, ina maana eneo lile hata na yeye asilitumie mpaka maamuzi ya mahakama, lakini hoja yangu bado inarudi kwamba eneo hili la ndugu Mudrik tumekwenda na watu wa ardhi na limo kwenye ramani yake aruhusiwe kuliendeleza na hiyo ndio hoja yangu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Hamza Hassan Juma ndio tunamsikia anasema suala hilo na nature ya hiyo kesi ambayo iko mahakamani sisi hatuijui, isipokuwa tunajua kwamba sehemu hiyo iko mahakamani.

Lakini yeye anasema kwamba huyo mwenye hiyo hoteli ya *Cristal Resort* amekubali kwamba hizo nyumba ziko kwenye eneo la Mudrik, basi kama amekubali basi hiyo ni kesi rahisi avunje kama amekubali na wala sio suala la kungojea suala la umamuzi wa mahakama, isipokuwa avunje tu na sio suala jengine. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nafikiri kuna haja ya suala hili kulifuatilia zaidi. Kwa hivyo, mimi na Mhe. Hamza Hassan Juma tulifuatilie suala hili, ili na mimi anielimishe zaidi juu ya suala hilo la wala si vibaya.

Kwa hivyo, mimi nakubali kama mtu anatumia ardhi ambayo hajapewa basi ni kuvunja ndio na tayari tumeshavunja baadhi ya maeneo, kwa sababu utatumia mahala ambapo hujapewa kwa nini na wala si pako na mwenyewe hataki, isipokuwa kama mwenyewe ataamua chukua na hilo ni suala jengine, lakini kama hajaamua basi ni kuvunja tu. Mhe. Mwenyekiti, nadhani tulifuatilie zaidi na tuangalie taratibu zetu za kisheria na kila kitu, ili tujue tunafanya nini.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, unajua chombo chako hichi ni kikubwa sana na tatizo wanalopata wananchi wetu ni kwamba wanapata jawabu nzuri sana kama hizi. Lakini sasa kuanzia hapo nani mwenye mamlaka ya kumvunjia yule mwekezaji aliyejenga ndani ya eneo la mzalendo, maana yake hapa mwananchi atakuwa amekunja mikono anaisubiri serikali na huyu mtu amekiri kwamba hizi nyumba kweli nimejenga ndani ya eneo la ndugu Mudrik na yeye ndugu Mudrik anashindwa kulitumia eneo lile.

Sasa je, nani atakayechukua hatua hii au Idara ya Ardhi inachukua dhima ya kulishughulikia hili suala ambalo amelizungumza Mhe. Waziri baada ya kulifuatilia kwa kina. Mhe. Mwenyekiti, baada ya kulifuatilia kwa kina kwa sababu tulipokwenda tulikwenda na watendaji wake wa Idara ya Ardhi na michoro ya ramani zote wanayo, huyu mwekezaji wa *Cristal Resort* ramani yake ilipofika wanayo na huyu ndugu Mudrik eneo lake lilipofika wanayo.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri anisaidie nani mwenye kuchukua hatua hii kwa sababu huyu mzalendo Mhe. Mwenyekiti kama nitakupeleka hata hayo maboti yake ambayo ameyaleta kwa ajili ya kuwekeza yameshaoza kutokana na mwekezaji huyu ambaye amemuzuia asilitumie eneo lake.

Kwa hivyo, ninahitaji maelezo ya zaidia kwamba nani atakayechukua hatua hii, maana yake laiti kama ingelikuwa kamati inaruhusiwa kwenda kuvunja basi sasa hivi tukitoka tu tungekwenda kutia mafuta *bulldozer* na tukaelekea Paje hivi sasa.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, sijui kama hiyo hoja nimeifahamu sawa sawa, lakini kuna *Court Injunction* kwa upande mmoja, lakini *Court Injunction* hiyo haihusiani na eneo hilo. Sasa kama huyu jamaa yeye amezuiwa na huyu mwekezaji kwa kutumia mwamvuli wa ile *Court Injunction*, basi yeye achukue hatua ya kumshtaki huyu, inavyoonekana hapa na kama nimeifahamu sawa sawa hii hoja.

Kwa kweli yeye huyu anadhulumiwa na huyu mwekezaji kwa maelezo uliyoyatoa, sasa kama anadhulumiwa na huyu mwekezaji na wala haihusiani na ile *Court Injunction*, basi sasa huyu aende mahakamani na nadhani ndio utaratibu wake. Kwa hivyo, lifanyieni kazi pamoja na Mhe. Waziri, lakini kwa nilivyofahamu mimi inakuja katika sura hiyo, maana

vyenginevyo Mhe. Waziri hataweza kuchukua hatua ya kuvunja na yule anaendelea kudhulumika na mwekezaji anatumia mwamvili wa *Court Injunction*.

Sasa Mhe. Mjumbe, kumbe unatuambia *Court Injunction* haihusiani na kama haihusiani na bado anaendelea kudhulumika, basi achukue hatua za kisheria yeye sasa ninavyoona mimi na sijui Mhe. Mwanasheria Mkuu kama anayo maelezo, lakini kama nimefahamu vizuri mimi nahisi iko hivyo.

Mhe. Waziri kuna maelezo zaidi.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, jibu langu lilikuwa liwe hivyo, lakini tayari umeshanisaidia ninakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, hapo tulipokwenda ukiacha huyu ambaye amemzuia asijenge kuna eneo jengine mwekezaji huyu wa *Cristal Resort* amemzuia mtu hivi sasa mwaka wa 7 na ngoma iko huko mahakamani.

Sasa huyu baada ya hiyo miaka na huyu ameshazuiliwa hivi sasa unafika na yeye mwaka wa tato na leo akaanze kufungua kesi mahakamani, kwa sababu huko mahakamani huyu hivi sasa ana *Court Injunction* karibu nne, yaani huko mahakamani ndio kwao. Mhe. Mwenyekiti, ndipo pale niliposema kwamba namuomba Mhe. Mwanasheria Mkuu pamoja na Waziri wa Katiba na Sheria watusikilize pamoja na kutusaidia, ili wananchi wetu wapate afueni. Kutokana na hali hii, ina maana huko mahakamani ndio chaka la wawekezaji dhidi ya wanyonge. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, juzi Mhe. Salmin Awadh Salimn nilimsikiliza sana na alisema kwamba leo wananchi wanaacha vyombo tulivyoviweka vya Kikatiba wanakimbilia Baraza la Wawakilishi kudai haki zao.

Sasa mimi nafikiri Mhe. Mwanasheria Mkuu, Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati amenisikiliza, nafikiri tutalipatia ufumbuzi si muda mfupi na wala hatutaingilia uhuru wa mahakama, isipokuwa utauacha vile vile na *Court Injunction* ziendelee miaka 10, 15, 20, 30 na wananchi wanaatilika wacha ziendelee kukaa, lakini haya ambayo yanatekelezeka, basi tutashirikiana na vyombo hivi kwa ajili ya kutatua matatizo haya. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri aniahidi tu kwamba atashirikiana na mimi katika hili, ili kuweza kulipatia ufumbuzi bila ya kuingilia amri ya mahakama. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, mimi mwenyewe nilisema kwamba niko tayari kushirikiana naye, isipokuwa ninaweza kupata kikwazo tu ikiwa kumeingia mahakama, kwa sababu mahakama lazima imalize kazi yake. Kwa hivyo, niko tayari kushirikiana na yeye lakini kama kuna kikwazo cha mahakama nitakuwa sina cha kufanya. Mhe. Mwenyekiti, niko tayari kushirikiana naye kikamilifu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, shirikiana na Mhe. Waziri kama ulivyoomba. Tunaendelea.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, ahsante na mimi ninasema kwa kuweka hansard sawa maana ninajua nitakwenda na mwisho utaniambia, lakini hansard najua itakuwa inaweka kumbukumbu zangu vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, nataka kupata maelezo kwenye fungu hili la 0901 Idara ya Ardhi ya Usajili nakwenda kwenye kifungu 220701, 220102 kuhusu matengenezo madogo na mkubwa ya ofisi kama ambavyo nilivyohoji kwenye Idara ya Nishati iliyopita. Mhe. Mwenyekiti, narejea tena kwamba mafungu haya ingawa Mhe. Waziri anasema si sahihi lakini mimi naendelea kusema kwamba yamewekwa wekwa.

Kwa mfano, utakuta kuna shilingi milioni 8,000,000/= kwa ajili ya matengenezo madogo na shilingi milioni 14,000,000/= kwa ajili ya matengenezo makubwa. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti atusaidie maelezo kwenye mafungu hayo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema kwamba mapendekezo haya yahakupachikwa na kama angekuwa na nafasi akenda kutembelea hilo jengo la Idara ya Ardhi na Usajili akaona jinsi ilivyofanyiwa matengenezo, kwa sababu matengenezo makubwa yapo na yanaendelea pamoja na yale madogo madogo ya ndani ya ofisi yanaendelea. Kwa kweli lile jengo limetengenezwa vizuri sana, basi angalie tu na wala hayakupachikwa.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, mimi sijamfahamu Mhe. Waziri na sijui amekusudia vipi. Kwa kweli mimi ninachosema au hoja yangu ni kwamba tunatenga mafungu mawili katika kazi moja, maana hayo matengenezo makubwa ni matengenezo ya hilo jengo pia na matengenezo madogo ni ya hilo jengo. Sasa kinatengenezwa kipi kiwe kidogo na kipi kiwe kikubwa, kwa sababu kama unatengeneza matengenezo makubwa basi na yale madogo yanaingia mule.

Kwa hivyo, unapotenga fedha kwa ajili ya mafungu mawili tofatui yaani matengenezo madogo na makubwa ah! Mimi ndio nikawa ninasema fungu hili moja linakuwa halina sababu ya kuwepo. Mhe. Mwenyekiti, ninaona fungu hili la matengenezo madogo hakuna haja ya kuwepo, kwa sababu matengenezo makubwa yanafanyika, kama unafanya matengenezo makubwa basi matengenezo madogo ya kazi gani wakati makubwa ndio yanajumuisha na hayo madogo, kwani yawepo madogo ndio yapatikane hayo makubwa.

Sasa mimi nadhani kama tunatengeneza nyumba au unaifanyia *repair* yote basi huna haja ya kusema kule chooni kunatakiwa fungu lake mbali maana yake matengenezo yake madogo wakati matengenezo ni matengenezo yote kwa pamoja na hoja yangu iko hapo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, mimi nilisema hapa na tukizungumza hapa ndani hatutaelewana labda Mhe. Mjumbe tumepeleke kwenye jengo la ardhi akalitizame na tumuoneshe sehemu gani iliyofanywa matengenezo madogo na makubwa na huko ataridhika, lakini kwa hapa ndani naona hatoridhika.

Kwa hivyo, ninavyosema ni kwamba matengenzo makubwa na madogo yapo na taarifa nimeletewa hapa, kwamba kuna matengenezo ya ndani ambayo ni madogo madogo na yale mengine ya *overall* yale ya jengo lenyewe lote. Mhe. Mwenyekiti, nadhani kama haturipo kwenda pale hatoona ile hali halisi ya matengenezo yenyewe.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, nafikiri suala hili linakaribia kufika mwisho lakini muda wetu hauturuhusu na wacha tulitolee maelezo moja kwa moja na halafu tuombe muda.

Mhe. Mjumbe, nadhani suala hili hebu mashauri ya Mhe. Waziri, maana kuamua jambo katika sura hii kuna uzito wake, basi tukaona hayo matengenezo makubwa na madogo, kwa sababu anasema yote yapo, basi ni vyema tukaone.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kazi bado haijamalizika na muda umebakia mchache. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa kazi ya Kamati ya Matumizi ya kupitia mapato na matumizi bado haijamaliza kazi yake na kwa kuwa muda uliopo mbele yetu ni mchache. Kwa hivyo, naomba Baraza lako litengue Kanuni ya Muda, ili ituwezeshe kumaliza bajeti hii ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda na leo hoja imekubaliwa. *(Vicheko/Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

KAMATI YA MATUMIZI

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tumeishia kwamba Mhe. Mbarouk Wadi Mussa anafuatana na Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwenda kuangalia hayo matengenezo makubwa na madogo. Kwa kweli hii ni ile kutokana na kwamba

umepata nafasi ya kupata maelezo na pia Mhe. Waziri uweze kuthibitisha yale anayoyazungmza kwenye fungu hili basi muende huko. Tunaendelea.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa, tunaendelea.

Kifungu 0901	Idara ya Ardhi na Usajili	312,250,000/=
Kifungu 1001	Idara ya Upimaji na Ramani	

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, naendelea kukushukuru kwa kunipa nafasi hii tena, ili nipate ufafanuzi wa ziada kutoka kwa Mhe. Waziri hasa katika hoja yangu ya yule mwekezaji ambaye ana mradi wake wa kujenga kiwanja kidogo cha ndege cha kufundishia marubani.

Sasa Mhe. Waziri katika maelezo yake alieleza kwamba huyu mwekezaji wamemtaka atafute watu wa *TCAA*, ili kuweza kupata ufafanuzi wa kutosha katika huu mradi wake. Lakini hoja yangu Mhe. Mwenyekiti, kwamba huyu mwekezaji amepeleka maombi yake kwa muda mrefu na kwa bahati amepata maelekezo mbali mbali kutoka ndani ya vyombo vya serikali ikiwemo pamoja na *ZIPA*, ambao wao wamesema hawana tatizo la mradi wakea, ambapo *document* ameniletea ninayo hapa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa ninavyofahamu kwamba sisi tumeanzisha hii Taasisi ya *ZIPA* pamoja kwamba haiko kwenye eneo lake, lakini pale *ZIPA* kuna watu wa Ardhi, Mipango Miji, Mazingira, yaani taasisi zote zipo pale. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, huyu mwananchi baada ya kupewa tama kwamba mradi wake unatekelezeka basi amekwenda na kuzungumza na wananchi wape na ameshawalipa fidia na leo anaambiwa kwamba mradi huu ndio kwanza aanze kufuatilia upya.

Kutokana na hali hiyo, naomba kupata maelezo ya ziada, ili niweze kuliruhusu fungu hili. Kwa kweli hofu yangu Mhe. Mwenyekiti, kwamba huyu mwekezaji tayari anazo hizo ndege ambazo anazozifundishia hao marubani na jana nilitoa takwimu karibu marubani 53 tayari ameshafundisha na 32 miongoni mwa hao ni wazanzibari. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa hiyo sehemu aliyokodi, yaani amekodi hanga lile ambalo tunalolizungumza na Mkurugenzi wa Mamlaka ya Uwanja wa Ndege na wao ndio wanaotakiwa kutoa *do ahead*, kwamba huyu huu mradi wake uendelee au usiendelee. *(Makofi)*

Sasa leo tutegemee kwamba huyu mwenye mamlaka ambaye ndiye yeye aliyemkodisha huyu akiweza kutoa *authority* ya kuweza eneo la kule ina maana huku atahama na atakosa kodi. Kwa hivyo, ndipo pale tulipozungumza kwmaba mtu anapokuwa katika dhamana basi asiwe na kitu ambacho kinachokuwa na maslahi yake na matokeo yake ni miradi kama hii inakwamishwa bila ya sababu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo kwa nini mwekezaji huyu anazuia mpaka leo hajaruhusiwa kuanzisha huo mradi wake wa kurusha ndege za kufundisha marubani.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mhe. Hamza Hassan Juma kwa ukakakamavu wake, lakini nasema kwangu mimi ni ardhi, sasa ardhi inategemea wanataka kufanya nini, wanataka kujenga kiwanda cha ndege kuna masuala ya usalama huko angani na pia usalama wa nchi kwa jumla na lazima nipate ripoti ya *TCAA* na bila ya hivyo kutoa ardhi mimi itakuwa ngumu.

Vile vile nakubali kwamba amesema kwamba *ZIPA* wapo watu wa ardhi, lakini mimi kama sijapata ile ripoti ya *TCAA* nitatoa vipi kibali, kwa sababu kwangu ni kutoa ardhi na wala sina tatizo wakati mradi wenyewe unakwenda kwa mujibu wa taratibu na yeye mwenyewe alifanyiwa mkutano huyu na watu hawa wote walikuwepo na walizungumza na akakubali kwamba hiyo kazi anaifanya na ataleta jibu baada ya kukamilisha.

Kwa hivyo, ametoka pale kwamba wanaendelea kwenda kufanya kazi hiyo na sisi tunangojea tupate jibu au hizo taarifa kutoka huko na sisi tukipata taarifa kutoka huko basi sisi hatuna matatizo na suala hilo Mhe. Mwenyekiti.

Nadhani hilo ndilo jawabu la swali hili na Mhe. Mjumbe ajue tu kwamba ardhi ipo na huyu bwana tayari ameshalipa fidia na ninachotakiwa mimi ni kumtilia saini hati yake ya ardhi. Mhe. Mwenyekiti, kama sikupata taarifa hizi za *TCAA* kwa ajili ya kujenga kiwanja cha ndege basi siwezi kuruhusu. *(Makofi)*

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu ninaijenga zaidi katika *conflict of interest*. Mhe. Mwenyekiti, *TCAA* lazima wawasiliane na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ndio wenye *authority* ya kusema *allocation* gani iweze kuwekwa hicho kiwanja cha ndege na huyo bosi ambaye yeye atatakiwa atoe maoni yake yeye amemkodisha huyu mwekezaji hizo ndege zake zimo ndani ya banda lake, hivi kweli ataweza kutoa *comments* za kuruhusu huyu ajenge kiwanja chake na ile kodi aikose na wala si rahisi, kwa sababu hapa kuna *conflict of interest*.

Mhe. Mwenyekiti, narejea tena na kwamba suala hili huyu mwekezaji ameshahangaika sana na ningelifurahi zaidi angelikuwepo Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano kwa ajili ya kuweza kutusaidia suala hili.

Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, ndio maana nikasema na sisi tulipoanzisha ile *ZIPA* tulisema, kwamba wale Wajumbe wa *ZIPA* waende pale watu wenye maamuzi, sasa leo kama *ZIPA document* imeshamwambia mradi huu hauna matatizo na taasisi zote ziko pale *ZIPA*. Sasa mtu huyu au mwekezaji amekula hasara mpaka anakwenda kuwalipa wananchi na leo dakika za mwisho aje aambiwe kwamba mradi huu hauwezi kufanyakazi hapa.

Nadhani Mhe. Mwenyekiti, labda nipate maelezo ya ziada lakini hoja mimi kwa kusema *TCAA* hawawezi wakatoa *authority* bila ya kupata mamlaka ya ZAA. ZAA huyo bosi ndiye aliyemkodisha huyo muwekezaji ndege zimo ndani ya banda lake kila mwezi anakula hela ataweza kusema basi hilo eneo ni salama apewe. Naomba maelezo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Hamza Hassan, hoja anayoijenga Mhe. Mwenyekiti, ipo nje ya uwezo wangu. Uwezo wangu miye ni kutoa hati ya kutumia ardhi. Sasa anajenga hoja ambayo ipo nje ya uwezo wangu, labda angeisubiri Wizara ya Mawasiliano wakaelewano lakini mimi siwezi kumjibu vyengine. Mimi nikipata a*uthority* ya TCA kiwanja kipo nitatoa, sina matatizo katika hilo. Sasa kama kuna *conflict of interest*, mimi sina hakika ya hilo, namsikia Mhe. Hamza anasema.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nadhani kwa mujibu wa utaratibu kalieleza vizuri Mhe. Waziri kwamba mwenye mamlaka haya ya kutoa kibali cha kujenga uwanja wa ndege ni Mamlaka ya Usalama wa Unga yaani (*Tanzania Civil Aviation Authority*) wao wanaweza wakatafuta uhalali huo. Ukitizama kwa mujibu wa ile sheria yenyewe ya Viwanja vya Ndege. Maana yake tulipitisha sheria mbili hapa Sheria ya Mamlaka ya viwanja vya Ndege ambayo yeye mamlaka yake Mkurugenzi Mkuu zaidi ni kusimamia viwanja vya serikali. Tukapitisha na sheria nyengine ya Viwanja vya Ndege ambayo mamlaka katika sheria ile yamempa zaidi Waziri sio Mkurugenzi Mkuu. Mimi nadhani angetusaidia hata ukitizama hii sheria yenyewe ya viwanja vye ndege kuna kifungu kipo wazi kabisa kuhusu mamlaka ya Waziri kuhusiana na masuala ambayo yanatakiwa na mamlaka ya viwanja vya ndege.

Mimi nadhani suala jepesi angetusaidia Mhe. Hamza kwamba kweli huyu mtu kumetakiwa maelekezo ya Mamlaka ya viwanja vya ndege na imekataa. Kwa sababu Mhe. Waziri wa Miundombinu anayomamlaka ya kutengua hayo mamlaka ya Mkurugenzi Mkuu chini ya hiyo sheria ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. Lakini suala hili la kujenga kiwanja cha ndege halishughulikiwi na Sheria ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege inashughulikia na Sheria ya Viwanja vya Ndege, ambavyo tulivipitisha kwa pamoja ambayo mamlaka yapo kwa waziri. Kwa hivyo wasi wasi wake naomba niuondoe kwamba mamlaka yapo kwa waziri zaidi kuliko ya Mkurugenzi Mkuu.

Lakini la pili hili analolisema kwamba *conflict of interest* ninavyokumbuka mimi na tulitakiwa mimi binafsi kulisimamia ni kuhakikisha Mkurugenzi Mkuu kwenye ile kampuni ambayo ndiyo ilikuwa imekodisha lile henga lenyewe, yeye mwenyewe ajitoe. Aliambiwa *pacifically* tuliambiwa tumwambie, tukamwita na amejitoa. Kwamba ama achague kazi ya serikali au achague hizo hisa zake katika Kampuni. Akaamua kuchagua kazi ya serikali. Sasa kama hilo bado halijafanyika au anahisi kwamba bado atakuwa na *conflict of interest.* Mimi nadhani suala ambalo tunaweza tukakaa tukaliangalia na kushirikiana ili kulitatua. Mimi silioni kama linatatizo kwa kushirikiana na Wizara yenyewe ya Miundombinu na sisi Ofisi yetu ambayo tulipewa ya kuhakikisha hiyo *conflict of interest* inaondoka kwa Mkurugenzi Mkuu.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, huu Mwezi wa Ramadhani na mimi nimefunga, hajajitoa bado anamiliki kwa sababu yeye ndiye anayepatana mpaka na hiyo kodi na huyo muwekezaji. Sasa kama huko kakwambieni kama keshajitoa, hajajitoa. Na katika kupatana na huyu muwekezaji na huyu muwekezaji sasa hivi tatizo lake anaona kwamba kule akihana yule bwana atakosa mapato. Hilo bado naliachia serikali kama ilivyo, lakini mimi kitu ambacho ninachotaka kukisema ndio maana nikasema kwa bahati

Waziri wa Miundombinu hayupo, yeye Waziri wa Miundombinu kafika kumuhakikishia huyu muwekezaji kwamba yeye hana tatizo na hilo, tatizo watu wake wa Mamlaka. Ndio maana nikasema jamani haya mambo mtu unajua ukimuuliza atakujibu vile anavyoona yeye, lakini sivyo katika utendaji.

Mimi naomba Mhe. Mwanasheria Mkuu hiyo kazi uliyopewa uendelee nayo haijakamilika katika hili eneo la *conflict of interest.* Mimi bado Mhe. Mwenyekiti, nadhani kwa kuwa Waziri hayupo na kwa kuwa yeye ana uwezo wa kufanya maamuzi kama mamlaka au ya sehemu nyengine. Sasa uniruhusu niendelee kujakuzuia fungu hili katika Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na Uchukuzi. Ukiniruhusu hapo Mhe. Mwenyekiti, nitakaa kitako, hujaniruhusu hapo itabidi tuahirishe Baraza mpaka atakapokuja Waziri wa Miundombinu aje atoe jawabu.

Mhe. Mwenyekiti: Sikushawishi uje uzuie ila kama kuna haja ya kuzuia hilo litakuwa lipo juu yako. Lakini lile ambalo Mhe. Waziri halipo katika mamlaka yake nadhani yeye tumuachie aendelee. Sasa utaangalia kama wakati huo maelezo yatakuwa mazuri au si mazuri utajua hapa nimzui huyu, nimbane hiyo utatizama wakati huo, tunaendelea.

Kifungu 1001	Idara ya Upimaji na Ramani	355,211,000
Kifungu 1101	Idara ya Nyumba na Makaazi	227,818,000
Kifungu 1102	Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba	24,000,000
Kifungu 1201	Mahkama ya Ardhi	190,632,000
Kifungu 1301	Idara ya Uendeshaji	

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nipo katika kifungu 1301 nilikuwa nataka maelezo kidogo kwa Mhe. Waziri kwenye mafungu mawili haya kuna fungu la 220603, Ununuzi wa Samani, Viti na Makabati, kuna milioni 30 zilizotengwa. Mwaka jana kulikuwa kuna milioni11 na mwaka juzi kulikuwa kuna milioni 10. Fungu 220701 Kwenye Matengenezo Madogo ya Ofisi narudi tena pale pale kuna milioni 32. Nilikuwa nataka maelezo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, kwa kumjibu swali lake namwambia tu kwamba mwaka jana tulikuwa tuna ununuzi wa thamani milioni 11. Lakini ajue kwamba kulikuwa na mchango wa meli kwa hiyo milioni 11 ilikwenda kwenye meli. Mwaka huu tumeweka hizo milioni 30 kwa ajili ya ununuzi wa thamani ya Ofisi Kuu pale tulipo sisi wenyewe thamani zimeshachoka sana, ni lazima tufanye marekebisho katika ofisi nyingi na kuna ofisi nyengine ni pale ni mpya, kwa hiyo tunaongeza pale.

Halafu matengenezo madogo madogo ya ofisi, tumekaa, tumefikiri, tumeona tunakuja kwenye sherehe ya miaka 50 ya Mapinduzi basi jengo letu liwe vile lilivyo? Kwa kweli lina hali ngumu ukilitizama jengo la Wizara ya Majenzi. Ukitokea kule Serena ukija pale utashangaa sana ukiambiwa kwamba hii ndio wizara, utashangaa sana. Kwa hivyo tumeambiwa tuifanyie matengenezo angalau madogo kuisafisha safisha kwa ajili ya Sherehe za Miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, kwenye hili fungu la mwanzo la ununuzi wa samani na viti na makabati naona limenitosheleza maelezo ya Mhe. Waziri kwamba mwaka jana hakuwa amepata kitu kwa sababu ziliondoka kwa hiyo mwaka huu anaamua kwamba atanunua, mimi sina tatizo.

Kwenye hili fungu la pili hapa labda kidogo angetusaidia Mhe. Waziri maana milioni 32 sijui kazi zipi ambazo anakusudia kuzifanya katika kipindi hichi. Sherehe za miaka 50 kweli zipo lakini isiwe sherehe tena ikawa tunashereheka kwa kuongeza mafungu ya fedha. Hebu atupe kidogo kazi anazokusudia kuzifanya katika kipindi hichi.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, amepata nafasi ya kupita akaiona ile Wizara? Inatisha hivyo, kwamba ndio Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, inahitaji kufanyiwa matengenezo ile, ili angalau kwenye miaka 50 iwe ile nyumba kidogo inatizamika. Angalau angeniomba *break down* ningeona kaniomba kitu kizuri ningemwambia *break down* yake tunatengeneza nini na nini. Lakini jengo ni lazima tulitengeneze lile Mheshimiwa liko hali mbaya, ni lazima tulifanyie matengenezo, hizo 32 sijui kama zitatosha lakini sisi tutazitumia hizo hizo katika kipindi hichi.

Kifungu 1301	Idara ya Uendeshaji na Utumishi	781,509,000
Kifungu 1401	Msajili wa Ardhi	

Mhe. Hamza Hassan Juma: Kwanza namshukuru sana Mhe. Waziri kwa utaratibu aliouanzisha wa kusajili ardhi za wananchi. Suala hili kama likiweza kufanikiwa vizuri basi litaweza hata kuwasaidia wananchi wetu katika kushirikiana na wawekezaji mbali mbali kwa yale maeneo ambayo wanayamiliki wao wenyewe.

Sasa nina mambo matatu, lakini haya mawili nitamuomba Mhe. Waziri nitamtafuta kwa wakati wake ili tuweze kushirikiana na ikiwezekana hata kulikabidhi Kamati yake kulishughulikia. Suala la Nungwi ni lile suala la wananchi wa Mchangamle, hili tutalifatilia kwa utaratibu ili nisimchoshe Mhe. Waziri. Hapa nilikuwa nazungumza zaidi suala la jimbo langu, tayari nina miradi mitatu na kiwanja kimoja.

Mhe. Mwenyekiti, mimi Mhe. Waziri wanaponipa viwanja kwa ajili ya maendeleo ya wananchi basi huwa sisiti najenga miradi ya wananchi. Nina miradi mitatu na nina kiwanja kimoja ambacho sijapatiwa hati. Kama alivyosema Mhe. Ussi Jecha, tatizo sasa hivi sio pesa, tunaishukuru serikali sasa hivi inatuwezesha hawa kwa mambo yanayowagusa wananchi. Niambie tu Mhe. Waziri lini nikalipe ili waweze kunipatia hati miliki za miradi yangu ya juu. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, ninachotaka kumwambia Mhe. Hamza Hassan Juma, hicho kiwanja chake kimeshapimwa na tayari kina *site plane*. Kama kimeshapimwa na kina *site plane* basi hiyo ndiyo huletewa mimi kwa kutia saini ya hiyo hati yake ya matumizi ya ardhi. Akinijibu kama kimeshapimwa na kimeshatengewa *site plane* na kama ipo tayari waulize watu wako wailete nikutilie saini. Mimi saini yangu sio ghali kiasi hicho, ukishakufuata sheria tu basi.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Nakubaliana na Mhe. Waziri kweli saini yake wale sio ghali maana yake gharama iliyoandikwa na serikali ndiyo ile ile ambayo tunayolipa. Hichi kiwanja kimekwisha kupimwa kwa muda mrefu na *bicorn* zipo. Bahati mbaya kama yalivyo majengo mengine hati bado hatujapewa. Kwa bahati sasa hivi ndio kama hivyo tumeshawekeza. Sasa ukijenga skuli ya wananchi unaweza ukapata muwekezaji akataka kuiendeleza kwa kushirikiana na wananchi. Kwa hiyo kama hatuna kitu mkononi, watasema ile skuli sio yetu, itakuwa tuna skuli hewa au hospitali hewa.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani sasa hivi Hospitali ya Kwamtipura unaijua hadhi yake ilivyo, ipo katika *standard* ambayo mtu yeyote akipata *pressure* anaweza akalazwa na akatibiwa wala hakuna kunguni wala wale mende wasiokufa wale hawamo. Mimi nafikiri tukishakupata hati miliki tunataka kujiendeleza zaidi na hasa sasa hivi kuna benki unaweza ukawekeza hati yako pale ukaweza kupata nguvu za kuweza kufanyia na mambo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, akinambia hayo yote yanaweza kufanyika manne nitaweza kumlipa mara moja ili tuweze kupata hizo hati halafu baadaye tuendelee.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, juzi hapa kulikuwa kuna tatizo la Mhe. Thuwaibah Edington Kisasi ana ardhi anataka kujenga Skuli, na mfadhili ni Wachina. Basi ilitengenezwa *site plane* ameleta nimeshasaini nimeshampa na kazi ya ujenzi inaendelea. Ilikuwa ijengwe skuli ya chini lakini wamekubaliana kwamba watajenga skuli ya ghorofa, wamekubaliana wenyewe na kazi inaendelea.

Mhe. Hamza Hassan Juma, tupo karibu tunapishana kila mara hapa ngazini, issue hiyo kwa nin hujaniletea nikamaliza. Mheshimiwa nasema tena mimi nilikuwa mwakilishi wa jimbo nayafahamu hayo, kwa hivyo angeniletea tu wala si suala la kuja kunililia hapa ingelikuwa tumeshalimaliza zamani hilo. Lakini tufate sheria hicho ndio kitu muhimu, ukishakufata sheria mimi sina matatizo, lete tu Mhe. Hamza.

Kifungu 1401	Msajili wa Ardhi	190,914,000
Kifungu 1501	Idara ya Mipango Miji	309,568,000
Jumla ya fungu		**7,519,000,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 25 - WIZARA YA ARDHI, MAKAAZI, MAJI NA NISHATI

Kifungu 0491	Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	59,571,530,000
Kifungu 0801	Idara ya Nishati	6,870,000,000
Kifungu 1001	Idara ya Upimaji na Ramani	3,279,500,000
Jumla ya fungu		**69,721,030,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirejea)

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha ya Wizara yangu bila ya mabadiliko sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali mabadiliko haya.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe niwahoji wanaoafiki makadirio hayo wanyanyue mikono, wasioafiki, walioafiki wameshinda.

(Hoja ilitolewa Iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Katika hatua hii basi naseme *offweeee*! Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni kwa kazi nzuri tuliyoifanya kwa mashirikiano makubwa na sasa niakhirishe Kikao hichi hadi kesho tarehe 16/7/2013, saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 8:20 mchana Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 16/07/2013 saa 3:00 za asubuhi)